ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Tatu – Tarehe 13 Machi, 2015

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Naibu Spika: (Ali Abdallah Ali) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 6

Ubovu wa Barabara ya Hospitali ya Chake Chake kupitia Soko la Qatar

Mhe. Saleh Nassor Juma: - Aliuliza**:-**

Barabara mbovu, pamoja na zogo la watu na magari katika soko la Qatar lililopo Chake Chake limechangia sana uchafu pamoja na uwezekano wa kutokea ajali katika eneo la soko hilo. Kwa kuwa Baraza la Mji wa Chake Chake mara nyingi huvuka malengo katika kukusanya mapato kutoka kwa wananchi wa Mji huo kwa kuwa ni wajibu wao kulipa kodi.

Je, ni lini Baraza la Mji wa Chake Chake litatimiza jukumu lake kwa walipa kodi wa Mji huo kwa kutengeneza ile nusu kilomita ya Barabara ya Hospitali ya Chake Chake kupitia soko la Qatar hadi barabara kuu ya Chake/Tibirinzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli barabara inayoanzia Hospitali ya Chake Chake kupitia soko la Qatar hadi Barabara Kuu ya Chake/Tibirinzi haiko katika kiwango cha kuridhisha, hii inatokana na kuwa kwa muda mrefu haijafanyiwa matengenezo makubwa na ikizingatiwa kuwa ipo katika eneo la mteremko wa bonde na inatumiwa na magari mengi na uchakavu unakuwa kwa kasi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Mji Chake Chake limekuwa likifanya matengenezo madogo madogo mara kwa mara ili kuifanya barabara hiyo ipitike mwaka mzima, na hivi karibuni Baraza limefanya ukarabati wa njia hiyo kwa kiwango cha kuwekewa kifusi.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa tunawasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya kuitia lami, kutokana na fedha zitakazotoka Mfuko wa Barabara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Chake Chake ni uso wa kisiwa cha Pemba na ni sehemu ya biashara ya kile kisiwa na kwa kuwa sasa hivi kisiwa kile wanapenda sana wageni kukitembelea wakiwemo watalii na *mawatwani* (wananchi) hawa wengine ambao walihama zamani kwa maana ya *diaspora* na kwa kuwa barabara ile ni chafu sana kiasi ambacho siku za mvua harufu inakuwa kali sana katika soko lile kiasi ambacho hata wageni wanaona tabu kwenda kununua bidhaa pale kiasi ambacho hupata shida sana katika suala la kukudhi mahitaji yao kwa soko lile la Qatar.

(a)Je, hamuoni kwamba kuendelea kuchelewa kupata jibu kutoka Mawasiliano na kuweza kuwajenga kipande kile cha nusu kilomita cha barabara cha kiwango cha lami, si kuendelea kuwafukuza wageni katika nchi ile ambayo ni sehemu kubwa ya mapato katika nchi yetu.

(b)Kwa kuwa Baraza la Mji la Chake Chake linaongoza kwa kulipa kodi, yaani kila mwaka linazidi asilimia mia moja kwa kukusanya kodi pale. Hamuoni kuendelea kukusanya kodi na huku mkiwaachia wananchi wa pale wakipita katika matope na kununua bidhaa katika maeneo machafu machafu ni kufanya *betrayal* ya ile kodi yao wanayoilipa na hivyo kuwa hamuwatendei haki wananchi wa Chake Chake na wageni wanaiongia katika mji ule.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

(a)Mhe. Naibu Spika, kwanza majibu kutoka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tayari tumeshayapata na tumeyapata tatizo la wenzetu wa Miundombinu na Mawasiliano ni tatizo la ufinyu wa vifaa na ukizingatia kwamba Wizara hii ina majukumu sana ya kutengeneza barabara nchi nzima.

Kwa hivyo, tayari tumeshapata ahadi baada ya huko wanakofanyakazi sasa hivi wakimaliza watakuja kukitia lami kipande kile cha kutoka Chake Chake Hospitali mpaka Tibirinzi. Kama nilivyosema mwanzo fedha wenzetu wa Mfuko wa Barabara wanazo na zipo kwa ajili ya kazi zile.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba astahamili kwamba sisi tunalishughulikia jambo hilo na kama nilivyosema mwanzo kwamba sisi tumekuwa tukichukuwa hatua dharura kwa kutia kifusi. Hizo pesa ambazo amesema ni za walipa kodi ndizo tunazozitumia kwa kukodi magari na kukodi mabuldoza na kununua kifusi kwa ajili ya kuiweka ipitike ile njia katika kupindi chote kama nilivyoeleza katika suala langu la mwanzo.

(b)Mapato tunayokusanya zaidi ya asilimia mia moja ni kweli. Kiwango cha mapato katika Baraza la Mji wa Chake Chake kimeengezeka na kimeengezeka kutokana na Mkakati ambao tayari tunao wa kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zinakusanya zaidi kutokana na uhalisia wa mambo.

Kwa hiyo, mimi nataka nimuhakikkishe Mhe. Saleh Nasor Juma, kwamba fedha tunazozikusanya kutokana na ada mbali mbali zinazotokana na wananchi tunazirejesha kwa wananchi wenyewe wa kuwapelekea miradi mbali mbali ya Maendeleo. Kwa Chake Chake pesa hizi zimetumika nyengine kwa ajili ya uwekaji kifusi katika barabara hiyo inayotoka Chake Chake Hospitali kutokezea Tibirinzi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa barabara ile ni mbovu pamoja na juhudi ya kuingiza kifusi hicho ambacho unasema kwamba ipitike angalau kwa kipindi cha mwaka na kwa kuwa barabara ile imeambatana na mlima ambao inaponyesha mvua fusi lile linakokolewa na mvua na kuondoka kabisa.

Je, wizara yako ina mpango gani wa dharura kuiokoa barabara ile ili watu wanaolitumia soko lile na gari zinazopita barabara ile zipite katika hali ya usalama na kuokoa ajali ambazo zinaweza kutokea bila ya kutegemea hao wafadhili ambao wakimaliza huko ambako wanafanyakazi hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba wenzetu wa mfuko wa barabara wametupa pesa za dharura kwa ajili ya kuitia lami barabara ile kutoka Hospitali ya Chake Chake mpaka kutokea Tibirinzi. Sasa mpango ndio huo ambao tayari sisi kama wizara tumeshawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu wameshatupa ahadi, kwamba sasa tatizo sio pesa tatizo ni kusubiri wenzetu kuwastahamilia wamalize kazi waliyonayo na sijui kama hiyo kazi ambayo wanaifanya wenzetu wa Miundombinu kama haina maslahi na wote tuliomo humu ndani, maana wanashughulikia barabara zinazokwenda vijijini vile vile.

Lakini wametwambia kutokana na ufinyu wao ni vizuri tukawastahamilia wakitoka huko, watakuja pale Chake Chake ili waje waiweke lami. Mpango wa kuiweka lami ndio utakaondoa hilo tatizo la maji ya mvua kutoka kwenye mlima kwenda bondeni na kuiharibu ile barabara kila wakati. Kwa hiyo, nikuombe tuendelee kuwa wastahamilivu ili tuweze kufanya hiyo shughuli.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu, mchangamano wa soko la Chake Chake toka kuzaliwa hili soko la Qatar na ilizaliwa kutoka na msongamano wa magari yanayoingia sokoni *stand* pale pamoja na wafanyabishara wadogo wadogo kama wauza nyanya, vitunguu, mbatata na wengineyo.

Sasa soko hili kutokana na msongamano huo ilibidi wale wauza vitunguu na nyanya wakaweka Qatar, lakini wakati huo huo tulifanya kikao baina ya Mawasiliano na Taasisi mbali mbali zilizopo pale sokoni ili kufungua barabara nyengine ambayo kuwa gari zikiingia zitoke kwa mlango mwengine. Sasa ile kuingia na kutoka mlango mmoja ndio inayosababisha msongamano zaidi na tulifanya kikao na tukakubali, tukakagua eneo kwa ajili ya kufungua njia nyengine ili gari inayoingia isitokee mlango wa kuingilia.

Je, namuuliza Mhe. Waziri, suala hili kwanza analielewa na kama analielewa kwa sababu lilipofika hatua nzuri, kukawa kuna nyumba moja ikawa ni kikwazo. Je, hatua ile imefikia hatua gani na je, Mhe. Waziri, haoni kuacha kuwa njia ile inayoingia gari na kutokea ni ile ile jambo ambalo hupelekea msongamano Chake Chake sokoni utakuwa maisha haumalizi. Je, kama ni hivyo, ni lini hatua zitachukuwa ili kuingua gari zisitokee njia ile ile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, suala hili nalielewa baraza la Mji wa Chake Chake linao mradi wa kujenga *stand* ya kudumu katika eneo la Michakaeni. Bado watu wa Wizara ya Ardhi wanaendelea kufanya *Evaluation* kwa ajili ya kuwalipa fidia watu ambao tutawaondoa Michakaeni ili wapate pahala pa kuishi. Lakini vile vile wapo watu ambao wana viwanja Wizara ya Ardhi inafanya mpango wa kuwapatia viwanja vyengine ili watu hao waweze kuondoka pale bila ya matatizo yoyote na Serikali iendelee na mpango wake wa kujenga *stand* ya kudumu katika eneo la Michakaeini.

Lakini hivi sasa pia tunao mpango wa dharura ambao unachukuliwa na Baraza la Mji wa Chake Chake la kuhamisha *stand* na msongamano ulioko pale kuwapeleka wenye magari Chanjaani kwa ajili ya kunusuru na kuokoa tatizo liliopo pale.

Suala la kwamba barabara ya kutokea na kuingilia hii ni suala la ubishi tu wa madereva, lakini utaratibu upo toka zamani kwamba gari inayoingia Chake Chake kupitia Hoteli kwa jina la sasa inaitwa *Barclays* inatakiwa izunguke ama itokee Miembeni ama itokee Tibirinzi. Sasa jambo linalofanyika sasa la kutoa gari kutoka kwenye *Stand* ya zamani ya Chake Chake na soko la sasa la Chake Chake kwenye mnada kurudia Miembeni ni jambo linalofanywa kwa ubishi na madereva na hilo ni jukumu la Jeshi la Polisi, tutaendelea kuwasiliana na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha madereva wanaovunja sheria waweze kufata utaratibu wa sheria.

Lakini utaratibu uliopo na unaoeleweka kisheria kwamba gari inayoingia Chake Chake sokoni inatakiwa kama haiendi ndani iteremke Miembeni na kama inakwenda ndani basi irudie njia ya Tibirinzi, huo ndio utaratibu. Sasa tabia za watu tutaendelea kuwaelimisha ili waweze kufuata sheria. Ahsante sana.

Nam. 45

Ujenzi wa Viwanja vyengine vya Soka

Mhe. Saleh Nasor Juma: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Serikali imefanikiwa kujenga kiwanja cha Amani Unguja na Gombani Pemba kwa ajili ya mchezo wa mpira wa miguu na hivi karibuni vimetiwa nyasi za bandia.

(a) Viwanja hivyo vya Amani na Gombani vimejengwa mwaka gani.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanja vyengine kama hivyo.

(c) Je, Serikali imejipanga vipi kukarabati viwanja vya michezo vilivyopo ambavyo vinatumika kwenye ligi vikiwemo Bungi, Mwanakombo, Jambiani Mfumbwi na Kitogani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Kiwanja cha Amani kimejengwa mwaka 1969 na kuzinduliwa mwaka 1970 na Kiwanja cha Gombani kimejengwa 1987 na kuzinduliwa mwaka 1992.

(b) Mhe. Naibu Spika, Serikali inayo mipango ya kujenga viwanja vyengine kama hivyo hapo baadae kulingana na uwezo utakavyokuwa na kwa kuanzia Serikali itaujenga upya Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* ili uweze kutumika kwa ajili ya sherehe mbali mbali za Taifa na zaidi kutumika kwa michezo mbali mbali hapa Zanzibar.

(c) Mhe. Naibu Spika, Serikali haina mpango hivi sasa kuvikarabati viwanja vya Bungi, Mwanakombo, Jambiani Mfumbwi na Kitogani vinavyotumika kwa ajili ya kuchezea ligi. Mpango wa Serikali ni kujenga viwanja vya michezo vya Wilaya vitakavyokuwa na hadhi ya kuchezea michezo mbali mbali. Lakini kabla ya kujengwa ni lazima viwanja hivyo vipimwe na kutolewa hati ya umiliki.

Mhe. Saleh Nasor Juma: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza dogo sana kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wananchi vijana wetu katika maeneo ya vijijini wanapenda sana mchezo wa soka au kabumbu na kwa kuwa kukosekana kwa viwanja vya soka vya kisasa katika maeneo ya vijijini au *country side* ya visiwa hivi, nchi yetu inashindwa kabisa kuibua vipaji na kwa kuwa vipaji vingi vipo vijijini kwa mfano katika Kijiji cha Bungi, Mwanakombo, Jambiani na Mfumbwi katika Jimbo la Muyuni wamewahi kutoa vijana wengi waliochezea timu ya Taifa ya Zanzibar wakiwemo akina Salhina na Abdulwakati Juma, walitokea huko huko.

Je, huoni kucheleweshe kujenga viwanja katika maeneo ya Muyuni kule na mukaendelea kujenga hiki kiwanja hapa *Mao-Tse-Tung* wakati hapa mjini, hamuoni ni kurudisha vipaji vinavyotoka vijijini ambavyo vipo kwa wingi sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nimeeleza vizuri kwenye swali la msingi. Kama unavyojua Serikali na Wizara ina mikakati na kama nilivyoeleza tutajenga viwanja vya Wilaya, Mkoa wa Kaskazini Pemba tutajenga Kinyasini na Nungu kwa Unguja tutajenga na Mkoa wa Kusini pia tutajenga. Kwa sababu Mkoa wa Mjini/Magharibi viwanja vipo na kwa kweli kama nilivyoeleza kiwanja cha *Mao-Tse-Tung* kitajengwa mfumo wa kisasa na kiwanja cha Wilaya ya Micheweni pia na Wilaya nyengine tutajenga.*(Makofi)*

Sasa hivi Wilaya ya Wete kuhusu kiwanja cha *netball*, Wizara tayari imeshakwenda kukagua kwa ajili ya timu za *netball* kwa Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni pia kuna kiwanja kitajengwa kwa ajili ya *volleyball* na *netball* na michezo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekwishakujibu kwamba katika viwanja ambavyo vinatarajiwa kujengwa kimoja wapo ni Kiwanja cha *Mao-Tse-Tung,* kiwanja ambacho ni cha zamani sana. Sasa sijui Mhe. Naibu Waziri, anaweza kutwambia ni lini hasa ujenzi wa kiwanja hiki utaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni jana tu tulikuwa pamoja na Ubalozi wa China ili kuweza kukagua na kuweza kufanya tathmini kama nilivyoeleza kwenye swali la msingi la kikao kilichopita.

Mhe. Naibu Spika, jana tulikuwepo uwanja wa *Mao-Tse-Tung* na leo hii tunakwenda tena ili kushirikiana na wafadhili ili kuweza kukagua ili kuanza kujengwa kiwanja hichi. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri, swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, aliyoeleza kama kuna mpango wa kujenga viwanja vya Wilaya ili kuendeleza michezo. Lakini namuuliza Mhe. Naibu Waziri, viwanja vya michezo vinategemea na wachezaji kuhamasishwa na kupewa mafunzo ya ile michezo yenyewe. Ninamuuliza Mhe. Naibu Waziri wakati Zanzibar tuna mgogoro wa chama cha michezo na bado Mhe. Naibu Waziri alituthibitishia kama migogoro haijatatuka na wakati michezo inategemea vyama vile vya michezo kusimamia vizuri michezo.

Je, kwa sababu ya mgogoro huo haujatatuka, haoni Mhe. Naibu Waziri kama suala hili linarudisha nyuma michezo. Na je, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alituahidi kama watahamasisha michezo kila Wilaya ili kuinua vipaji vya michezo vya michezo katika nchi yetu, ni lini hasa wizara yake tutaona hiyo hamasa kwa nguvu kuwahimiza vijana wetu kuingia katika ajira ya michezo na ikawa kama ni ajira michezo kama wenzetu, ni lini hasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo langu la Micheweni kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, maelezo yote jana Mhe. Waziri alitoa, lakini nataka nikwambie Mhe. Mwakilishi, hamasa sasa hivi ipo na kama unavyojua Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna timu yetu ya Shaba, *Sharp Vita* na timu nyengine nyingi. Kwa kweli sasa hivi kuna vipaji vya kutosha na hata kwenye Jimbo lako la Micheweni vipaji vipo na kwa kushirikiana na wewe ili tuweze kuendeleza vipaji vya vijana wetu ili wawe na vipaji zaidi na wapate ajira na wapate shughuli nyengine za kujitegemea.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Mhe. Waziri majibu ya ziada.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na Mhe. Naibu Waziri amejibu vizuri sana, majibu yote isipokuwa kuna nyongeza naomba kuieleza kwamba kwanza ni suala la migogoro ya vyama vya michezo. Hili ni wajibu lugha iliyokuwa haipendwi sana na wadau wenyewe wa michezo kuhakikisha kwamba wanaondoa migogoro yao.

Baraza la Michezo la Zanzibar lina vyama 33 ambavyo imevisajili. Kwetu sisi vyama vyote hivyo ni sawa sawa. Kwa Wizara *ZFA* ni sawa sawa na Chama cha Karata, vyote kwetu sisi vina haki sawa. Kwa hivyo, ni jukumu la kila chama kuhakikisha kwamba kinaondoa migogoro yao ili Baraza la Michezo lipate nafasi ya kushirikiana na vyama husika katika kuondoa matatizo na katika kuendeleza mbele michezo nchini.

Jitihada kubwa inafanywa na inaonekana. Kuhusu kujenga viwanja vya michezo Mhe. Naibu Spika, hili ni jukumu letu wote. Nadhani Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wana nafasi nzuri katika hili, kuna baadhi ya Waheshimiwa naomba niwapongeze kwa jitihada ambazo wamezifanya. *(Makofi)*

Mmoja ni Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, amejenga kiwanja cha michezo kwenye Jimbo la Uzini. Ni jambo zuri. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, Baraza la Wawakilishi wengine waige mfano wa Mhe. Mohamedraza, ambaye amenitia moyo pia Mhe. Mahmoud Thabit Kombo wa Jimbo la Kiembesamaki na yeye ameanza. *(Makofi)*

Kwa hivyo, na yeye nimpongeze. Hivyo, ningefurahi pia Waheshimiwa wote wenye uwakilishi Mhe. Subeit Khamis Faki, kuona kwamba ameshirikiana na michezo kujenga viwanja vya kisasa vya michezo katika Wilaya zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, haya ni majukumu yetu wote, nadhani tushirikiane na Serikali kwa kuendeleza hilo.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Naibu Waziri na Mhe. Waziri. Katibu tunaendelea.

Na. 34

Tatizo la Kuzalisha "*Hormone*" ya Uzazi kwa Mama Wajawazito

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kabla jibu langu la swali la Na. 34 halijapata majibu, naomba pafanywe marekebisho kidogo hapa kwa kuongeza neno, hili neno liliopo katika *parandesi*, neno "*labour* "ambalo nimeliingiza katika *parandesi* liongezwe "*labour pain"* badala ya "*labour"* pekee.

Mama mjamzito hushindwa kupata uchungu, nimeandika neno "*labour"* ndani ya *parandesi,* lakini liingizwe neno "*labour pain"*.

Miongoni mwa matatizo yanayozorotesha afya ya mama na mtoto katika nchi yetu ni kushindwa kwa akina mama wajawazito kuhudhuria *clinic* kwa wakati kwa ajili ya kupima ujauzito na kupata ushauri wa kiafya, lishe duni na kutojifungulia katika vituo vya afya. Kwa kuwa kuna taarifa kuwa wakati mwengine mama mjamzito hushindwa kupata uchungu *(labour)* pamoja na uwezo wa kusukuma na kumtoa mtoto tumboni *(pushing),* siyo tu kwa kukosa afya, lakini pia kwa kushindwa kutoa *"hormone"* anayeitwa *oxytocin* na hivyo kushindwa mama mjamzito kupata "*labour*", jambo linaloweza kuzorotesha afya yake.

a) Je, taarifa hii ni ya kweli.

b) Kama ni ya kweli wataalamu wanaweza kuigundua hali hiyo kabla ya mama mjamzito kuingia kwenye chumba cha kujifungulia *(pre-natal detection).*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua fursa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia wote tukiwa katika Baraza hili leo na afya njema, tukiwa wazima katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kutoa taarifa kwamba suala hili tayari limeshajibiwa katika Baraza lako hili katika kikao chako cha 17, mwezi wa Oktoba, 2014 likiwa kama swali Nam. 13 na hivi sasa limejirejea tena, kidogo likiwa tofauti kupitia kwa Mheshimiwa huyu huyu Mhe. Saleh Nassor Juma.

Hata hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe maelezo tena kwamba hii *hormone* ya aina *oxytocin* hutolewa wakati mama anapokuwa na uchungu wa uzazi *(labour pain)* kama alivyorekebisha Mheshimiwa swali lake na pia wakati wa unyonyeshaji. Lakini pia, daktari humpatia mzazi *oxytocin* ili kuanzisha ule uchungu wenyewe wakati kuna panapotokezea haja ya kufanya hivyo au kuufanya uchungu wenyewe uwe mkali zaidi. *Oxytocin* ni *hormone*, yaani chembe chembe ambazo hutengenezwa kwenye bongo na *gland* inayojulikana au eneo linalojulikana kama *Hypothalamus*.

Chembe chembe hizo husafirishwa na kutolewa na *Pituitary gland* ambayo jina lake jengine ni *master gland* ya mwili nzima inayo-*control glands* nyengine nyingi pamoja na *hormone* nyengine nyingi zinazotoka mwili na chembe chembe hizi za *oxytocin* zinapotolewa hufanya kazi mbili.

1. Hufanya kazi wakati wa kuzaa.

2. Hufanya kazi wakati wa kunyonyesha, yaani *triggering* ya kutoa maziwa mengi zaidi kupitia *hormone* hiyo.

a)Mhe. Naibu Spika, taarifa hii ya kukosekana kwa *hormone* ya aina *oxytocin* katika mwili wa mwanadamu siyo sahihi, lakini inapotokea haja ya kuongezea *hormone* hiyo basi *hormone* hizo zipo katika hospitali zetu zote zinazotoa huduma za mama na mtoto pamoja na uzazi na siyo kwamba hutolewa katika kila *labour*, hutolewa baadhi tu ya *labour*, yaani baadhi tu ya uzazi ambapo daktari ama mkunga mtaalamu ama mzalishaji anapoona kuna haja hiyo na kufanya uamuzi wa kutoa *oxytocin* ili kuongezea nguvu za kusukuma mtoto.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, lishe inapokuwa ndogo mama hushindwa kupata nguvu wakati wa kujifungua na kusababisha kuchelewa kujifungua. Yaani lishe ndogo husababisha pumzi za mama kushuka na kuwa ndogo na pia, nguvu za kusukuma na hata wakati mwengine *hemoglobin (HG)* hupungua katika damu yake ambayo nao inachangia kumkosesha nguvu kwa sababu *HG* hubeba *oxygen*.

b)Wataalamu wa afya wanaweza kuigundua hali hiyo ikiwa mama mjamzito atakuwa anahudhuria *clinic* ya wajawazito kwa mpangilio aliopangiwa. Kuhudhuria *clinic* huku ni muhimu sana na ni njia pekee ya mama mjamzito kuweza kutambuliwa matatizo yake mapema ambayo yanaweza kujitokeza wakati wa ujauzito wenyewe ama wakati wa kujifungua na hata pia baada ya kujifungua matatizo hayo huwa yanaweza kuonekana mapema.

Mhe. Naibu Spika, hivyo basi kwa kumtambua mzazi juu ya kuhitaji au kutokuhitaji *hormone* hii ya *oxytocin* ni wakati wa ujauzito na siyo wakati wa kujifungua, yaani siyo wakati wa *labour pain*. Katika *clinic* wao huwatambua mapema zaidi ikiwa kuna mahitaji hayo. Kipindi cha mwanzo cha mama mjamzito anapokwenda *clinic* ndipo *monitoring* ya ujauzito wa mzima unapofanyika na kujulikana mahitaji yake yote atakayohitaji mama mjamzito huyo na kila anapokwenda *clinic* hususan hizi *clinics* za *RCH*, yaani *Child Healthier Clinic* na *mother* huweza kutatuliwa mambo mengi zaidi hata kabla ya kujifungua.

Mfano mtoto anapokaa upande katika vipindi tofauti, mapigo ya moyo ya mtoto yanapokuwa madogo, mgeuko wa mtoto na *activities*, yaani zile *movements* zake, kucheza cheza ndani ya tumbo kuwa mdogo, kunapopungua mambo yote mengine pamoja na *other defects*, yaani kasoro nyenginezo.

Kwa hivyo, naomba kusisitiza tena kuwa ni muhimu sana kwa mama mjamzito kwenda *clinic* kwa wakati na mapema ili kuepukana na matatizo yote hayo yanayoweza kutokea baadae hasa wakati wa kuzaa pamoja na kutusaidia Serikali katika kupunguza *Child and Maternal Mortality Rate*, yaani vifo vya mama na mtoto.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, naomba tena kupitia kwako na kupitia Baraza hili la Wawakilishi kwa Wawakilishi wote kusisitiza sana akina mama wajawazito kufika *clinic* wakati hasa Mikoa ya Kaskazini Unguja na Micheweni Pemba, kwa sababu wao ndiyo wanaoongoza kwa *figures* za uzazi kila mwezi na kila mwaka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, yenye ufafanuzi wa hali ya juu sana. Naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa lengo na dhamira ya Serikali kama alivyokiri Mhe. Naibu Waziri *Reduction of Mother's Child Mortality Rate*, kwa maana ya kupunguza vifo vya mama na mtoto. Kwa kuwa hapa ametwambia kwamba *ditectation* ya *deficiency* ya *oxygen* katika mjamzito inakuwa *dictated* kabla hajaingia katika *post pre-natal* pale hajaingia, yaani anaonekana hapo kwamba ana upungufu wa *oxytocin* huyu *hormone* anaye *bring about labour*.

Sasa swali langu lipo hapa ni sababu gani ya msingi inayopelekea mjamzito ndani ya *labour room* kuambiwa mtieni maji ya uchungu huyo, maana kule Pemba huambiwa hana maji ya uchungu mtieni. Sasa huku nyuma ilikuwa haijakuwa *dictated* hiyo. Je, kwa wale waliokuwepo *outreach* na hii *clinics* za wajawazito kwa mfano waliokuwepo kwenye visiwa, ikiwa maji ya uchungu hawakufika haraka wakapewa yale maji ya uchungu, itakuwa ndiyo sababu ya kumpoteza mama na mtoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa ni kweli hayo anayoeleza kuwa baadhi ya wakati yanatokea, lakini zipo sababu nyingi ambazo zinapelekea kutokea hayo. La kwanza kabisa na naomba hili niliseme kwa uwazi kabisa, maana juzi tulikuwa na kikao na wakunga wote wa jadi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na kwa nini tulionana nao.

Mhe. Naibu Spika, tulionana nao baada ya kufanya *research* na kugundua ujauzito wote unakuwa hauna matatizo ila matatizo hutokea pale mjamzito anapoingia katika *labour process*, anapoanza ile *first labour pain*. Tumegundua nini? Ndiyo tukafanya kikao na wakunga wa jadi ili sasa tuanze kuwatambua wao kama wale waganga wa kienyeji kwa kuwapa kupitia ile Bodi ya Tiba Asili kuwapa vibali na vitambulisho na hawa wakunga wa jadi sasa tunataka tuwatambue, tuwape na wao mafunzo maalum, wapate na wao vyeti na wawe na leseni za kutusaidia kuzalisha kwa sababu bado akinamama wa mikoa hiyo hususan Mkoa wa Kaskazini Unguja na Wilaya ya Micheweni Pemba, kule kawaida wanafanya *consultation* moja kwa moja kutokana na imani zao kwa hawa wakunga wa jadi.

Mhe. Naibu Spika, sasa tatizo lililotokezea hapa kuna haya madawa ya kienyeji ambayo hawa akina mama wajawazito huwa wanasema tokea enzi ya bibi hizi dawa zinatumika. Moja nimepewa jina juzi, mimi sizifahamu na mti wenyewe nimeoneshwa unaitwa mpatakuva. Pili, nimeoneshwa juzi pia hivyo hivyo na mti unaoitwa mzaliwa-nyuma.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, haya majina nimejifunza kama siku tatu zilizopita baada ya kufuatilia suala hili tulilokuwa tunapata kwamba *mortality* na *child rate* tunafanya jitihada, lakini hazipungui, zipo *graph* yake ipo *almost constant,* yaani ipo pale pale. Sasa baada ya kuzungumza nao tunagundua haya yafuatayo ambayo najibu sasa swali lako Mhe. Saleh.

Tukagundua kwamba huu mpatakuva, mzaliwa-nyuma pamoja na madawa yote mengine yanasaidia sana katika kumsukuma mtoto kutoka wakati wa *labour pain*, kama kazi ambayo *oxytocin* inafanya, lakini tatizo liko hapa. Unapomsukuma mtoto na mtoto anapotoka. Nachukulia mfano mkono wangu huu ndio mtoto, unapomsukuma mtoto na mtoto anapotoka lakini ile njia ya huku chini haijafunguka kuanzia hapa *pelvic girdle* haijafunguka ile njia nzima, kwa sababu kiuno kizima hutanuka na kumpisha mtoto na kichwa chake aweze kutoka.

Kwa hivyo, yule mtoto anapofika chini hukwama kwenye ile njia, huku kuna *pushing*, kwa sababu o*xytocin*, patakuva na mambo mengine yote yanasababisha yule mtoto asukumwe, lakini anapofika chini anakwama, anapokwama mtoto yanatokezea mambo matatu; Jambo la kwanza, anakosa pumzi, yaani ile *circulation* nzima ya damu kuingia katika mwili wa mtoto inakosekana pale, mtoto anakuwa anakwama njia haijafunguka, njia ndogo mtoto mkubwa hawezi kutoka.

Lakini la pili, husababisha yule mtoto kupata *suffocation* ya mzunguko wa damu pamoja na kubanwa kwa baadhi ya viungo, ndio hapo unaweza kutoa *brenda mage* au uka-*damage* vitu vingine. Lakini la mwisho kabisa husababisha kifo cha yule mtoto kwa kukaa muda mrefu, kwamba juu anasukumwa kutoka chini na chini njia haijafunguka ya kumruhusu kutoka.

Sasa tulichokifanya ni kukaa na hawa wakunga wa jadi kwamba kujaribu kuzungumza nao kwamba waendelee kutumia mpatakuva na mambo mengine kwa kumsukuma mtoto, lakini washirikiane na sisi kwa ajili ya kufungua njia ile ya kutokea mtoto na *oxytocin* inasaidia katika kazi ya kufungu njia ya kutokea mtoto, unapomsukuma mtoto ukawa hujafungua njia, basi yule mtoto pale anakwama na inaweza pia ikasababisha kifo cha mama mjamzito.

Kwa bahati nzuri tulipokelewa vizuri na hawa wakunga wa jadi, tumefanya mazungumzo mazuri na wao walitulaumu wamesema nyinyi siku zote mlikuwa wapi hamjaja kuzungumza na sisi, walitulaumu kidogo na sisi tumekubali zile lawana na sasa tunaendelea kushirikiana. Ninatarajia, tulifanya *survey* pale Mkoa wa Kaskazini ndio maana nikasema inaongoza. Wale wakunga wenyewe wa jadi tulifanya *survey* haraka haraka kila mmoja ana watoto wangapi, yule wa chini kabisa ana watoto 10, inaendelea 11 mpaka 12 na kila mmoja alisema aidha yeye mke wa pili au mke wa tatu.

Kwa hivyo, mtapiga mahesabu nyinyi wenyewe Waheshimiwa wastani wa baba mmoja ana watoto wangapi kwa kule Mkoa wa Kaskazini. Sasa hilo tumefanikiwa na naomba nishukuru kwa swali lako la nyongeza, limeweza kunisaidia kutoa maelezo na elimu ambayo tutaweza wote kushirikiana kuitoa kwa wazazi wetu.

Mhe. Naibu Spika. ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali (a) na (b). Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kuweza kuelewa kwamba kuna mpatakuva na kuna mzalia nyuma ambao huu huwasaidia sana mama wajawazito wakati wa kujifungua, huwa wakipewa wanapata nguvu ya kuweza kujifungua.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa kina mama wengi wanapobeba ujauzito hukosa hamu ya kula na ndio sababu mojawapo inayowasababisha kukosa nguvu wakati wa kujifungua. Je, Mhe. Naibu Waziri hali hii husababishwa na nini.

Lakini pili, Mhe. Naibu Waziri, huoni kuna haja ya wizara kuteremka chini ili kutoa elimu kwa akina mama wajawazito na wale ambao wanatarajia kuwa wajawazito, ili waweze kuelewa elimu hii ya mama mjamzito mapema ili wanapobeba ujauzito waweze kuijua hali ya kuwa ni wajawazito.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Nashukuru sana kwa hili swali la kwanza, kwa sababu hata mimi nilijaribu kuwauliza wataalamu waliobobea, maana ile ziara tuliifanya na watu mbali mbali, pamoja na watu wa Umoja wa Mataifa kutoka *UNFPA* na kutoka shirika lile la *CHAPAIGO* na bahati nzuri wale

wakuu wa idara hizo sasa hivi kwenye Umoja wa Mataifa walikuwa ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya, mmoja wao alishawahi kuwa *martron* kwa muda wa miaka 18 pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hili swali likaja la kwamba, kwa nini mama mjamzito anapokuwa na ujauzito anakuwa hana hamu ya kula.

Mhe. Naibu Spika, siku hiyo ndipo nilipokuja kujifunza, kwamba sio kwamba anakuwa hana hamu ya kula, lakini vile vyakula wakati mama mjamzito, kwa sababu anakuwa na kitu kama, ina lugha ya kitaalamu limenitoka hilo, lakini ni kuhisi kichefuchefu. Sasa katika kichefuchefu kile kunatakiwa vyakula maalum vile vilivyochapuka vipatikane. Sasa wale wanaoandaa vile vyakula kwa ajili ya yule mzazi wakiwa hawalijui hilo.

Kwa mfano vile vyakula vikali, ndimu, embe na kadhalika vinavyochanganywa katika vyakula vya kawaida, vinatakiwa viwe vinaleta ladha nzuri kwa sababu hata ladha mdomoni kwenye zile *taste bards,* wakati wa ujauzito kuna kuwa na ute ambao unajipanga unapunguza ulimi kupokea ile hisia ya ladha.

Kwa hivyo, wale wanaokaa na wazazi au hata kina baba wale wanaowaangalia akina mama wakati ni wajawazito walijuwe hili, kwamba vyakula kidogo vinabadilika, inakuwa sio vile vya kawaida. Kama ulikuwa unaweka chumvi kidogo inabidi uongeze, kama unaweka ndimu kidogo inabidi uongeze, kama unaweka embe mbichi kidogo inabidi uongeze na kadhalika, pale yule mwanamke ndipo anapopata *appetite* ya kuweza kula. Sio kama hawezi kula, lakini anakuwa ile hali ya kichefuchefu inamfanya akione kila kitu kibaya. Hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la pili, sisi tayari sasa hivi elimu inatolewa ya kutosha sana, kwa sababu tuna *outreach services*, yaani wale ma-*nurses* ama wakunga wa kwetu na wale wauguzi wengine huwa wanatoka wanagawana, nusu huwa wanatoka kwenda kutoa elimu katika jamii pamoja na maafisa wa afya jamii.

Lakini la pili, tuna *Home Base Care* baada tu ya mama mjamzito kuja *clinic* kupimwa, basi anaweza pale akaomba *Home Base Care* na kama eneo lile kuna kina mama wengi basi huwa wanakwenda kutoa elimu.

Lakini la tatu, huwa tunatoa vile vipeperushi ambavyo nitajitahidi nivilete hapa Barazani, niwape Wawakilishi akina mama na akina baba wote waweze kutusaidia kufikisha majimboni kwao. Hayo ndio tunayoyafanya mpaka sasa hivi mbali ya vipindi vya redio na vipindi vya *TV*, pamoja na magazeti ambayo tunawashukuru sana waandishi wa habari wanatusaidia sana katika kutoa elimu, hasa ya afya ya mama na mtoto katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ya kitaalamu, lakini naomba anielimishe maswali yangu mawili kwa maana ya (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri, amekiri kwamba wanawake wakunga wa Kaskazini Unguja wamempa tamaa kubwa juu ya mti wa mpatakuva na mzalia nyuma. Ni kweli kwamba wazee wetu wengi hasa vijijini, wamekuwa wakitumia mti huu kwa muda mrefu na pengine wengi wetu humu ndani bila ya kujijua wamezaliwa kwa msaada wa mpatakuva na mzalia nyuma na ndio maana wanaamini wazee kwamba mti huu pia umechangia sana kuzaa watoto wenye akili na wenye ufahamu mzuri.

(a)Mhe. Spika, kwa msingi huo mbali ya kupata taaluma hiyo ya wazee wetu. Je, wizara itachukua juhudi gani sasa kushirikiana na wazee hao kutumia mti huu kuufanyia utafiti wa kitaalamu ili waweze kupata *product* ambayo itasaidia sana katika shughuli za uzazi wa wananchi wetu.

(b)Naomba kujua Mhe. Naibu Spika, hili suala la *hormones* ambazo zinasababisha mjamzito kupata nguvu ya kusukuma mtoto. Ni tofauti gani ya mama mjamzito ambaye anajifungua mtoto mmoja na mama mjamzito ambaye anajifungua watoto wawili, watatu hadi wanne kiwango cha *hormones* hizi zinakuwa ni kiasi gani. Kwa sababu kama kiwango sawa, mama ambaye anajifungua watoto watatu, kunakuwa na msaada gani mwengine ambao unatofautiana na mama ambaye anajifungua mtoto mmoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Nashukuru kwamba yeye pamoja na sisi tunakubaliana katika kutambua umuhimu wa hawa wakunga wa jadi, kwa sababu wanaisaidia Serikali kwa upande mmoja katika uzalishaji, ila tunataka tufanye programu maalum ambayo wale wakunga wa jadi watakuwa wanatambulikana.

Pili, panapotokezea tatizo yule mkunga wa jadi aweze kuja na mzazi moja kwa moja hospitali, hususan pale mama mjamzito anapopoteza damu nyingi au pakatokezea tatizo la mtoto kujizonga na ile *umbilical cord* au mengine kama hayo kwa akina mama wanaozalia nyumbani. Kwa hivyo, hilo tunaendelea kufanya mawasiliano nao na mafunzo mara mbili yameshatolewa kwa wakunga wa jadi, kujua wao jinsi wanavyofanya, sisi tunavyozalisha hospitali na pia mashirikiano gani tupeane pale panapotokezea tatizo ili wao wajuwe wapi pakukimbilia.

Nakubaliana pia na Mhe. Mjumbe kwamba wengi pengine, hata humu ndani ya Baraza kama alivyosema yeye wamezaliwa kwa kupitia huo huo mpatakuva na mzalia nyuma. Lakini naomba aelewe kuwa mama zetu wakati huo lishe yao ilikuwa nzuri kuliko sasa hivi, walikuwa wanakula *natural products*, yaani vile vyakula vya asili, wali wa mtama, mkate wa uwele, vitu hivyo sasa hivi havipatikani. Kuna Mheshimiwa hapa ananiambia vipo, lakini havipatikani kirahisi.

Kina mama na kina baba nyinyi siku zote mama akikuambia anataka *chips* kuku, wewe unakwenda moja kwa moja kuchukua *chips* kuku, wanasahau kama lile dagaa dogo ndio lenye *one of the richest source of ion* kwa mama mjamzito, yaani dagaa lile dogo. Nashukuru Mheshimiwa samaki na nyama kanipongeza kwa hilo, yaani uvuvi na mifugo, kwa mfano dagaa, mchicha, maziwa hizi ndio *the richest sources,* lakini utakuta mama anakula *chips* zimejaa *tomato source*, ndani zina *float* na kuku huyu aliyepigwa sindano na kadhali.

Sasa huwezi kumfananisha mzazi yule na wazazi wetu waliokuwa wakati huo walikuwa na nguvu, hata *oxytocin* ikitoka nyingi au kidogo wakati huo yule mama mwenyewe ana nguvu za kusukuma, anasukuma mtoto moja kwa moja anatoka, pengine hata haitaji hiyo *additional hormone*.

Mhe. Naibu Spika, haya mambo tunayaona sasa hivi yanajitokeza kwa wingi kwa sababu sasa hivi ile lishe wanayotumia akina mama imepungua kwa sababu, sio samaki wamepungua Kaskazini hapana, ila hawali tena hawarudi kwenye kile chakula cha asili. Utakubali vipi mwanamke wa Mkoa wa Kaskazini awe na *HB* ndogo, hakuna sababu, kwa sababu Mkoa wa Kaskazini ndio wenye *richest source of protein*, yaani samaki wakubwa na wengi wanatokea kule, mfano mchicha mtu anaweza kukupa fungu bure bila ya kununua, ndio *one of richest source*.

Sasa unakuta mtu anakuja pale *ion level*, chuma katika damu iko kidogo, *HB* iko chini. Hii inatokana na lishe tunayotumia sasa hivi, turudi tena kwenye vyakula vya asili, vyakula vya asili vipo, kuna mikate ile ya kiasili ya mitama na kadhalika, ambapo hata wagonjwa wa kisukari mara nyingi huwa wanashauriwa na madaktari wale vyakula vile vya asili, kwa sababu wanapata tiba mule mule ya kupunguza maradhi ya kisukari kupitia vyakula hivi hivi, kama mtama, uwele na kadhalika.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba utafiti hivi sasa tayari umeshaanza kwa huo mpatakuva na mzalia nyuma na Idara ya Mkemia Mkuu na Idara ya Mfamasia Mkuu zinashirikishwa ipasavyo.Tukishindwa hapa tutawapelekea wenzetu wenye *laboratory* kubwa ili waende wakaangalie na baada ya hapo haki miliki iwepo kwa wale wanaotumia dawa hiyo.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nilitaka kujua tofauti ya wingi wa *hormones,* ambazo mama mjamzito aliyejifungua mtoto mmoja na mama mjamzito aliyejifungua watoto watatu. Kuna uwiano gani wa *hormones* kwenye tofauti ya wanawake hao wawili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Samahani Mhe. Naibu Spika, kwa sababu majibu yalikuwa mengi kidogo. Mhe. Naibu Spika, mwili unapoamua kutoa *hormone* hii *master control,* yaani *pituitary gland* ndio inayoamua. Lakini kwa swali lako Mheshimiwa, mimi sidhani kama kuna wingi wa *hormones* au kidogo wa *hormones*. Mama mjamzito anapozaa mtoto wa kwanza ile njia inakuwa ndogo kidogo, kwa hivyo, naamini atakuwa anahitaji *hormones* nyingi ili njia itanuke zaidi.

Lakini kila anapoendelea mtoto wa pili inakuwa ile njia tayari pamoja na kiuno na ndio maana mwanamke anaongezeka hata umbo, *size*, uzito, anakuwa mwanamama pale. Kwa hivyo, ile njia ya mtoto wa pili inatanuka zaidi, mtoto wa tatu hivyo hivyo, mtoto wa nne, mtoto wa tano na mpaka akiendelea sasa hapo anakuwa tena hata haja ya *hormones* hanayo tena kwa sababu tayari ile njia imeshakuwa safi.

Ila kwa mtoto wa kwanza na ndio maana inasisitizwa sana kwenda *clinic* kwa mtoto wa kwanza, kwa sababu ni muhimu sana ku-*monitor* njia, upana wa njia na nguvu za kusukuma pamoja na damu ndani ya mwili wa mwanamke, pamoja na *level* yake ya *pressure,* yaani nguvu za kusukuma damu. Kwa hivyo, naweza kusema kunakuwa hakuna tofauti ya *hormone* kutoka, lakini kunakuwa kuna tofauti ya kutanuka kwa ile njia, baina ya mtoto wa kwanza, wa pili, wa tatu na kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.(*Makofi*)

Nam. 47

Malipo kwa Huduma ya Maji ya Mifereji ya Nje

Mhe. Saleh Nassor Juma: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Kuna baadhi ya maeneo ya nchi yetu yanajengwa mifereji ya nje kwa ajili ya kuhudumia watu wengi katika eneo moja.

Je, kwa nini wananchi wanachangishwa kulipia wakati hapo awali ilikubaliwa na waziri hapa kuwa huduma hiyo ya jumla haitalipwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 47 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kimsingi napenda kutoa ufafanuzi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba suala la uchangiaji wa huduma ya maji ni la kisheria, ambalo linamtaka kila mwananchi anayepata huduma ya maji safi na salama kuchangia huduma hiyo bila ya kujali aina ya matumizi ya maji, kinachoangaliwa ni kupatikana kwa huduma hiyo na ikithibitika kuwa mteja hapati huduma hiyo basi huwa hachangishwi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na jibu la kukatisha tamaa sana la Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa haki ya kuishi ni haki ya kikatiba ya nchi hii, haki ya kuishi imeelezwa katika Katiba zote mbili; Katiba ya Zanzibar na hata ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuwa kuna watu Mhe. Naibu Spika, wapo duniani, lakini uwezo wao kimaisha ni mdogo sana, kwa hivyo, hawawezi hata siku moja kuingiza maji katika nyumba yao na kufanya malipo. Kwa kuwa kuna bomba sisi tunaita mifereji iko nje, wanafanya *public services* ya maji hapo, tangu enzi ya mzee Karume hadi leo hii mifereji ile ipo na sasa mnawalazimisha watu hawa walipe. Je, kwa kuwa hawana uwezo watu hawa maskini za Mungu, wagonjwa na walemavu waliokuwa hawana uwezo wa kulipa. Je, wasiendelee kuishi kwa sababu hawana uwezo wa kulipa maji. *That is* (a).

(b)Huoni kwamba kuwanyima maji watu wa *sample* hii, maskini za Mungu ambao wanapata maji nje ya bomba, katika bomba za nje, kuendelea kuwanyima maji kwa sababu hawamudu kulipa ni kwenda kinyume na dhamira halisi ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuhakikisha kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wake na kwa utaratibu huu wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji, imeandaa mpango maalum wa kuwawekea baadhi ya wananchi ambao hawawezi kuunganisha huduma hiyo ya maji kwa mifereji ya nje, ambapo mifereji hiyo ipo, lakini kwa utaratibu maalum. Kinyume na utaratibu wa wananchi ambao au baadhi ya wananchi ambao hufanya kazi ya kuweka mifereji bila ya kupitia utaratibu wa kisheria wa wizara.

Kwa hivyo, wizara imejitahidi kufanya utaratibu huo wa kuweka mifereji kwa baadhi ya wananchi wale ambao hawajiwezi.

Pia, tunao utaratibu wa kuwaunganishia wananchi ambao hawana uwezo wa kuingiza maji kwenye nyumba zao, kwa utaratibu wa mkopo nafuu, hili tayari tumeshaliandaa na kwa mwananchi yoyote ambaye anataka kuunganishiwa maji kwa njia ya mkopo ambaye hajiwezi basi Wizara iko tayari kumsaidia katika njia ya kumuunganishia kwa mkopo nafuu. Lengo la Serikali kama nilivyoeleza ni kwamba ni kuhakikisha wananchi wake kuwapatia huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaeleza naomba niseme jambo dogo tu, muda mfupi hapa nilipata shauku kubwa sana na nimefurahi sana kumuona Naibu Waziri wa Afya ameeleza mambo utafikiri kama ni *specialist*, ameeleza vitu ambavyo ni mtu ana *long experience*. Kwa kweli amenipa shauku kubwa sana anajua nini maana ya ukunga, anajua mambo mengi tu, ametoa taaluma, naomba hiyo nimpe hongera kubwa sana na Manaibu wengine muwe muna-*act* kama yeye kwa sababu ni muda mfupi tu.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye suali sasa. Mhe. Naibu Waziri, umeeleza katika majibu yako katika suala mama, umesema kuwa si kweli kuna watu ambao waliokuwa hawapati maji na hawatozwi pesa.

a)Mheshimiwa, utakubaliana na mimi na niko tayari twende mguu kwa mguu kuna watu ambao hayafiki maji na wanatozwa pesa kama kikawaida.

b)Lakini pili, Mheshimiwa ulisema kuna utaratibu ambao wa kuweka mifereji ya nje kwa watu ambao waliokuwa hawana uwezo, lakini kuna njia ambazo zinafanywa. Je, Mheshimiwa, kuna watu ambao hasa katika kijiji Kichungwani wamefuata utaratibu wa kutosha na hatimae mifereji ile imekatwa. Huoni Mheshimiwa kusema hapa Barazani ni kulidanganya Baraza?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Kama nilivyoeleza hapo awali Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji haimchangishi mtu ambae hapati huduma hiyo na kama limetokezea suala hilo basi limetokezea kwa bahati mbaya na tunamuomba yule yeyote ambaye kachangia bila ya kupata huduma hiyo, basi aje Wizarani na suala hilo tutalishughulikia.

Lakini suala la pili, kuhusiana na suala la Kichungwani, kama nilivyoeleza hapo awali mtu yeyote au mwananchi yeyote ambaye hana uwezo wa kuunganisha maji, lakini anahitaji kuunganishiwa maji ndani ya nyumba yake, basi aje Wizarani tutamshughulikia kwa kumsaidia kwa kupitia njia ya mkopo nafuu. Kwa hivyo, kama wapo wananchi hao na hawajafanyiwa huduma hiyo basi waje Wizarani kwetu tutawashughulikia.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza suala la nyongeza dogo kabisa.

Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu umesema kama Wizara ina mpango wa kuwawekea maji wale watu ambao kuwa hawana uwezo wa kuweka majumbani, lakini sisi kama Wawakilishi wa wananchi tunapata mfuko wa Jimbo na tunaweza kuwawekea wananchi wetu sehemu kwa ajili ya kupata huduma hiyo muhimu ya maji safi. Mimi nilipata kusikia kwa mfanyakazi wa Wizara hii ya Ardhi, Maji na Nisharti kuwa si ruhusa kuweka mifereji nje.

Je, jambo hili ni sahihi na kama ni sahihi, kwa nini hatupewi elimu na sisi tukafahamu na kama si sahihi, mfanyakazi huyo amekwenda kinyume na taratibu za Wizara?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ni kweli haturuhusi mwananchi yeyote kuweka mfereji nje ya nyumba yake kwa kutumia aidha ufundi wake yeye mwenyewe na kutoboa miundombinu yetu na kuweka mfereji bila ya kupitia Mamlaka ya Maji, ipo mifereji ya nje mingi tu ambayo imewekwa kisheria kupitia Mamlaka ya Maji, hiyo ni mifereji ambayo tumeweka makusudi kwa ajili ya wale wananchi ambao hawawezi kuingiza huduma hiyo ndani ya majumba yao.

Kwa hivyo, haturuhusu kabisa mwananchi yeyote kwenda kutoboa kwenye miundombinu yetu na kuweka mfereji wa nje kwa sababu tu ya kisingizio kwamba wananchi wanahitaji huduma na hawana uwezo, lazima aende katika utaratibu wa kisheria kwa kupitia Mamlaka ya Maji.

Nam. 57

Majosho ya Mifugo Unguja na Pemba

Mhe. Nassor Saleh Juma: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Kwa wananchi wa Zanzibar ni wafugaji wa mbuzi, ng'ombe na kondoo, kwa baadhi ya sehemu kuna majosho na kwa kuwa kuna baadhi ya sehemu nyengine hakuna na kwa kuwa na wananchi hupata shida.

(a) Je, kwa upande wa Unguja yapo majosho mangapi.
(b) Na kwa upande wa Pemba yapo mangapi.
(c) Je, ni lini Serikali itaongeza majosho kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu namba 57 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Matumizi ya majosho hutumika kwa kuzuia kupe na wadudu wengine kama; mbu, chofua na usubi ambao hueneza magonjwa mbali mbali kwa wanyama aina ya ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa si maeneo yote ya Unguja na Pemba kuwa huduma hii ya majosho inapatikana, hii inatokana na uchakavu wa majosho, maeneo ya ufugaji kubadilishwa matumizi yake na kuongezeka kwa makaazi ya watu ndani ya maeneo husika.

Mhe. Naibu Spika, ili kukabiliana na kupe pamoja na wadudu wengine wenye kueneza magonjwa ya mifugo, Wizara yangu imesambaza mabomba ya kunyunyuzia dawa ya kuzuia kupe kwa kila kituo cha kutolea huduma ya matibabu na uzalishaji mifugo. Wafugaji huwasiliana na wataalamu wa mifugo pindi ikitokezea haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Naibu Spika, naomba sasa kujibu suala lake namba 57 lenye kifungu (a), (b) na(c) kama ifuatavyo:-

a) Kwa upande wa Unguja kuna majosho tisa ambayo kati ya hayo ni matatu tu ndiyo yanayotumika. Majosho yanayotumika ni la Kisakasaka kituo cha Karantini, Pangeni pamoja na shamba la mifugo la Kizimbani katika shamba la chuo ambalo linaendelea.

b) Kwa upande wa Pemba kuna majosho manne; majosho mawili yako Wilaya ya Micheweni katika kijiji cha Konde na Makangale, Josho moja liko Wilaya ya Wete kijiji cha Ole na Wilaya ya Mkoani katika kijiji cha Mjimbini. Ni josho la Mjimbini na Makangale tu ndiyo yanatumika kwa kuogesha wanyama na mawili yaliyosalia yanahitaji ukarabati mkubwa.

c) Josho la Mjimbini ni jipya ambalo limezinduliwa rasmi katika Sherehe ya Mapinduzi matukufu ya miaka 51 na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Hii ni katika kutekeleza adhma ya Serikali ya Mapinduzi, kuwaondoshea kero zilizokuwa zinawakabili wafugaji wa Wilaya ya Mkoani. Bado Wizara yangu itaendelea kujenga majosho mapya na kukarabati yale makongwe hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize suala la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa ametuambia kwamba katika kisiwa cha Unguja kuna majosho tisa na katika haya ni matatu tu ambayo yanafanya kazi na katika kisiwa cha Pemba ni mawili tu katika manne yanayofanya kazi na kwa

kuwa asilimia kubwa ya Wazanzibari katika kutekeleza mpango wa Serikali wa 2020 pamoja na ule mpango wa kupunguza umasikini na kujiengezea kipato wamewekeza maisha yao katika sekta ya mifugo.

Je, haoni Mheshimiwa kwamba uchache wa majosho yaliyopo unaweza ukarudisha nyuma jitihada za wananchi katika suala zima la kujipatia kipato kutokana na kwamba mifugo yao haina majosho. Hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa umekiri kwamba wanyama hawa hawana majosho na wanakuwa ni chanzo cha wadudu kama vile mbugo, chofuo na wengine, sasa huoni kwamba kuendelea kukosa majosho na huku wakati tunafuga ni kuongezeka kwa mdudu anaitwa *eases fly* ambaye anayeleta ugonjwa wa malale, huoni kwamba mdudu huyu anaweza akatusababishia hata sisi binadamu au sisi wafugaji ugonjwa wa malale.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Niseme tu katika jibu langu la msingi kuwa baada ya kukosekana majosho na miundombinu mingi kuwa mibaya, tuligawa mabomba kwa wafugaji mbali mbali na katika vituo vyetu ambavyo vya uzalishaji na utibabu wa wanyama ili kuongeza *speed* ya kuweza kuwahudumia wafugaji wetu.

Lakini hata hivyo kwa wale wafugaji ambao wanafuga ng'ombe wa maziwa tuliwafundisha wao wenyewe kwa masomo ya muda mfupi na kuweza kuwagaiya mabomba yale ili kuondoa hili, lakini huu uchakavu umetokana na uchakavu wa majosho. Majosho sasa kuna mambo mengi; moja kuwa wananchi wamesogea karibu ya majosho yale kwa kujenga, lakini vile vile mengine yapo kwenye mashamba ya wakulima ambayo pia yataleta bughudha kubwa sana, kama unavyojua madawa yale ni makali yanaweza kuharibu mazingira, ndio maana yametokana na hivyo, lakini jitihada hizo zimefanyika.

Lakini hata hivyo, zipo dawa ambazo sasa tunatumia, kwanza nikutoe wasi wasi *eases fly* hii haipatikani hapa Tanzania hii iko Afrika ya Magharibi sana sehemu za Gambia ambazo ndio zinapatikana *sleeping seek nears*. Kwa hivyo, nitoe wasi wasi kwa wananchi wote kwa *East Africa* kuwa maradhi haya hayapo hapa.

Vile vile, kuna dawa ambayo sasa inatumika kwa kupiga sindano ambayo inaitwa *evometrics,* hiyo nayo inapigwa shindano na kuuwa wadudu hawa mara moja kuliko hata kutumia yale majosho ambayo dawa nyingi sasa inaweza ikapotea na tukaweza kuipoteza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafsi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, amekiri kama majodho yaliyopo kwa upande wa Pemba ni manne yanayofanyakazi na kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Micheweni ni wafugaji sana walio wengi, Kiuyu, Maziwa Ng'ombe na Maziwa ya Ng'ombe yenyewe na Micheweni, wote ni wafugaji. Haoni wananchi hao wa Jimbo la Micheweni kutoa ng'ombe pale mpaka wakafika Konde ni usumbufu mkubwa, kama ni usumbufu, lini Wizara yake itafanya utaratibu wa kuwawekea josho katika eneo la Micheweni ili kuwapunguzia usumbufu.

Na pia, namuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu amesema kama kuna mabomba wamegawa ili kuwasaidia wafugaji wapunguze hiyo haiba ya kuwaosha ng'ombe ili kupunguza hao wadudu.

Sasa namuuliza Mhe. Naibu Waziri, ni lini wamegawa mabomba hayo na wamegawa kwa utaratibu gani na je, wanawajua wafugaji wote kwa utaratibu wa kuwaandika kuwajua kama hapa huyu ameshapata bomba na huyu hajapata. Kama hivyo ndivyo na kama hawajatumia utaratibu huo, ni lini watatumia utaratibu huo ili wafugaji wote waweze kupata hayo mabomba kwa ajili ya kukosha ng'ombe wao na kuwaondolea uvivu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Kwanza tu niseme mabomba haya tumeyagawa kupitia wale wataalam wetu wadogo wadogo tuliowapa mafunzo madogo madogo ambayo wanaitwa ni *cows* kila wilaya, lakini vile vile Wizara yangu sasa inafanya taratibu maalum za kuweza kuona kila Wilaya linakuwepo josho moja ili kuondoa zile kero za wananchi zisiweze kupatikana kila mara.

Na haya mabomba ambayo labda kama wewe Wilaya yako umegundua hayajapatikana, basi nakukaribisha uje ili tuende tuone kama bado yatakuwa hayajapatikana tutaweza kukusaidia katika zile sehemu ambazo zilikuwa mabomba hayajafika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri ambayo anaweza kuyajibu kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini pia, niseme kwamba katika jibu lake mama alisema kwamba Wilaya ya Micheweni au Wilaya ya Wete kuna majosho mawili, Wilaya ya Mkoani vile vile kuna majosho mawili, lakini katika majosho mawili haya, josho hili la Mjimbini kama nimesikia vizuri bado halijaanza kufanyiwa kazi.

Je, Mhe. Naibu Waziri, ni lini josho hili litaanza kufanyiwa kazi? lakini pili, kuna elimu yoyote ambayo imetolewa kwa wafugaji hawa namna ya kukosha hawa ng'ombe. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nadhani Mhe. Mwajuma, sasa ni vyema tukaanza kutembelea jimbo ili tuweze kujua na Wilaya nzima tuweze kujua matumizi hakika na lini limeanza kutumika, labda taarifa tu kwa Baraza lako tukufu kuwa tayari josho lile limeanza kutumika siku ile tu ambayo Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo amelifungua pale na tayari tukaweza kutoa fursa ya wafugaji wetu waweze kukosha.

Lakini hata hivyo tumetoa tayari elimu kwa wafugaji pale wadogo wadogo ili kuweza kulitumia pamoja na wale viongozi wa Shehia kuweza kulitumia kwa urahisi zaidi. Nadhani hilo halina wasi wasi na nikuhakikishie kuwa josho lile tayari linatumika ipasavyo.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni ya Mwaka 2015

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majina niliyopata ya wachangiaji wawili wa kwanza Mhe. Mohammed Haji Khalid, wa pili Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ambaye ameshatoka nje, kwa hivyo, naomba wenye nia ya kuchangia walete majina na tunamuanza Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mwakilishi wa Mtambile Pemba.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kupata fursa hii ya kutoa mawazo yangu machache juu ya mswada ulioko mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukaa hapa katika shughuli zetu za kawaida, pia, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi aidha nimpongeze Waziri na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu, pia, Kamati husika zaidi kwa Mwenyekiti wake kwa kuwasilisha mapendekezo au maoni ya Kamati.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwenye neno "maana ya utamaduni" kama ilivyoelezwa katika huu Mswada wenyewe, neno "utamaduni" kwa lilivyotafsiriwa humu maana yake ni mfumo maalum wa maisha unaohusiana na mila, desturi na amani za watu maalum katika wakati maalum.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na tafsiri hii ya neno "utamaduni" ina maana hauna tafsiri maalum vile vile, tafsiri yake inakwenda kwa lugha ya sasa na wakati uliopo, yaani watu leo wakiwa hivi utamaduni uko hivi, ndio maana ikawa Zanzibar hatuna pa kushika kuhusu utamaduni na ndio maana kila mtu ikawa anavaa, anatembea na anafanya anavyotaka kwa sababu hatuna utamaduni.

Kama ulivyosema utamaduni wa Mzanzibari ni upi? Kwa sababu mtu anasema ni maalum, vile mtu anavyofanya kwa yeye ndiyo mtu maalum, kwa wakati maalum. Sasa wakati huu ni wakati maalum, sasa wakati huu ni wakati maalum. Je, hivi tunavyofanya au tunavyokwenda ndio utamaduni wetu ulivyo? Kwa hivyo, neno "utamaduni" kwa maana hii umepoteza maana yake na utakuwa utamaduni utamaduni wa Zanzibar haupo.

Mhe. Naibu Spika, nianze na muundo wa hili Baraza. Baraza hili la sanaa niliposikia lina jumla kama la wajumbe 12 wanaotokea katika kada mbali mbali. Kuna wajumbe wawili tu wanaowakilisha vikundi vya sanaa. Jambo lenyewe ni la sanaa, lakini wale wasanii wenyewe katika muundo wa hili Baraza wapo wawili tu. Kwa hivyo, hawa wasanii binafsi bado hawajapewa kipaumbe katika Baraza lao la Sanaa na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Watu wengi waliokuwemo katika Baraza hili la sanaa ni wale wanaoingia kwa nafasi zao ambao takribani wote ni watendaji au kutoka Taasisi za Serikali. Kwa hivyo, ningependekeza hapa kwa kuwa hili ni Baraza linalowahusu wasanii, wasanii wenyewe waongezwe kidogo ili ionekane kuwa na wao wamepewa kipaumbele katika jambo ambalo linawahusu.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye sifa za Mwenyekiti, kwa hili Baraza tunalolizungumza. Nikaambiwa Mwenyekiti anaweza kuteuliwa au mtu anaweza kuteuliwa kuwa mwenyekiti, wa Baraza akiwa Mzanzibari, anaouzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa na ana maadili yanayokubalika katika jamii. Ingawaje haujatajwa uzoefu wa muda gani na takriban Miswada mingi huu uzoefu huwa unapewa kiwango aidha unakuwa wa miaka mitatu, mitano, saba na kadhalika, lakini hapa awe na uzoefu tu; uzoefu unaweza ukawa hata wa mwezi mmoja au mwaka mmoja. Kwa hivyo, hapa huu uzoefu nao ungeainishwa ni uzoefu wa muda gani.

Halafu awe na maadili yenye kukubalika. Kama nilivyosema pale mwanzo nilipotafsiri huo utamaduni katika hali hiyo niliyoiyona, niliona kuwa vyovyote mtu alivyo kulingana na tafsiri ya utamaduni ni hali iliyokubalika, vyovyote vile. Nyinyi watu wa Wizara mmeleta tafsiri hii kwa sababu kuna kitu mnachokiita haki za binaadamu, ndio maana mmeona huu utamaduni mkiufanya katika hali halisi ya Kizanzibari mtajifunga na watu wengine kutembea, kwenda, wanavyotaka wakiwa *half nacked.*

Kwa hivyo, mtumie akili yenu msijifungu mtu vyovyote atakavyokwenda ni wakati maalum. Kwa hivyo, huyu Mwenyekiti vyovyote atakavyokuwa na vyovyote atakavyovaa atakuwa anakwenda kwa wakati maalum. Kwa sababu ndivyo utamaduni wetu ulivyo unakwenda kwa wakati maalum. Ningependa kujua hii ana maadili yamekubalika katika jamii. Jamii hii tunafanya mengi, sijui yepi yanokubalika.

Mhe. Naibu Spika, nende mbele kidogo katika kifungu cha 7(2) kinahusu utoaji wa vibali na leseni. Mambo haya ya sanaa ambazo tuna sanaa za aina mbali mbali; kuna sanaa za maonyesho, kuna sanaa za ngoma na kadhalika. Huko nyuma vibali vilikuwa vinatolea na taasisi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano baadhi ya ngoma au baadhi ya maonyesho ya zamani yaliyokuwa yakifanywa katika shughuli za harusi.Watu wanakodi beni kwa mfano, msewe, kibati na kadhalika, hayo ni mambo ya sanaa. Lakini vibali vyake vilikuwa havitoki katika taasisi ya sanaa, ilikuwa watu wanachukua ruhusa tu kwenye jeshi la polisi kama kuja kulinda usalama. Kwa hiyo, kunakuwa kuna taarifa tu kwamba Mgogoni leo kuna harusi na kutapigwa beni.

Mhe. Naibu Spika, lakini taasisi hasa ya sanaa ilikuwa haitoi kibali ama watu wanakwenda kwa Mkuu wa Wilaya, ile fedha ya kibali inaingia katika sehemu siyo husika. Sasa leo ulipoanzisha hili Baraza likawa Baraza ndilo ambalo litatoa leseni na vibali. Hili nawapongeza kuwa ni sahihi kwa sababu ndio shughuli zao wenyewe wahusika.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar kwa kima fulani vikundi mbali mbali vya ngoma vimepungua sana na hii inatokana na muamko mkuwa kwa Wazanzibari kujua dini yao.Shughuli nyingi ambazo zamani tulikuwa tunapiga mabeni, misewe na ngoma nyengine, leo tunafanya harusi zetu bila ya kutumia vikundi hivi. Kwa hivyo, vikundi vya sanaa zaidi vile vya ngoma kwa kima fulani vimepungua mno.

Ni wachache sana watu wanaofanya hayo. Sasa watu wanaokodi ngoma kwa ajili ya shughuli zao wapo, lakini wamepungua sana. Kwa hivyo, kama Serikali inataka kuhuisha na kurudisha mambo haya katika kiwango kikubwa itabidi Wizara ifanye kazi kubwa ya ziada, kuwafanya watu ambao zamani shughuli zao zinaambatana na ngoma watuoneshe kuwa utamaduni wetu upo hivi, kwa hivyo, tusiupoteze. Vyenginevyo, itakuwa hii shughuli tulioifanya tutakapoifikisha itakuwa matumizi yake sio makubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna haya masuala ya filamu haya ambazo zinaonyesha katika majumba ya maonyesho au sehemu nyengine mbali mbali, ambazo kwa kima fulani kwa sababu kuna utoaji wa leseni na vibali na kuna ukaguzi wa filamu mpaka ukubalike na Baraza husika itabidi wakaguzi wa filamu hizi wawe makini na wasiwa wachache. Kwa sababu haya mambo ni mengi sana na udhibiti wake, si rahisi.

Kwa sababu mbali ya majumba ambayo yapo kwa shughuli hizo. Tujaalie bwana fulani yeye hana kibali, lakini anatumia nyumba yake mwenyewe kwa kuonyesha filamu ambazo hazijakaguliwa zile ambazo zinakatazwa, lakini anatumia nyumba yake. Nyumba yake sio nyumba ya maonyesho, lakini ni nyumba yake ya kuishi, lakini kaamua anaweka filamu zake anazozipenda hizo ambazo tunazoziita "filamu za ngono" na kadhalika na wanakuja watu kutizama nje ya wale watu wa nyumba kwake.

Je, watu wa aina hii wao tutawachukulia hatua za aina gani ili kuona kuwa kazi hiyo wasiiendeleze. Kama kuna hatua za kumchukuliwa, je, kwa kuwa ile nyumba yake si nyumba ya shughuli hizo itakuwa mtu huyu tukimfanyia katazo fulani, je, hatumuingilii katika uhuru wa nyumba yake.

Mhe. Naibu Spika, sanaa ya maonyesho ni sanaa ambayo ina hitaji kuangaliwa vizuri sana. Sanaa hii ni taaluma kwa wengine ni ajira. Kwa hivyo, wasanii wetu ni vyema watambuliwe na wajisajili ili katika kufanya kazi zao iwe wanafanya kazi kihalali kabisa. Lakini kuna wasanii kama watungaji mashairi, utenzi na kazi zao ikawa zinakwenda katika redio na zinatangazwa, kadhalika hawa nao ni wasanii.

Mhe. Naibu Spika, hawa ningetoa wito na kuiomba Wizara vipaji vya aina hii vya watu wenye fani ya kutunga mashairi na tenzi, wajitokeze, wawasajili na tuwape motisha ya kujiendeleza katika kazi hizi, kwa sababu ni fani ambayo nahisi pole pole inaanza kupotea. Siku hizi fani hii ya tenzi zaidi inaonekana katika mikutano ya kisiasa tu. Lakini zamani ilikuwa kuna vipindi maalum hata katika redio zetu na *TV. ZBC* wakati huo ilikua ni redio tu Zanzibar, ilikuwa kuna kipindi maalum vya tenzi na mashairi. Nadhani kwa sasa vipindi kama hivyo vimeondoka.

Mhe. Naibu Spika, mtazamo wangu mimi naona wasanii hawa ni muhimu, kwa hivyo, ni vyema na wao wakajitokeza, tukawaorodhesha na tenzi zao na mashairi yao ikawa yanasomwa katika redio ili watu walio na hamu ya kujua mambo hayo wakaweza kuwasikiliza.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kazi za Baraza. Kwenye kifungu cha 7(a) imesemwa kwamba;

(a)"Kuvitambua na kuvisajili vikundi vyote vya sanaa na vyama vya sanaa vilivyopo Zanzibar".

(b)Kuhifadhi, kulinda na kuimarisha mila, silka na maadili ya utamaduni wa Zanzibar".

Hili ni jambo la msingi kweli kweli. Hawa wasanii katika kufanya kazi zao za sanaa kuhusu haya maadili na utamaduni wa Mzanzibari ambao mimi sikubaliana na tafsiri hii iliyokuwepo hapa wakati maalum, yaani Zanzibar tuna utamaduni wetu ambao unaheshima. Kwa hivyo, hivyo vikundi vyetu vya aina yoyote, pale wanapofanya maonyesho yao, mavazi yao yawe yanakubaliana na utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Spika, wasije watu kwa sababu ni utamaduni wakati maalum, wanakuja katika maonyesho yao katika ukumbi kama huu wanapituka na kucheza wakiwa na mavazi ambayo ni kinyume na utamaduni huu ninaoutaka mimi wala sio unaotaka wizara. Kwa sababu wizara wanataka utamaduni maalum kwa mtu anavyokwenda yeye mwenyewe kwa wakati maalum. Mimi nataka kwa wakati wote utamaduni wa Zanzibar uwe ni ule wa heshima, watu watembee na wavae kwa heshima, wakenda katika michezo yao wawe na mavazi ambayo ni mazuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hii ni jambo la msingi. Kwa hivyo, kazi moja hii kama itafanyika vizuri tunaweza kulinda heshima na utamaduni wetu, ingawaje hakuna tafsiri ya utamaduni wa Mzanzibari kila ukiuliza hupati jibu sahihi.

Mhe. Naibu Spika, jengine namba (f) katika kazi zao, kushajihisha ushiriki wa kikundi au mtu binafsi katika kuwakilisha Zanzibar katika shughuli za sanaa ndani au nje ya Zanzibar. Hapa kuwashajihisha hawa wasanii lazima waandaliwe kwa sababu kuwafanya waonyeshe maonyesho hayo ya kisanii nje ya Zanzibar, lazima wapikwe na wawive, waandaliwe na waandalike, watayarishwe na watayarishike na wasaidiwe, ili waweze kuwa ni watu ambao au viwe ni vikundi ambavyo zinaweza kuonesha maonyesho yao nje ya Zanzibar.

Ikiwa ni kikundi cha taarab, kikundi cha maonyesho au michezo ya aina nyengine. Ili wawasilishe Zanzibar katika vikundi mbali mbali vya nje ya nchi, lazima wizara ichukue juhudi kubwa ya kuviandaa ili wawe ni wawakilishi wazuri wa masuala haya nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nilihisi kuwa niseme kidogo katika hizi kazi kuweka utaratibu mzuri wa kuwatambua, kuwapa tunzo, wasanii wa zamani ambao wamechangia maendeleo ya kazi za sanaa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kama hili likitendeka wale wasanii wa zamani ambao bado wapo wakatambuliwa na wakapewa tunzo wanaweza kuwashajihisha wasanii wa leo na wakashajiika kama na sisi kama tutatenda vizuri kama wanavyofanya hawa, na sisi hatimaye tunaweza tukapatiwa tunzo ya kazi zetu. Kwa hivyo hili Mhe. Naibu Spika, ni jambo zuri pindipo likitendeka, wasanii wa zamani, waliopo, wako wasanii wa nyimbo, wako wasanii wa ngoma, wako wasanii wa mashairi na kadhalika kama hawa wakitafutwa au wakijitokeza na wakafanyiwa takrima fulani na kupewa hizo tunzo na wasanii wa sasa na wao wanaweza wakavutika na hiyo hali na hatimaye tukapata wasanii wa fani mbali mbali katika nchi yetu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nimesema kuwa kukagua matangazo ya burdani yanayotolewa kwenye magari na mabango ya biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kumekuwa na mtindo sasa katika nchi yetu kuja watu na biashara zao wakawa wanatoa matangazo wakati mwengine wanapiga na nyimbo na kucheza na vyenginevyo. Kwa hivyo ni vyema sasa matangazo ya aina hii kama ilivyoelezwa hapa kwanza yakakaguliwa kabisa ili yatambulikane ndani yake muna ujumbe gani katika tangazo hili. Kwenye magari watu wanatipuka kwenye magari yao ule mtipuko wao una heshima gani katika utamaduni wetu.

Mimi siku moja ilikuwa natembea tembea pale watu wana tangazo lao wanacheza cheza kaja mtu anataka kunikumbatia mimi napita na njia zangu yeye ana yake anatipuka, napita babu, babu, babu nikakimbia mimi kukumbatiwa hadharani, sitaki, kwa hivyo hata yale kati ya yale matangazo yao na ile michezo yao lazima pia ikiwezekana maana ya sensa ni kukagua vile mtu ambavyo atafanya kwenye *reality* yenyewe, wakati wa kutoa tangazo lako unataka kutangaza vipi. Kwa hivyo ni muhimu Mheshimiwa Naibu Spika, haya matangazo yakaguliwe na yakaonekana mantiki zake na *concern* zake kabla hayajatangazwa.

Mhe. Naibu Spika, niende kidogo katika ukurasa wa 391 kwenye uwezo wa Mrajis. Kifungu cha 23(1)(b) kwenye uwezo wa Mrajis kusimamia au kufuta kifungu chochote cha utamaduni kufanya maonesho ikiwa kitashindwa au kukataa kutekeleza amri au maelekezo aliyopewa na Baraza. Sasa kama kuna kikundi chetu chochote pengine kinafanya sivyo na kikapewa maelekezo na kuamrishwa fanyeni hivi na wakakataa, Mrajis hii ni haki yake kukifuta

hicho kikundi. Lakini kadhalika Mrajis asijekuwa na utashi tu kwa kikundi fulani yeye binafsi hakipendi pamoja na kuwa kinafuata maelekezo na maagizo na amri, lakini kwa utashi wake yeye mwenyewe tu pengine ndani ya kikundi muna watu hawakubaliani akaamua kukifuta. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, migogoro mingi inayotokea katika michezo ni utashi wa watu tu, kuna mtu hakubaliani na huyu wanajengeana majungu haya na yale na wengine wakatumia uwezo walionao dhidi ya wengine. Kwa hivyo uwezo huu anaopewa Mrajis lazima wautumie kiuadilifu sana ili asijemuonea mtu wala asijempendelea yeyote.

Mhe. Naibu Spika, jengine liko katika ukurasa wa 397 kifungu cha 38 kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, mimi napendekeza kukifanyia marekebisho. Kifungu hiki cha 38 napendekeza mimi binafsi kukifanyia marekebisho kwa ujumla baada ya kuwa kina 1 na 2 nimeifanya kwa muono wangu mimi iwe kama hivi ifuatavyo:-

Kikundi chochote cha utamaduni ambacho kitafanya maonesho yake bila ya leseni kitakuwa kimekwenda kinyume na masharti yaliyotolewa kwa nyumba za kuonesha maonesho na kitakuwa kimetenda kosa na kikipatikana na hatia kitalazimika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni mbili, kwenye uhalisia ilikuwa milioni tatu au hapa kwenye mswada imeandikwa kufungwa mimi nimependekeza au kufungiwa kuonesha maonesha yake kwa kipindi kisichozidi miaka miwili badala ya miaka 3.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hapo nimefanya mapendekezo yangu hivyo. Sasa niende kwenye katazo la picha za ngono. Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo pagumu, pagumu kuwa hapakataziki, aa, tunataka kukataza picha lakini watu tunatembea barabarani hilo tunalokatazwa tunaliona waziwazi, sasa tunakataza picha lakini kile kitu halisi tunakiona tukitembea tunakataza nini. Iwe picha ni kosa kuliko yule mtu mwenyewe aliye na kitu ambacho tunakikataza. Mtu anatembea kinachotokeza utakiona kile lakini picha ni kosa hiyo ngono. Picha unaikataza lakini mtu anatembea unamuona *alive* maumbile yote unamuona.

Mhe.Naibu Spika, tunakataza nini kuwa mtu asione picha tu lakini akione. Tunakwenda hoteli tunaona kila kitu lakini picha yake tu ni kosa kuiona. Hapa ningeomba Mhe. Naibu Spika, nisaidiwe, kama kile kitu halisi tukikosa kosa ni picha sawa, lakini na yule mtu mwenyewe kwenda vile ni kosa, kuna hatua gani za watu wanaofanya hivyo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kifungu cha 46 na 47. Kifungu cha 46 Mhe. Naibu Spika, mtu yeyote hatoruhusiwa kutengeneza, kusafirisha, kutangaza, kuuza, kuingiza, kutoa nje ya nchi au kusaidia upatikanaji wa picha za aina yoyote za ngono. Sahihi kabisa. Picha hizi mimi sikubali kuwepo zikauzwa ikiwa zipo zikatolewa nje kupelekewa watu wengine, lakini pia habari yangu iliyopita nyuma iwe ni kama nafanya utenzi ni kibwagizo. Je, ni kosa kuuza picha hizo kutoka nazo lakini mtu mwenyewe kuingia na kutoka hasa katika hali hiyo ni kosa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 47, mtu yeyote atakayetengeneza au kushiriki katika kutengeneza, kusafirisha, kuchapisha, kutangaza, kuuza, kuingiza nchini, kutoa nje ya nchi au kusaidia kwa njia yoyote upatikanaji wa picha za ngono zinazodhalilisha watoto atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini ya shilingi milioni mbili za Tanzania au kifungo cha miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja. Hapa katajwa mtoto tu, je, mimi nikichukua picha za ngono ambazo si za mtoto kwa sababu ya mtu kama mimi hajakatazwa hapa, imekatazwa ya mtoto tu. Je, mimi nikifanya biashara aina hiyo nikachukua watu wa umri wangu, wa Mhe. Abuu na nani na nani hapa nikikamatwa nitakuwa nimeonewa. Kwa sababu hili halijakatazwa kwa sababu sisi si watoto tena na katazo limekuja kwa watoto tu, lakini mimi Mhe. Naibu Spika, ningependekeza kuwa iwe kwa aina zote isiwe kwa mtoto tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa huu mswada sijaupitia vyema naomba nimalizie hapo na kama Mhe. Waziri ataweza kunipa majibu sahihi zaidi ya yale ambayo mengine yaliyofanywa kuwa ni masuala, nitaunga mkono mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, na mimi niweze kuchangia mswada huu asubuhi ya leo wa Mhe. Waziri, nitoe barka zangu.

Mheshimiwa wakati nilipokuwa najiandaa katika kuchangia nilikuwa naangalia ule upande wa pili kama Waziri lakini kwa bahati nzuri nilikuwa nataka nimsifu sana Mhe. wangu Mwanasheria kwa kustahmili na kuwepo muda wote lakini kaongezeka na Mheshimiwa mwengine kule, kwa hivyo niwape hongera sana kwa kustahmili kwao na kuweza angalau hivi sasa ile *line* inatia sura kwa watu wawili ninashukuru sana kwa hilo.

Upande wa pili hakutaki kusemwe umejaa, ninashukuru kwa hilo na hasa leo kuna kitu ambacho kinapitishwa mswada mkubwa sana na ni mzito hasa katika kufanya hali halisi ya maadili ya nchi yetu. Kwa sababu kuna mambo mengine lazima viongozi wengine wawepo ili washuhudie jinsi gani tunavyoweka mikakati.

Mhe.Naibu Spika, tunaweka mikakati ya sheria sasa hapa. Ukurasa wa 389, unajua watu wengi sana hawajui nini maana ya sanaa na ndio maana wengine wanatafsiri wanavyotaka wao wenyewe. Wengine wanaona sanaa ni moja kianzilishi cha mtu kwenda uchi, wengine wanaona sanaa katika uvunjaji wa maadili, lakini nashukuru sana Mhe. Waziri na wataalamu wake wamekaa wakatafsiri kutwambia kuwa jamani ee msifikirie huko.

Mhe. Waziri ni mtu mmoja ambaye mwenye fikra na ubunifu wa mbali sana kabisa. Sasa ule ubunifu ndio maana ya sanaa na yeye ndiye keshabuni sheria. Mhe. Waziri na wewe katika watu upewe historia ya msanii au mwana sanaa na wewe mmoja tukuweke kwa sababu umebuni sheria ambayo itakayoweza kusaidia maadili ya Zanzibar, kwa hivyo na wewe unaingia katika *list*. Kwa sababu mimi nilisema tuwatafutie vijiji wale watu wenye ubunifu tena ingekuwa *good history* lakini hili suala tunadharau sana sisi Zanzibar kusema ukweli ni hilo.

Ukienda katika nchi za wenzetu mimi siku moja nilienda Ujerumani, nilipokwenda Ujerumani nilikwenda kuoneshwa sehemu ya Hitler anakwenda hapo kwa kustarehe tu maana kustarehe yenyewe ku-*enjoy* kama kuna *dance* na nini na hiyo nyumba watu wengi sana wanaingia na wanaingiza fedha za kigeni chungu nzima. Sasa na sisi tungekuwa na *special* ya vijiji kama alivyosema mzee mwenzangu hapa kuwa hatuwawekei kumbukumbu wabunifu wetu wa sanaa.

Mimi ningeomba sana Mheshimiwa kwa kuwa wewe umeanzisha hili neno hapa kuwatafsiria watu, sasa toa ubunifu, tafuta viwanja, tafuta eneo tuwe na kumbukumbu zetu na sisi wale wasanii waliopita, wazee wetu watoto wengi sasa hivi hawajui, tumeshamsahau Bi Kidude hatuna kumbukumbu naye. Tushawasahau na wengine na mimi ninashindwa kuwataja Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mimi mwenyewe nimeshawasahau kumbukumbu imenipita, lakini tungelikuwa na *special* kumbukumbu au tungekuwa na jarida kama hivi tunavyoweka katika utalii tungewakumbuka wale wote wa historia wale watu wa sanaa ingekuwa ni jambo zuri sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna vitu vyengine tunakuwa tunavidharau lakini vitu ambavyo vinaweza vikatia uchumi iko siku mimi nitasomesha uchumi hapa japo sina *qualification* ya uchumi lakini ni mbunifu wa uchumi tayari nimeshakuwa *doctor* hapo, kwa sababu udokta si lazima uende katika *theory* bwana, hata katika *practical* unaweza ukawafahamisha watu uchumi ni moja hilo. Tungekuwa na sehemu hiyo tungetia uchumi, tungezalisha Zanzibar kwa *foreign* nyingi sana tu tizama watu wanakuja kuangalia magorofa yale ya *long time ago* yale ya zamani ya mawe hebu nambie.Tizama watu wanatoka nchi za nje wanakuja kuangalia.Ndio maana Mkurugenzi yule wa Mji Mkongwe anakuwa mkali sana kubadilisha umbile la lile jengo. Kwa sababu anajua wazi tunapoteza fedha nyingi. Mhe. Waziri tuwekee kijiji ambacho kitakuwa na historia cha kuonesha kuna kumbukumbu. Unajua kumbukumbu nyingi tumezipoteza hapa Zanzibar kusema ukweli hilo tukubaliane nalo.

Sasa mimi nafikiria kuwa ubunifu unaotumia akili ndio sanaa yenyewe kwa sababu huwezi kuwa mbunifu bila ya kuwa na akili, ni lazima uwe mbunifu wa kutumia akili kubuni kile kitu. Mheshimiwa nikupe hongera kwa hilo japo juu simuoni mtu, simuoni Katibu wako, wala simuoni Mkurugenzi wako na leo tunapitisha kitu kama hiki, sijui baadaye utakuja kujibu nini, eeh hawapo na kama wapo wamejificha.

Sasa hiyo sio tunataka waonekane kitu gani wanachojificha kule, na hii leo ni wizara yao, wao wasikilize jinsi gani waheshimiwa wanavyotoa vitu, wanavyochangia. Sasa wewe uko peke yako, mimi sioni kule kama wapo hakuna hata dalili ya kuonesha kichwa kule, hivyo tunakwenda wapi Mheshimiwa na leo tunapitisha kitu kama hiki. Watanuna hawa Waheshimiwa Wawakilishi kuchangia namna hii na hili ni jambo Mhe. Naibu Spika, kusema ukweli linasikitisha, hawaji sijui kwa sababu gani tofauti na wenzetu kule Bungeni, wakisikia mswada wa wizara yao basi wanajaa mle wanasikiliza kwa kuweza kumsaidia Mhe. Waziri wakati wa kujibu hoja. Lakini leo hawapo kabisa na mpaka sasa hivi hawajaingia kwenye ukumbi, tunachangia nini Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, leo mimi nawasamehe lakini ilikuwa mimi nikatae kuuchangia mswada huu, lakini kwa vile Mhe. Waziri anataka kuniambia jambo lenye msingi.

Mhe. Naibu Spika, nimeangalia sana suala la madhumuni, ni kwamba madhumuni ya mswada huu yanasema ni kufuta sheria za Baraza la Sanaa na Muziki pamoja na sheria ambayo Nam. 1 ya 2009 ya Bodi ya Sensa na Utamaduni wa Zanzibar na kuimarisha utendaji.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ni mazuri sana, madhumuni haya tunajenga msingi wa sheria, sheria siku hizi wanasheria kila siku kukicha sheria zinakuwa zina-*change* na ndio maana siku moja nikauliza hapa Zanzibar tunatumia sheria za nchi gani ambazo angalau zinafanana. Nikaambiwa tunatumia Sheria za Jumuiya ya Afrika. Sasa ikiwa tunatumia sheria zile unajua ukiangalia sana kuna mambo mengine humu nataka nifafanue leo ya sheria ya kusema kuwa katika viwango vile kisiozidi, anasema hivi. Kiwango ambacho kisichozidi shilingi laki saba za Kitanzania au kifungo na nini. Mwanasheria naomba hapo munisaidie, hapa Hakimu atakuwa na uwezo wa kumpa mtu laki moja kwa sababu yeye ameambiwa asiende juu zaidi, kisipindukie lakini sheria hii watakuwepo Mahakimu watatu kwa siku moja au kwa siku tofauti anaweza akahukumu mmoja akaweka laki saba, mwengine akaweka laki mbili, mwengine akaweka hamsini.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana tuweke lugha ambayo ya moja kwa moja *otherwise* pengine nyinyi wenyewe mtakuja kujuta baadae duh! Ilikuwaje, ilikuwaje vipi laki moja, kumbe yuko sawa kwa mujibu wa sheria hii inavyoonesha, ana *right* kabisa kumpa mtu hukumu ya shilingi hamsini elfu. Ndio kwa sababu wewe hukuweka ile *ground* ya kuwaonesha kwamba mimi moja kwa moja itolewe hukumu ya shilingi laki saba *and then* na kifungo chake kiendelee, hapa hamukuweka. Wanasheria tuangalieni hizi lugha wakati mwengine zinapitwa na wakati za matamshi.

Kwa mfano, naweza nikasema kuwa kuna sheria moja ya kusema kuwa Mahakama ya Mkoa haiwezi kutoa msamaha, lakini ya rufaa inaweza. Kwa hiyo, tuangalieni hapa hiyo nitakuja kusomesha baadaye, kwanza nafikiri nataka kutoa kidogo mfano wa hapa lakini hiyo baadae hatari ya sheria hizi tusipokuwa tunaziangalia hatuzipiti mapitio Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria unaniangalia inavyoonesha hiki kitu kweli kimeku-*touch* na ndio ilivyo, kwa sababu kila baada ya muda tuweze kuangalia sheria zetu huko wenzetu kama vipi zina-*change* kila baada ya muda. Kwa hiyo, hili suala mimi nafikiria tutakuja kuliangalia baadaye.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwanza nikubaliane na moja kuwa katika kufanya *registration* mimi naamini Mheshimiwa sijui kama unazo *data* hizi. Kwa kweli una vikundi vingapi? Wapiga disko, watu wa sanaa na wengineo, mimi sidhani kama tunacho kitu hicho unaweza kuja kuniambia rasmi tu lakini *okay* haina tatizo itakuwa umeshanisaidia, nishajua Zanzibar sasa hivi tuna wasanii wangapi, wapiga disko wangapi, wacheza ngoma wangapi, wachonga vinyago wangapi na halikadhalika, hiyo utakuja kunisaidia baadaye.

Mhe. Naibu Spika, na kwa nini nikasema hivi? Kwa sababu hatuna utamaduni wa kuweka kumbukumbu zetu na siku hizi taaluma zipo katika mambo ya kompyuta; *database* kuweka vitu kama hivi hatuna hii Mheshimiwa. Sasa mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri njoo uniambie hizo lakini wewe utaniambia tu nikukubalie na nitakukubalia kwa sababu unajua ndio kwanza uanze katika wizara hii, ulikuwa katika Wizara ya Mifugo hapa *alhamdulillah* ningekwambia wafugaji wangapi ungenitajia kwa ghibu, sasa kule ndiko ulikoanzia na ulipopata kuchukua *CV* kule kutokana na utendaji wako ulivyokuwa mzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi kule nchi za wenzetu wanakuwa wanaweka mafungu *special* kwa kuwasaidia wale au kwa kuwainua wale wasanii wadogo ili kuwaweka katika *standard* ya juu. Sijui wewe Mheshimiwa bajeti yako iko kifungu hicho na kama hakuna basi ningekuomba kama ulivyotengeneza sheria hii na wewe uwatengeneze, kwa sababu sasa hivi Nigeria wanainuka kwa mambo haya ya filamu tena imekuwa nchi tajiri acha mafuta na mambo mengine. Lakini tizama sasa kanda zao zinavyonunulika lakini Zanzibar hakuna jambo hilo, tulikuwa nalo zamani kina Makombora wale, Halikuniki tulikuwa na michezo mizuri sana mheshimiwa unaona hatari hii yetu ya Zanzibar ni kwamba hatuwaendelezi. Sidhani na sijui Mheshimiwa angalau ipo siku kama uliwaita hawa ukaongea nao na ukawajua nini tatizo lao, sidhani kama hiki kitu mlikifanya hicho. Sidhani lakini ninakuomba kama umefanya ni kwa siku ngapi uliozungumza nao.

Mhe. Naibu Spika, tunatunga sheria lakini mimi huwa nacheka sana maana yake nimekwenda kwenye kama alivyosema Mhe. Haroun siku moja kuna makamusi ya Kiswahili, lakini mimi nimekwenda katika ma-*dictionaries* duniani ili kuangalia jinsi gani ambavyo sisi sheria zetu tunavyozipitisha katika chombo kikubwa kwa mujibu wa Katiba yetu, halafu leo zinakuwa hazifanyi kazi. Hapa mimi natafuta kwa nini najiuliza sana tunatunga sheria tena nzuri sana. Katika *East Africa* labda na sisi tunaweza tukawa katika nchi ya mwanzo inayobadili sheria kila baada ya

muda au kila baada ya siku, kila baada ya mwezi, kila baada ya mwaka ni Zanzibar. Lakini Mheshimiwa utendaji wake sasa, mimi hapa natafuta ni sababu zipi zinazofanya tusiweze ku-*take action* ya kufanya sheria zetu zifanye kazi vizuri.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri naomba sana hii itapita tu usiwe na wasi wasi wowote, lakini mheshimiwa tunakuwa na onesho kubwa sana la sauti za busara. Mhe. Naibu Spika, nitamuuliza suala hapa Mhe. Waziri hebu niambie vikundi vingapi vya Zanzibar unavishirikisha kuingia kwa sababu pale ndipo unajitangaza, pale ndio unawatangaza Wazanzibari. Hilo nataka unijibu Mheshimiwa uniambie kuwa vikundi vya aina gani na gani vinakwenda pale vya Kizanzibari, tunaona vikundi vya wenzetu tu *Mainland* tu hapo kwa mjomba na wengine kutoka Kenya, Congo na kadhalika, Amerika na sehemu nyengine. Lakini Zanzibar sijui ni wangapi maana yake sitaki nikusemee, nikisema mimi itakuwa haina maana hata kuchangia. Sidhani kama tunapita angalau *number one* mpaka *number two* na ni kwetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kunakuwa na maonesho kama haya katika nchi za wenzetu tunawapeleka, tunajishajihisha vipi, tunakusanya vipi kuwapeleka hawa vijana wetu. Leo wenzetu Bara unasikia leo nani kaenda Marekani, nani kaenda Uingereza kwa nini sisi Mheshimiwa tunashindwa, ni sababu zipi.

Mhe. Naibu Spika, ni sababu zipi ambazo Zanzibar tunashindwa kufanya jambo letu wakati Rais amejenga *studio*, mheshimiwa tunashindwa nini? Na mimi niseme kupigania mimi hapa huwa nashangaa sana mheshimiwa na inanisikitisha sana tena sana. Ninaomba sana hebu tuwe *serious* na *government* kwa sababu tukiwa *serious* na serikali *it means* na wananchi tutakuwa nao *serious*. Lakini hatuko *serious* na *government* ina maana *sorry* Mhe. Naibu Spika hatutokuwa *serious* na wananchi. Tuna vijana na wao walijitokeza na wao walikuwa sawa kama wale wenzetu kule kina *Ze Comedy* au *Futuhi*. Sisi hapa tuna vijana ambao wanaita Kombora la wiki. Wamekuwa wanafanya vizuri sana wale watoto, lakini tumewavunja moyo hatukuwapa *support*, hatukuwaendeleza zaidi kuwapa taaluma za elimu na mambo mengine tumewaacha halafu leo tunaleta sheria.

Mhe. Naibu Spika, zamani kulikuwa na sheria mzungu tu akishuka pale *Airport* au bandarini anapewa kanga za kuvaa na anafundishwa. Mhe. Waziri sheria hii ndio inaelekea huko, tena wazungu wenyewe wanapenda na wanahusudu kuvaa kanga, akaambiwa hii ndio *culture* ya Zanzibar anahusudu tena kila unapomfunga yeye anafurahi kabisa. Mimi juzi nilimuona mzungu mmoja nilicheka sana nilifurahi, lakini nimesahau ile lugha ya kumwambia pale jinsi vile alivyovaa aliisanifu kanga na kuifunga, aisee yule sema ile *white colour* inaonesha, lakini ingekuwa *black colour* ningesema Mzanzibari halisi. Kwa kweli ame-*enjoy* kabisa ameifunga kinyumbani kabisa anatembea Stone Town.

Mhe. Naibu Spika, leo ukianzisha sheria hiyo kwanza kina mama watafanya biashara nzuri za kuuza kanga, umeshaondoa ajira ya kina mama kurandaranda haidhuru na kina baba tofauti maana yake mimi baba kanga saa nyengine inakuwa ah ile kutembeza tembeza Mhe. Naibu Spika huona tabu sana lakini kanga zenyewe ni kina mama ndio wanajua *quality* hizi, wanajua misemo. Hii sheria nayo tuone hapo unatengeneza mambo mawili katika sheria yako, umetengeneza kuwakumbusha watu utamaduni wa Zanzibar hawatakiwi watu waende ovyo, wavae vinguo nusu uchi.

Lakini pili umefanya biashara sasa hivi ambayo wale kina mama watakaouza kanga zao kwenye sehemu za utalii zitoke haraka haraka. Mhe. Naibu Spika, hapo Mwenyezi Mungu atakupa yenye kheri na wewe kutokana na sheria hii. Mhe. Naibu Spika, naomba sana hilo suala kuliangalia kwa makini.

Mhe. Naibu Spika, tumesema mnataka sasa hivi kumbi za kisasa, hamuwezi mkapitisha kumbi za ovyo ovyo. Nakubaliana nalo lakini kuna *modern* sasa hivi za kumbi za kisasa unaweza ukazitengeneza na watu wakavuvitika kwa sababu ni sanaa. Mimi nataka hii sheria muiangalie vizuri, ni sanaa kwa sababu kumbi sio lazima *tiles* kwa kuwa *tiles* imejengwa vizuri ukasema hii ndio ya kisasa. Lakini unaweza ukatengeneza ukumbi *model* ya kizamani kabisa *without tiles* na ikawa tayari ile umetoa ubunifu wa sanaa katika ile kumbi na watu ooh. Mheshimiwa hapo itakuwa ni *good* kabisa, na hasa hizi msizisahau hizi, hizi nazo naomba kabisa watu wako hao makamisaa hao wanaopita wakaangalie na kutaka kutoa hukumu, msije mkahukumu hawa ni muundo tu. Unajua kila mtu na biashara yake anavyoitengeneza, ukiitengeneza biashara yako vizuri hasa watu wetu kutoka nchi za nje unajua kuna wengine nchi zao hakuna mapaa ya makuti wanapata Zanzibar. Ni kweli kabisa Mhe. Naibu Spika watu hawana yale mapaa ya makuti wanakuja Zanzibar kuyafuata kwa sababu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu sasa nataka nikwambie samahani sana na-*quote* na mimi utamaduni wa nchi za wenzetu. Nilivyokwenda Spain Mheshimiwa nimekwenda katika kumbi ambazo zenye starehe za madisko, unapita nje huwezi kuamini kama kunapigwa disko, kuko kimya lakini ingia ndani huko usikilize vitu ukumbi unalia hivi, kudu, kudu, kudu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa nakubaliana nalo hawa wanaopiga kelele mitaani kweli, watu siku hizi *pressure* zenyewe zinataka sababu. Mhe. Naibu Spika, *pressure* zinataka sababu siku hizi neno kidogo *pressure* mara huu, je, ukipiga ule mziki maana usifanye mchezo miziki mengine utasema kama hili jumba litaanguka, tu,tu,tu linavyonguruma. Sasa mimi nafikiria Mheshimiwa mimi nakubaliana nalo wenye mahoteli ni kweli lazima wapige disko ndio wapate *market* nakubaliana lakini watengeneze mazingira ambayo itakuwa haikeri wengine, hii nakubaliana nayo.

Mhe. Naibu Spika, na halafu siku hizi mmeweka *limit* ya kwisha kibali kwa muda wa mtu kushereheka. Hapa kidogo kwenye mahoteli ningeomba waachieni wenyewe kwa sababu wale kule wamekata vibali vyao, wamefanya na kila kitu hii nayo muangalie msimuwekee leo unamwambia mwisho saa tano, mwisho saa tano yeye anakulipa kodi, analipa mambo chungu nzima.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tugeuke tutafute maeneo ya *outside* za nchi yenyewe maana yake Zanzibar sijui niseme *Stone Town* iko wapi hata sijui nashindwa kufahamu. Jana nilisahau kumwambia Mhe. Waziri atutafutie mji ambao unakwenda na kisasa maana yake Zanzibar nashindwa.

Siku moja niliulizwa mheshimiwa *town* iko wapi Zanzibar, ilibidi nimeshindwa kusema, nikisema Kwahani *town* itasemekana kweli *town* kwa sababu haina *definition* ile, haina sehemu ya kuonesha maalum iko wapi, hiyo ni kweli *I am serious* Mhe. Naibu Spika nimeshindwa kuieleza *town* ni wapi Zanzibar. Kwa sababu sasa hivi ukienda Bububu *is a town*, ukienda Kiembesamaki ni *town* lakini nashindwa wapi hasa kusema *town* kwa sababu *town* ina *definition* zake za kuonesha kama ni *town*. Sasa nayo hii ningeomba mheshimiwa nilisikia wakati fulani kuna maonesho uwanja ule wa mwenye biashara atakuja kuniambia Mhe. Waziri tutaekewa eneo la mambo ya maonesho ya biashara, *yes* ndio twende huko. Lakini sijui mpaka leo imeishia wapi ule uwanja sijui kama haujapatikana haujatua hapa Zanzibar, sijui vipi atakuja kunieleza siku ya ripoti zake za kamati kwamba bado upo katika nchi za nje huko haujatua hapa, tutakuja kuonana huko.

Mhe. Naibu Spika, nalo hili kwa kupunguza sheria hii ili isigombane na watu waondoe siku hizi kuna wanaitwa Chukwani vijana wanaita Entebbe, watu siku hizi wanaelekea Entebbe hivyo ndio inavyotakiwa uende huko huko shauri zao na Entebbe yao huko. Wako masafa marefu na *town* ndio hiyo nashindwa sasa, *town* yenyewe iko hapo Mazizini sasa *far away* na pale sijui itakuwa vipi sasa lakini Entebbe Mheshimiwa. Sasa watu wanakwenda huko ukienda wewe mwenyewe umeyataka mwenyewe utakayoyakuta kule nani kakwambia uende. Ndivyo na ndio maana sheria hii usifuate mambo ambayo yaliyokuwa hayakuhusu kwa nilivyofahamu mimi kama wanasheria watanikaidi haya nimekwenda kwenye madhumuni mimi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimezungumzia madhumuni anasema ghasia zinazosababishwa na ngoma zinazopigwa kwenye makaazi ya watu hadi usiku wa manane na pia kuwashirikisha watoto wenye umri. Entebbe leo mtoto anakwenda kule anatafuta nini kama si mbea, anapelekwa kwenda kufanya nini Entebbe ni mbali kule na mji, lakini hawa waliokuwa wenye utalii kwenda kwenye vijiji vyetu ambao *special* vijiji tangu na asubuhi mheshimiwa weka sheria nakubaliana nayo, ukimuona mtoto tia ndani mwambie mzazi kwa nini ukamruhusu. *Yah*, hapo mimi nakuunga mkono na naku-*support* sana waachie wenyewe halafu na wazazi na wao hivi kweli mtoto wako ana umri wa miaka miwili, mitatu au minne, kweli ndio ana mvuto tu ule wa ugoma kule wewe umelala ndani inaonesha huyu si mtoto wako nakataa sana mimi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo mimi sheria hii nakubaliana nayo halafu la pili anasema kushindwa kulinda mila, silka na maadili kwa kutodhibiti maonesho ya sanaa yenye vitendo viovu. Nakubaliana nako kabisa, sanaa hairidhishi si vizuri kukaa wewe muimbaji unavaa nguo za kuonesha uchi pale kwa kweli si jambo zuri, vaa vazi lako zuri tengeneza *model* ya kisanaa lakini hakuna sheria hiyo ya kusema kuwa vazi la kisanaa liwe la uchi au nusu uchi, hiyo mimi nakataa wanajifanyia tu watu, sijui inakuwaje biashara ile. Watu wanachotaka pale ni sauti yako, minenguo yako hawataki kukuona vyengine vyovyote. Sasa mimi ningeomba hii sheria kwa kweli iwe kali sana.

Mhe. Naibu Spika, ningeendelea lakini naona kuna mwenzangu na yeye ana uchu kwa dakika zilizobakia niweze kumbakishia.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie na kumalizia kwangu ni katika hizi filamu za ngono. Nakumbuka kipindi fulani yule Mkurugenzi wa Hatimiliki mwanamama yule alilipiga vita kweli hili suala na watu wakafikia kumtishia amani ya kutaka kumuua, wanampelekea *messages* kwa sababu wanasema anawazibia rizki zao kutokana na zile filamu.

Mhe. Naibu Spika, hizi filamu huwa zinauzwa katika sehemu za kuuzwa kanda au kukodishwa, mule mnataka kufanyiwa *research* kubwa, unaweza kuwekewa kanda ya Bi Kidude ukasema hii ni nyimbo ya Bi Kidude kumbe sasa sio hilo, nataka kukwambia ukweli wewe huwezi kujua, lakini wenyewe wanajuana wanawaambia ndio hiyo. Mheshimiwa wanaharibu majina ya watu wetu kwa kutumia kanda zile, sheria imewekwa shilingi milioni mbili lakini ushauri wangu tunapokuwa tunaweka sheria kali ndipo tunaposema karipio linakuwa ni kubwa sana, hiyo adhabu ya shilingi milioni mbili ni kidogo sana.

Mimi nashukuru sana kuwa mmesema ni moja kwa moja analipa shilingi milioni mbili nakubali tamko hilo lakini sio isiyozidi, ukisema isiyozidi Jaji atahukumu anavyotaka mwenyewe.

Halafu adhabu nyengine ya kifungo ni miaka miwili, miaka miwili sawa sawa na siku mbili tu hizo. Wanasheria msiwe wabishi katika kuweka suala la hukumu ya jambo, unajua unapoweka kitu weka kitu kigumu sana. Mimi keshokutwa ninakuja na sheria ya wabakaji, nataka nije nayo hapa keshokutwa lakini hii msiweke shilingi milioni mbili tu, shilingi milioni mbili simu sipati unamuwekea mtu, hebu tuone kiwango ambacho kitaweza kum-*touch* mtu kwa kanda moja tu analipa shilingi milioni tano, anakwenda ndani miaka 10 atakuja na kanda kweli? Haji na kanda.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha sana na nimalizie maana naona kule juu watu wanachungulia tu kwa woga sijui wanakuwa na woga wa nini. Mimi nimeikubali sheria hii kwa asilimia mia moja nashukuru sana, sijui atanisaidia nani katika kujibu swali maana hapa tutapiga buti kweli kweli kwa sababu namjua Mheshimiwa atashindwa kujibu maswali haya na hana wa kumsaidia kule wote wako juu wamejificha wanachungulia mmoja mmoja tu, nishamuona mmoja kachungulia.

Mhe. Naibu Spika, nimeunga mkono asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie machache katika mswada huu ambao unakusudia kuweka masharti mazuri ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, pili nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nami kusema machache, lakini kabla sijaendelea nimpongeze Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa mchango mzuri ambao ameutoa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia nimpongeze Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla kwa kuleta mswada huu na kuwasilisha pia kwa ufasaha. Lakini jengine kwa mara nyingi sana Wajumbe wa Baraza hapa hasa akiwemo Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe. Jaku Hashim Ayoub wamekuwa wakizungumzia sana suala la mporomoko wa maadili katika nchi yetu hasa kwa upande wa vijana wa kizazi hiki cha sasa, lakini hata wadau mbali mbali nje ya Baraza kama *NGO's*, wazazi na hata Taasisi za Serikali na za Kidini zimekuwa zikipigia kelele sana juu ya mporomoko wa maadili katika nchi yetu na mashekhe mbali mbali akiwemo Sheikh Nyundo japo wakati mwengine anakwenda mbali zaidi, lakini anasaidia katika kurudisha watu kwenye mstari.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali hii mara nyengine huwa sikivu *somehow*, na kwa kuwa wamesikia zile kelele ambazo zimekuwa zikipigwa na Waheshimiwa lakini pia na watu wengine wa nje imeamua sasa kuchukua hatua za makusudi ili kuona kwamba yale maadili ambayo yanapigiwa kelele sasa yanarudi katika mstari.

Kwa mantiki hiyo nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwanza kwa hatua ambayo wameichukua kupitia *organization* yake ya USEWAZA, Umoja wa Serikali za Wanafunzi wa Zanzibar kwa hatua ambayo wanaichukua juu ya kupiga marufuku matumizi ya simu kwa wanafunzi wakiwa skuli.

Vile vile, pongezi hizi nizipeleke kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri ambayo imeifanya kwa kulea wizara hizi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kulea wizara hizi kuona kwamba yale mambo ambayo wananchi wanayapigia kelele basi yanarudi katika mstari na kuishauri serikali vizuri kuona kwamba haya mambo yanakaa sawa. Pia niiombe serikali kuunga mkono umoja wa wanafunzi wale katika jitihada zao ambao

wanazichukua ili kuona kwamba yale matumizi ya simu ambayo ndio sababu kubwa inayopelekea matumizi ya *smart phone*s ambayo ni sababu inayopelekea kwamba hawa wanafunzi ambao ni vijana wa sasa wawe wana *access* na hii mitandao.

Mhe. Naibu Spika, kama msomi mmoja alivyosema kuwa *globalization turn open window,* yaani ukifungua lile dirisha *fresh air* inapita lakini mbu na vumbi pia linaingia. Kwa hiyo, utandawazi ni mzuri kwa kiasi fulani lakini kwa upande mwengine kwa kweli inakuwa ni hatari hasa kwa vijana wetu lakini pia kwa maadili yetu ya Kizanzibari.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo Mhe. Makame Mshimba amegusia maeneo kadhaa na mimi naomba nigusie maeneo hayo ambayo ameyagusia ili kukazia ili serikali ione kwamba ni maeneo gani ambayo yanatakiwa kukaza buti na kuona kwamba yale maadili yetu yanarudi katika mstari.

Mhe. Naibu Spika, siku hizi kumetokea tabia ya kuuza *alcohol* kiholela, yaani kila kona kuna baa na watoaji wa vibali hivyo ni hao hao serikali. Kwa hiyo mimi naamini kama wanavyotoa vile vibali pia wana uwezo wa kuzi-*control* zile baa za kiholela ambazo hazitambulikani ili kuepusha baa bubu Mhe. Makame Mshimba ananambia, ili kuepusha hawa vijana wetu kwenda kununua hizi *alcohol* na baadaye kupelekea kufanya mambo mengine ambayo sio maadili kwa Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, mimi wakati ninasoma nimekaa nchi za watu huko, huko serikali ilikuwa inajitahidi sana kuona kwamba wale ambao wanauziwa pombe ni wale wanaoruhusika tu kuuziwa pombe na hilo waliliweza. Kwa sababu waliweka sheria ya kwamba mtu aki-*walk* kwenye baa au sehemu ambayo kunauzwa pombe muuza pombe anatakiwa kuhakikisha kwamba yule anayemuuzia ameshafikia umri wa miaka 18 kwa mujibu wa sheria yao. Nafikiri na sisi kwa mujibu wa sheria yetu miaka 18 tayari mtu ameshavuka ule utoto. Kwa hiyo ni vyema wakatambulisha kitu kama hiki, sijaona katika sheria lakini naamini sheria hii inampa uwezo Mhe. Waziri kifungu cha 54 kutunga kanuni, kanuni ambazo zitaweka masharti ya kutekeleza sheria hii. Kwa hiyo, mimi nafikiri kitu kama hicho kingelielezewa hapa angalau wale watakaokuwa wana *access* ya kunywa itakuwa ni wale ambao wanaruhusika tu.

Jengine kama kweli serikali inataka kurudisha na haitorudisha kama ilivyokuwa mwanzo, lakini angalau itapunguza makali katika huu uuzwaji wa pombe kiholela ni sambamba waka-*introduce* kitu kama hicho. Pia sambamba na kuweka masharti mahususi katika *night club*, katika ma-*disco* ambayo Mhe. Makame Mshimba ameyazungumzia.

Mhe. Makame Mshimba amezungumzia kuhusu Entebbe sitaki kuingilia mambo ya watu, lakini mimi bado kijana wakati mwengine nikikumbukia ujana huwa napita sehemu hizo. Kwa hiyo, aliyosema Mhe. Makame Mshimba ni ya kweli na mimi binafsi nishawahi kufika lakini mambo yanayotokea huko nasema tena sitaki kuingilia mambo ya watu haujanipeleka umbea zimenipeleka starehe zangu, lakini mambo yanayotokea huko ni ya ajabu na nilitaka kwenda baada ya kusikia maneno inavyozungumziwa hiyo sehemu, japo ipo mbali na watu lakini kwa kweli mambo yanayofanyika huko sio kabisa. Baada ya kwenda siku ile nikajiuliza hizi siku za mbele zinazokuja mambo haya sijui yatakuwaje kama serikali italifumbia macho jambo lile.

Mhe. Naibu Spika, kuna watoto wadogo, yaani ukimuangalia tu unamuona huyu mdogo lakini mavazi yanayovaliwa huko na matendo yanayofanywa kwa kweli inasikitisha, yaani huwezi kusema uko Zanzibar kama uko Texas au Miami**.**

Kwa hiyo, naomba serikali hili ilichukue na ilichukulie *serious* kabisa, japo kwamba wenyewe wanasema yule mtu ana kibali na kila kitu lakini ni vizuri wakaweka masharti katika hizi *night clubs* nikimaanisha madisko ili kuona kwamba yale maadili ambayo Zanzibar yalikuwanayo yanarudi katika mstari.

Jengine pia nichukue fursa hii kutoa wito kwa wazazi, wazazi wawe makini sana katika kuwalea watoto wao ili kuona kwamba nao wanasaidia serikali katika kurudisha maadili ya nchi yetu. La pili niseme kwamba, kama nilivyosema mwanzo kuwa serikali hii sikivu, na kwa kuzingatia zile kelele ambazo zilikuwa zinapigwa na wananchi na wadau mbali mbali, imechukua hatua ya kuleta mswada huu ili kuona kwamba kunawekwa masharti mazuri na utaratibu wa kuona kwamba sasa mambo yanakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nimepitia haraka haraka nilipopata huu mswada jana lakini nimeona kuwa mswada hauko *strict* sana kama kweli tuko *serious* tunataka kurudisha hali ya Zanzibar ilivyokuwa, lakini niseme tu hatuwezi tukaweka kila kitu kwenye sheria, lakini naamini kama nilivyosema kwamba Mhe. Waziri ana uwezo wa kutunga kanuni ambazo zitaweka masharti mazuri ya utekelezaji wa sheria hii. Kwa hiyo niseme tu kwamba, anapokwenda kutunga hizo kanuni awe makini sana. Sisi Baraza *on our behalf* tunamuamini yeye kwamba atatunga hizi kanuni, na kanuni atazitunga vizuri ili kuona huu utekelezaji wa sheria unakwenda vizuri na sheria inafuatwa kama ilivyowekwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba niingie katika vifungu vya mswada huu. Katika kifungu cha 6(b) kinachosomeka kwamba mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza ikiwa ana uzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa. Mapendekezo yangu ni kwamba, uzoefu huu ungeliwekwa wazi angalau tukajua uzoefu wa miaka mingapi. Mimi kwa mapendekezo yangu napendekeza miaka mitano angalau mtu awe ana uzoefu wa miaka mitano. Kwa mantiki hiyo kifungu hiki sasa kisomeke kwamba, ana uzoefu angalau usiopungua miaka mitano katika mambo yanayohusiana na sanaa. Kwa sababu tukiacha kama ilivyo katika mswada neno uzoefu bila kuliwekea muda maalum linaweza kutumika vibaya.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho ya pili ni katika kifungu cha 24(2). Katika kifungu hiki mimi sikiungi mkono na sikiungi mkono kwa sababu kifungu cha 24(2)(iv) kinasema "*...uamuzi wa waziri utakuwa ni wa mwisho*". Mimi sikubaliani na hili na sikubaliani nalo kwa sababu linapingana na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 katika kifungu cha 134(8) ambacho kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba nikisome.

Kifungu 134(8) kinasema kwamba;

> "Katika kifungu chochote cha Katiba hii kinachosema kwamba hakuna mtu au chombo fulani kitachoingiliana na mtu au chombo chochote katika kutekeleza kazi zake basi hakitokuwa na maana ya kwamba Mahkama zitazuilika katika mamlaka yake katika suala lolote hata kama mtu huyo au chombo hicho kimetekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyengine yoyote".

Kwa mantiki hiyo siungi mkono na kwa sababu siungi mkono kifungu hiki kinampa waziri *power* kuwa yeye ndiye *final say,*kwamba yeye ndiye mwenye mamlaka ya mwisho.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa kifungu hiki cha Katiba uamuzi wa mwisho utakuwa ni wa Mahakama na si chombo chengine chochote tu au mtu mwengine yeyote. Kwa hiyo, napendekeza kifungu chengine kidogo cha (4) kiongezwe ambacho kitasomeka, "Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa waziri anaweza kuomba kufanyiwa mapitio ya uamuzi wa waziri katika Mahakama yenye mamlaka". Kwa sababu tunaamini kwamba Mahakama kule japo kuna mambo mengine yanafanyika lakini tunaamini kwamba Mahakama ndio inatoa haki ya mwisho. Kwa hiyo, yeyote atayekuwa hakuridhika na uamuzi wa Baraza anaweza kwenda kwa waziri lakini pia asiporidhika na uamuzi wa waziri apewe fursa ya kwenda kwenye Mahakama ambayo ina uamuzi wa kusikiliza hilo shauri.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyopendekeza aidha tuongeze kifungu au tuiache hivi hivi tupitishe kifungu ambacho kinakinzana na katiba, ambapo siko tayari ili kifungu hiki hata kikipita baadae tunajua kwamba katiba yenyewe ita-*prevail,* lakini naomba tuongeze kifungu hiki ili tusipitishe sheria ambayo inakinzana na katiba.

Vile vile katika kifungu cha 38(2) kinachosomeka;

> "Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kikundi chochote cha utamaduni kitakachokwenda kinyume na masharti yaliyotolewa kwa nyumba za kuonesha maonesho kitakuwa kimetenda kosa na kikitiwa hatiani kitalazimika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tatu za kitanzania au kufungwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu".

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninajiuliza kikundi kitafungwa au kitafungiwa? Ninamuomba Mhe. Waziri akija anipe maelezo kidogo na bado najiuliza kama kitafungwa kikundi kwa maana ya kikundi au waliosajili kikundi? Kwa sababu kukifunga kikundi kwa maana ya kikundi itakuwa haiwezekani, lakini kuwafunga waliosajili kikundi inawezekana.

Kwa hivyo, mimi naomba kwamba kifungu hiki kingelieleza wazi, kwa sababu kwenye adhabu hii ya kifungu inaweza kuleta utata kwani ndani ya kikundi mara nyengine kunaweza kukawa na watu tu ambao wameajiriwa. Sasa

ukisema unakifunga kikundi utakuwa unawafunga watu wengine ambao hawana hatia lakini kama utasema utafunga waliosajili kikundi itakuwa unawafunga wale wenye kikundi. Lakini kama utasema utakifungia kikundi kufanya kazi zake hapo itakuwa hukufanya usawa kabisa.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kifungu cha 47 ambacho pia Mhe. Makame Mshimba alikigusia ambacho kinasema kwamba:-

Mtu yeyote atakayetengeza au kushiriki katika kutengeneza, kusafirisha, kuchapisha, kutangaza, kuuza, kuingiza nchini kutoa nje ya nchi au kusaidia kwa njia yoyote upatikanaji wa picha cha ngono zinazodhalilisha watoto atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini ya shilingi milioni mbili za Tanzania au kifungo cha miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono sana kifungu hiki, na niombe tu Serikali inapojaribu kurekebisha kama kweli wanataka watoto wapate haki zao inapojaribu kurekebisha sheria nyengine basi ziwe zinatizama zile sheria nyengine za ushahidi. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, katika kazi zetu za Kamati ya Katiba na Sheria kuna kipindi tulitembelea Afisi ya *DPP* pale na pale kuna kesi nyingi za haya mambo ya kudhalilisha watoto na tulikuta kesi moja ambayo imesita, na imesita kwa sababu ilikuwa inasubiri *ruling* kutoka Mahakama ya juu kama hii ni *document* au sio *document*.

Kwa hiyo, ile kesi ikawa imeganda haiendi na *ruling* kutoka Mahakama za juu haziji. Kwa hiyo naomba Serikali kwamba inapofanya marekebisho ya hizi sheria nyengine basi ni vyema ikatizama na zile sheria nyengine ambazo zinawatia hawa watu hatiani, kwa sababu mara nyengine watoto wanakutwa na kesi kama hizo, lakini mtoto tangu yuko 16 au 17 mpaka anafika 18 kwamba ameshaingia hatua nyengine tena sio mtoto tena bado hajapata kesi yake, bado hajapata haki yake na kesi bado inakuwa haijasikilizwa.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, niombe sana Serikali katika hili izingatie na naamini kwa kuwa imesema mara nyengine hawa wanakuwa wasikivu basi naomba na hili walisikilize na wakalifanyie kazi.

Baada ya kusema haya Mhe. Naibu Spika, nitaunga mkono baada ya kusikiliza maelezo ya Mhe. Waziri, nashukuru. (*Makofi*)

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukakutana hapa leo tukiwa na afya njema. Pia, naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa pamoja na watendaji wake kwa kutuletea Mswada huu ambao nia zetu na imani zetu kuwa Mswada utakuwa ni mkombozi wa Zanzibar hii na vilivyomo ndani ya Zanzibar hii.

Mhe. Naibu Spika, nataka nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri katika ukurasa wa 390 kifungu cha pili baada ya kuzungumza Wajumbe wa Baraza watakaochaguliwa katika nafasi zao na akakiri kuwa Waziri atazingatia usawa wa kijinsia. Naomba nikupongeze katika hilo kwa sababu hili ni jambo tunalolipigia kelele muda mrefu la kufuata usawa wa jinsia, nakupongeza katika hilo.

Mhe. Naibu Spika katika ukurasa huo huo kifungu cha 7 kuna kazi za Baraza. Kuna mtiririko wa kazi nyingi za Baraza ikiwemo (b) Kuhifadhi, Kulinda na Kuimarisha mila, silka na maadili au utamaduni wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kuwa Baraza litakuwa na kazi ngumu. Miongoni mwa kazi ngumu zitakazokuwa nazo Baraza mojawapo ni hii ya Kuhifadhi, Kulinda, Kuimarisha mila, silka na Maadili ya Utamaduni wa Kizanzibari.

Mhe. Naibu Spika, tunapiga kelele muda mrefu sisi Wajumbe wa Baraza, wazee wetu walioko nje ya Baraza kwa jinsi ya mmong'onyoko wa maadili ulivyopungua ndani ya nchi yetu. Sasa sheria hii nina imani kama itafuata kweli kweli maagizo yake aliyapanga humu basi tutafanikiwa kwa sababu Mhe. Naibu Spika, maadili wamemong'onyoka

kweli katika mambo tofauti vijana wetu wanapoteza maadili ya nchi yetu katika mavazi hata usemi wao sasa hivi umebadilika umekuwa wa kudharau hata familia zao mtu baba yake anamwita "*dingi*" mavazi ni ya ajabu.

Kama alivyozungumzia Mhe. Wanu Hafidh Ameir hapa mambo ya simu imekuwa ni balaa. Mtu anazungumza na simu au ana-*chart* kwa mambo ya watoto wa mjini mpaka baba yake anamuagiza kiti yeye habari hana kama hayupo. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri katika hili waisimamie sana sheria hii hasa katika kifungu hiki katika kufanikisha lengo la sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, nataka nije katika ukurasa wa 399 sehemu ya nne kwenye maombi ya Kibali. Mhe. Naibu Spika, utoaji wa kibali ndio chanzo za kupata mafanikio au cha kukosa mafanikio kwa kuporomoka maadili yetu. Sasa hapa wameelezea mambo mengi kuna mambo kama matatu Sheha atakuwa na jukumu la kutoa vibali kwa ajili ya shughuli zote zinazohusiana na upigaji ngoma, maonesho ya sanaa na maonesho ya Jukwaani, Burudani yanayofanyika katika Shehia yake. Sehemu ya tatu kifungu kidogo (3) kinasema;

"Malipo yanapaswa kutolewa."

Sasa hapa naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze malipo haya ya kibali yatakayopendekezwa ni kwa kiwango gani na ni nani atapendekeza malipo haya.

Mhe. Naibu Spika, nikija sehemu ya sita kwenye leseni na Usalama wa Nyumba za Maonesho. Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kama katika nyumba za maonesho usalama mara nyengine unapungua zinatokezea hujuma mbali mbali katika nyumba za Maonesho. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri katika hili la kutoa leseni basi paangaliwe sana masuala ya muda wa leseni kwani muda wa leseni ukiwa mrefu sana labda pawe na sheria nzito ya kufanya mtu huyu baada ya kukiuka haya mambo anyang'anywe hii leseni, lakini tukiendeleza tuweke tu leseni kama miaka mitano miaka sita, saba, minne hivyo itakuwa ngumu. Kwa hivyo, leseni isiwe ya muda mrefu kama kuangaliwa mtu katika hali ya utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, nataka nije katika ukurasa wa 405 sehemu ya Madhumuni na Sababu. Nikija kwenye Madhumuni na Sababu ya Mswada huu au Sheria hii kuna mengi aliyoyazungumza Mhe. Waziri mimi hapa nataka nije sana katika ukiukwaji wa Maadili na Silka za Kizanzibari, naendelea kutilia mkazo hapa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, katika ukiukwaji huu wa maadili na Silka za Kizanzibari kuna mambo mengi. Hapa nakumbuka alizungumza Mhe. Makame Mshimba lakini nilikuwa mdogo lakini nilikuwa na kumbukumbu yangu nzuri tu wazee wetu huko nyuma walikuwa wanavaa nguo fupi kupindukia. Lakini baada ya Marehemu Mzee Abeid Aman Karume kutoa agizo la kuwa kuvaliwe nguo refu na atayeonekana kama amevaa nguo fupi ataadhibiwa basi kazi ile ilikwenda vizuri na nchi yetu watu wakawa wanabadilisha mavazi, kwa sababu mavazi pia ni kivutio kimoja kikubwa cha kuvunja maadili yetu walizungumza sana wezangu waliopita kama mtu anavaa nguo lakini kilichomo ndani ya mwili wake chote kinaonakana.

Sasa hapa kiukweli Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alisimamie kweli kweli hili pamoja na taasisi yake husika waliyoandaa rasmi sheria hii kwa nia njema ili Zanzibar yetu iokoke na haya mambo yaliopo ya kupita tukiambiwa kuwa kama hii Zanzibar ya sasa sio za zamani na ukizingatia ni hakika Zanzibar sasa imebadilika.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye wamiliki wa mabaa. Mhe. Naibu Spika, hawa wengine wanafanya kazi bila ya kutumia sheria na nataka nimwambie Mhe. Waziri kuna malalamiko ya muda mrefu sana katika eneo la Jimbo la Amani wananchi wa Amani walipiga kelele sana ndani ya eneo lao, kuna mabaa manne lakini mawili yako karibu sana na majumba wanayoishi wananchi wetu. Nataka tukubali Mhe. Naibu Spika, ndani ya maeno yetu wamo watu wazima maana yake wazee maradhi ni mengi, kuna watoto wachanga na wale waliomo ndani ya mabaa haya yalioko karibu na majumba wanafanya fujo vibaya mno, wanapiga ngoma kuanzia saa mbili mpaka saa nane za usiku ngoma hizi wanapiga kwa sauti wanayoijua wenyewe sio ile aliyoitolea mfano Mhe. Makame Mshimba katika

matembezi yake ya kuwa ukiingia ndani ndio unasikia lakini ukitoka nje husikii kitu. Hili Mhe. Naibu Spika, linakera na si kwa maeneo hayo tu, maeneo ya Amani na maeneo ya Mji Mkongwe kila siku yanapigiwa kelele.

Nataka nimuulize Mhe. Waziri kama suala hili analijua kwa sababu wananchi wa Amani wao wenyewe binafsi wanasema wameshapeleka malalamiko yao katika maeneo tofauti ikiwemo Wizara yake, ikiwemo Ofisi za Chama cha Mapinduzi, ikiwemo kwenye Ofisi za Shehia; mote wameshapeleka lakini bado hawajapata ufumbuzi wa matatizo haya.

Kwa hiyo, nina imani sheria hii kupitishwa kwake tutaipitisha hii sheria lakini naomba nitakuwa nina imani kubwa sheria hii itakapopita wawaondolee balaa hili wenzetu hawa wa eneo hili, na kwa sababu mbali na hayo pia wanahofu ya vijana wao kupoteza maadili zaidi na zaidi kuliko walivyo sasa, kwa sababu watoto wadogo wanakimbia na wao wanakwenda katika maeneo hayo. Hapa Mhe. Makame Mshimba alizungumzia kwamba na yeye ameshaenda kuna Entebbe huku, watu wameshahamia mbali na mji lakini mambo yalioko waliokwenda ndio wameshawahi kuyaona. Mimi sijaenda Mwenyezi Mungu anijaalie nisiende huko.

Sasa hapa Amani na eneo la Mji Mkongwe haya mabaa mengine na hizi ngoma zinapigwa kati kati ya mji, sasa kati kati ya mji si kweli mtoto pengine atatoroka lakini huko mbali tuseme atafuata mwenyewe, lakini kati kati ya mji mtoto atakwenda na hata kama hakwenda atasikia na kusikia nako pia kunashawishi, kwa hiyo naomba sana Mhe. Waziri katika hili kwanza hapa uwaonee huruma hawa wananchi ambao wameshaleta malalamiko yao kwa muda mrefu kama unalikumbuka, kama hulikumbuki hilo lipo na maeneo mengine pia iwe ni funzo kwa watu hao wanaofanya hivyo.

Kwa sababu hawa wamiliki wa haya mabaa na wao pia kwa sababu wanajifanya hii sheria kama yao wenyewe, kuna wamiliki pia wametajwa na nawafahamu kwa majina yao katika suala hilo kuna mmiliki mmoja kuna jina la baa inaitwa Volantia mmiliki wake ni mama Frank, na huyo naye ni hivyo anapiga ngoma kuanzia saa mbili mpaka saa nane kwa sauti kubwa, watu hawapati kulala, watu hawali, imekuwa ni balaa kubwa Mhe. Naibu Spika, na jina jengine la baa inaitwa Baa Garage mmiliki ni Owiso Father Mchange ndio mmiliki wa baa hiyo.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri hili lisimamie uwaonee huruma hawa watu, kwa sababu tumetunga sheria hii kwa sababu ya kuondosha utamaduni mbovu uliomo ndani ya nchi yetu ambayo huko nyuma tulikuwa ni wa kupigiwa mfano. Sasa tukiliondosha hili na tukiliweza Zanzibar yetu itarudi kama ilivyokuwa zamani.

Mhe. Naibu Spika, jambo lolote lile ni kujiamini nchi yetu ni nchi ya heshima, viongozi wetu ni wasikivu tunatunga sheria nyingi lakini utekelezaji wa sheria unatupiga chenga. Hapa alipokuwepo Marehemu Mzee Karume palikuwa na sheria, hawa wenzetu wazungu hawa watu kutoka nchi za nje wakifika Uwanja wa ndege walikuwa wakivalishwa kanga, sisi tukienda kwenye nchi za wenzetu tunafuata sheria lakini wao wakija hapa kwetu hawafuati sheria. Lakini sio wao ni sisi wamiliki wa hii nchi yetu. kwa hivyo, kama sisi tutakuwa tayari tutawaelekeza jamani hapa kwenye nchi yetu utamaduni wetu uko hivi tusihofie kama wataondoka, kwa sababu hasara tunayoipata ni kubwa kuliko faida.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Naibu Spika, wizara hii ilisimamie hili kwa nguvu moja tuondokane na balaa kubwa tulilokuwa nalo kuja kuangamizwa ndani ya nchi hii kisiwa chenyewe ni kidogo, lakini mambo yanayofanyika ni makubwa watoto wetu wote wameshaharibika na waliobakia wanaendelea kuharibika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nitaunga mkono baada ya Mhe. Waziri kunieleza au hatua atakayochukua baada ya kusikia malalamiko ya watu hawa wananchi wa Amani nakushukuru Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa nakushukuru Waheshimiwa nimebakiwa na wachangiaji sita. Wa kwanza ni Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Panya Ali Abdallah, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Saleh Nassor Juma. Tunaomba tuje mapema jioni tuchangie.

Baada ya hayo naahirisha kikao chetu hadi saa 11 jioni.

(Saa 5:55 Mchana Kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Sasa nafasi tunampa Mhe. Raya Suleiman Hamad na baadae ajitayarishe Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kutujaalia kwenda na kurudi na ikawa sote tupo salama tukaweza kushiriki katika kazi zetu za kila siku zinazotuhusu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza ninamshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kutuletea huu Mswada, tukawa na hii sheria ambayo itafuta sheria hizi kongwe na tukaweza kupata sheria mpya ili kuweza kuitumia katika malengo na mafanikio ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuwa na sheria, sheria tunazo nyingi lakini ule utekelezaji wa sheria kutekelezeka ndiyo ngumu, lakini sheria tunazo wala siyo mbaya lakini lazima kuwa utekelezaji ndiyo uliokuwa unatupa vikwazo.

Mhe. Naibu Spika, katika Mswada huu ni Mswada wa Sheria ya Kufuta za Utamaduni hizi zilizopita 1983 na kuifuta hii ya Na.1 ya 2009. Kwanza kulikuwa na Bodi, hapa niwapongeze wale watu wa Bodi waliweza ile Bodi ya Sensa kidogo kuweza kupunguza lile wimbi tulilokuwa nalo la mambo kuonekana hadharani. Nyimbo zisizokuwa na maana, filamu zilizokuwa hazikuonesheka pia wale mimi ninawapongeza walijitahidi kiasi chao inavyowezekana. Na leo tunatunga sheria hii Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakapopitisha na *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu itapita, basi sheria hii iweze kuchukua mkondo wake kwa kutekeleza yale yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, tukija katika utamaduni wa Mzanzibari. Wazanzibari wote mila zetu, hulka, silka zote tunazijua na utamaduni tulionao. Isipokuwa watoto wetu Mhe. Naibu Spika, ndiyo wameingiwa na wimbi la wigo kuweza zile tamaduni za hapa petu wakawa wao hawawezi kuzifuata. Mfano kama kivazi watoto wanawake na watoto wanaume, hawa wanafuata mila za wenzetu katika utandawazi wanaouona.

Mhe. Naibu Spika, zile nguo za zamani zilizokuwepo zikapigwa vita vikakatazwa, sasa zinarudia tena. Ninaziona suruali mfano ni zile suruali zilizokuwa zikiitwa chupa, wanazigeuza majina wanaziita modo lakini ni ile ile haina tofauti. Sasa tunaomba tutakapotunga sheria yetu hii na ikapita basi tuweze kuzikanya nguo kama hizi, zikishonwa nchini mwetu au zikija ikiwa ni za mitumba pia tusiziruhusu kuingia, kwa sababu watoto wetu wigo ndiyo unaowaletea wakaingia katika wimbi lililokuwa siyo lao.

Mhe. Naibu Spika, kwenye Mswada kuna Baraza la Sanaa la Wilaya. Katika Baraza la Sanaa la Wilaya na watu wake hapa wamewekwa watakuwa na majukumu hayo, watakaoteuliwa ni Mkuu wa Wilaya, muna wajumbe walio hapa na wajumbe hawa siyo kidogo, lakini tunaomba katika hawa wajumbe uwepo uwiano ijapokuwa umewekwa, lakini sasa katika uwiano wa wanawake pengine katika Mabaraza wanaweza likatungwa Baraza lile la Wilaya ukaja ukashuhudika mwanamke ni mmoja ikawa zote nafasi wakapewa watu wengine zilizotajwa hapa. Hapa pana watu wengi waliotajwa na sifa zao na vyeo vyao wote watakaoingia katika Baraza hili la Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, tukija vibali vitakavyotolewa au leseni. Mimi naona wale watakaopewa vibali hivi au wakapewa hizi leseni kujisajili, kwanza watizamwe wanafanya mambo gani ndiyo waweze kupewa kile kibali au leseni ajulikane leseni hii ni ya kitu gani aweze kukaguliwa, kama mfano tunavyochukua leseni za maduka. Pengine anaweza akachukua kibali hichi au leseni hii akaja pale akasema nina utamaduni fulani, lakini akifika kule akaenda akafanya yeye yale anayoyataka pengine akatuletea mambo yaliyokuwa hayastahiki kuyaleta kwa nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, halafu ni hivi vitu vyetu vinavyotuonesha vilivyokuwa ni vya utandawazi. Mfano, televisheni, haya ma-*videos*, picha zilizokuwa zinaoneshwa. Mhe. Naibu Spika, tutakapoupitisha Mswada huu waweze kuwa na nguvu nzito kuweza kuvizuia vitu kama hivi, kwa sababu ni maonesho ambayo hayastahiki kuoneshwa kwa jamii. Kama hizi zinazoambiwa ni picha za ngono watu wanazo hizi, kwa sababu zimezuiwa lakini watu watakuwa wanazo na wanaonesha majumbani mwao na pengine wimbi kubwa linalotizama mambo yale ni watoto.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba atakayekutwa nazo kuziuza, kusambaza au kuzipokea tu akawa akakamatwa nazo basi sheria hii iweze kumdhibiti na sheria kuchukua mkono wake. Watoto wetu wamepoteza maadili yao ya hulka za Mzanzibari kwa kufuata wimbi lililokuwa siyo letu.

Mhe. Naibu Spika, watoto wote sasa hivi kuna mchezo tu anaouonesha yule anayeitwa Kitale, watoto wote wanakuwa Vitale sasa hivi, kila mtoto anamuiga yule. Ule ni utandawazi, yule ana utamaduni wake lakini na watoto wote wameingia katika wimbi lile la kuiga kwa kuona.

Mhe. Naibu Spika, watoto wa zamani tulikuwa hatuoni, ndiyo ikawa tulikuwa ile hulka inayotakikana katika nchi yetu na yale tunayofunzwa na wazee wetu yakakaa katika nyoyo zetu na tukawa watoto wema mpaka tukafika muda huu. Watoto sasa utandawazi unakuwa mkubwa na wanaiga yale wanayoyaona yaliyokuwa hayastahiki kuonekana.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri tutakapoupitisha Mswada huu tuwe bega kwa bega, wazee, wazazi kuweza kumsaidia Waziri kutekelezeka sheria hii kwa wale watoto wetu wa vizazi vya sasa na vijavyo. Kwa sababu tuna lawama kubwa kuzipeleka Serikalini, lakini je, tujiangalie Rais wa nyumba ni nani, ni baba, Waziri Kiongozi wa ndani ni mama. Je, nyumba zetu tunaweza kuzihudumia, tunaweza watoto wetu kuwarudisha hatuwaogopi. Maana ikiwa mtoto tutamuogopa kwa yale yaliyokuwa hayastahiki basi tusiitupie lawama Serikali, Serikali haitokuja mpaka ndani kuweza kutufundishia, yeye atangojea barabarani mtoto amefanya kosa, ameonekana na kitu hakistahiki akamatwe, utaambiwa tu mtoto kapelekwa Polisi, lakini yanaanzia majumbani mwetu, sisi wazee ndiyo tuliyokuwa na jukumu kubwa la kuweza kufundisha watoto hawa ili kuweza kufuata maadili yetu.

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano mdogo. Zamani ilikuwa akija mposhi basi hapokewi tu mposhi yule mpaka atatolewa kinara kwenda kutizama kule kwao. Je, huko kwao kunaendeka, wana tabia nzuri? Hulka zao ni njema? Ndiyo halafu mume yule anapokewa kuja kupewa yule binti. Sasa mtoto anakuja kukwambia mchumba wangu ni huyu. Humjui anakotoka wala humjui hulka yake, hulka mila yake na desturi na wewe huwezi kumkataa lazima unamfuata mtoto kumpa. Siku ya pili mtoto yule anarudi amepigwa, analala nje, anakomelewa nyumba, hii ndiyo halisi. Kwa hivyo tufuate utamaduni wetu ili kuweza kupata tabia njema na nchi yetu iweze kuokoka na janga hili la maafa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa katika kazi za Bodi na hii Bodi hapa wenyewe. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri kwa kuweza kuunda Bodi hii na kazi zao zikawekwa hapa zikaainishwa, lakini tu huu muda uliowekwa wa kwamba awe na sifa ya hii miaka, kila siku hii miaka tunaililia na sehemu nyingi tukipewa Miswada au vitu vyengine mpaka Mswada uliopita juzi, ilikuwa ya huu miaka saba.

Mhe. Naibu Spika, miaka saba kwa kweli ni mingi. Tunaomba itakapopangwa kama hizi kazi na sifa zitakazowekwa na mtu yule akawa sifa hizi anazo, basi angalau ishushwe kidogo hii miaka, ikiwa mitano pia siyo vibaya kuliko kuwa kila siku tutaweka miaka, awe na miaka kumi na tano, mtu huyo tena hata akifika miaka kumi na tano akipata sifa hizi, hata akija kuajiriwa anafika miaka pengine minne mitano keshamaliza muda wake hajapata kutumia vizuri katika ile kazi iliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, halafu naomba ya kuwa elimu nayo inatakikana kwa sababu ukitoa elimu katika kile kitu utakachokifanya Waziri aweze kutangaza, maana kutoa elimu ili kuwaelimisha watu utakapopita huu Mswada wetu na hii sheria waweze kujifahamu kuwa kuna sheria yetu ishapita, na sheria inataka itekelezeke kwa jambo hili na hili, na hili litakalofanyika ikiwa lisilo hili mtu ataingia hatiani, ataingia makosani kwa hichi atakachokifanya.

Mhe. Naibu Spika, haya majumba ya starehe au majumba tuseme ya kupigia ngoma, hayo yatakayosajiliwa kuweza kufanyia kazi zao. Majumba haya ni udhia kwa sababu haya majumba saa nyengine yapo kati kati ya vijiji, watu hupata shida katika nyumba hizi. Watu wakiingia mule pengine wataelewa, watapigana, ngoma zinapigwa hazina kiasi, watoto watashawishika wataingia mule na watoto wetu mpaka kukimbia majumbani kuweza kufuata hivi vishawishi.

Tunao watoto wanakimbia majumbani kufuata vishawishi lakini tutakapopiga nguvu zetu zote katika kuyapiga vita haya, huenda pengine Mwenyezi Mungu akatujaalia tukawa na busara tukaweza kufanikiwa na kuwe na muda wa vibali vyao hawa watakavyopewa. Wewe unakwenda kuweka muziki lakini muda wako ni muda kadhaa unaanza saa kadhaa uwe umeshavunjika muziki wako, ngoma iwe haipo tena, michezo yake yote ianzie ikiwa itaanzia saa

tatu, lakini ikifika kama tano, sita basi waweze kuvunja isiwe tena ni mtogoo na mtogoo wakaweza kutuwekea mashaka yale yaliyokuwa yanatupa udhia.

Mhe. Naibu Spika, katika Mswada huu vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi yake kubwa. Kwanza nataka nijue huyu Mkuu wa Wilaya, maana yake hapa Baraza la Wilaya, Mkuu wa Wilaya ndiye atakayeliteua hili Baraza na wakawa hawa wajumbe aliowaweka; pana mjumbe wa Sheha, pana na wajumbe wengine kama mjumbe wa wanawake na mwanasheria.

Mhe. Naibu Spika, hawa tunataka tujue watatoka kwa fani na watatokea wapi au watatokea katika zile zile Wilaya zao wanazotoka au watachaguliwa tu watu waliokuwa na sifa zile kuingia hapa kwa hizi sifa zilizotajwa, vile vile aje atueleze Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, halafu utamaduni wa Mzanzibari ni kivazi. Tunapopita popote sisi tunajulikana kuwa watu hawa wanatoka Zanzibar kwa ajili ya kivazi chetu. Ikiwa ni wanawake vivazi vyetu vinajulikana, tunavaa nguo vizuri kujitanda na mambo mengine. Mhe. Naibu Spika, tunaomba Mswada huu ukipita wale watakaokutwa wanabadilisha kivazi mfano wakavaa nguo zilizokuwa kwapa nje, nguo zikawa fupi, hawajitandi basi vile vile na wao wachukuliwe hatua, kwa sababu ikiwa ni mtu mzima anayafanya yale basi na mtoto aliye chini yake anaona yale ndiyo mazuri na anayafuata.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu mimi nilikuwa nikisema sheria hii ikiwepo mpaka wale machangudoa, tusiwaachie. Yale machangudoa, Mawaziri mara moja walitwambia Waziri wetu mmoja hapa alitaka kutekwa na hao machangudoa. Mhe. Naibu Spika, tusiwaachie, tukiwakuta tu njiani kama alivyofanya mara moja tulipokuwa tunatoka Kikwajuni Waziri Kiongozi, tunatoka pale madudu yapo pale hayana nguo, akatoa ruhusa wakamateni hao na wakakamatwa. Watoto wale walipofika pale kumbe pengine wanaaga kwao nakwenda kwa rafiki yangu, lakini walikuja kuvua nguo pale karibu ya Baraza la Wawakilishi na wakakamatwa.

Tunaomba huu Mswada uchukue sheria hii na hawa wakikutwa watupa wimbi baya basi na wao waweze kukamatwa na kuweza kupewa adhabu kali iwezekanavyo waweze kukoma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, halafu katika Mswada huu vile vile kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kuweza kutuletea Mswada huu kwa Baraza na Baraza hili Mwenyezi Mungu alijaalie liwe. Katika Baraza hili sisi tuna wasomi walemavu, usije kusahau kututilia katika Baraza la Wilaya yote yatakayopita, lazima walemavu wamo waliosoma na walio na sifa kama hizi ulizoziweka hapa, utupatie mlemavu kwa kila Baraza awemo mlemavu kwa kila Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi naunga mkono hoja na nakupongeza wewe na ninampongeza Mhe. Waziri na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie Mswada wetu upite kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Raya. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa baadaye ajiandae Mhe. Panya Ali Abdalla na baaadaye Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa jioni hii ya leo kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika Mswada wetu huu unaohusiana na masuala ya Sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho mwaka 2009 kama ambavyo umewasilishwa kwetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na madhumuni kwanza na ninaomba kunukuu baadhi ya vifungu katika haya madhumuni ya Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria Na. 6 ya 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki na Sheria Na.1 ya 2009 ya Bodi ya Sensa na kutunga sheria mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Kusimamia Majukumu ya Kulinda na Kuhifadhi Mila, Silka, Maadili Mema ya Wazanzibari na kuutumia Utamaduni katika kupunguza umaskini kwa jamii.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia malengo hasa ya madhumuni ya Mswada huu ni mambo mazuri sana ambayo yanalenga kuisaidia jamii yetu ya Kizanzibari. Mimi nichukue fursa hii vile vile Mhe. Naibu Spika, kuwapongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake katika Wizara, lakini vile vile na Kamati pamoja na wadau ambao wamekaa kwa pamoja na kuweza kuupitia Mswada huu na hatimaye baada ya marekebisho ambayo wameyaona,

wakaona kwamba Mswada huu sasa watuletee sisi ili na sisi tuweze kutia mawili matatu na hatimaye iweze kuwa sheria ambayo itaweza kutuongoza katika taratibu zetu ambazo tunajiwekea.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele kuna kifungu hapa kinazungumzia suala zima la ghasia zinazosababishwa na ngoma zinazopigwa kwenye makaazi ya watu hadi usiku wa manane na pia kuwashirikisha watoto wa umri usiopaswa kuwemo kwenye ngoma hizo. Kushindwa kulinda silka na maadili kwa kutodhibitiwa maonesho ya sanaa yenye vitendo viovu. Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ambayo yalikuwa yameandikwa hapa lakini tukiangalia kwa utamaduni wetu na silka za Kizanzibari, suala zima la desturi, silka ni suala ambalo linahusu familia zetu ndani ya majumba yetu. Kutokana na wimbi la maendeleo na wimbi kubwa tulilonalo la utandawazi Mhe. Naibu Spika, ndiyo haya yameweza kutufikisha hapa sasa hivi.

Mimi niwashukuru sana ndugu zangu hawa katika Wizara inayohusika kwa kuweza kukaa na kufikiria hili kupitia katika Serikali Kuu na hatimaye wakaweza kuja na Mswada huu ambao tunahisi unaweza ikawa ni kichocheo cha kusaidia maadili mema, desturi, mila, silka na mambo yote yakaweza kwenda vizuri kama vile ambavyo tunatarajia sisi wenyewe. Lakini kazi hii Mhe. Naibu Spika, naomba turejee katika taratibu zetu za kizamani, irudi zaidi katika familia na maeneo ya dini, vile vile ndio hasa maeneo ambayo yanatakiwa kuchukua hatamu katika kuhakikisha kwamba mambo haya yanalindwa, yanaendelezwa na kuhakikisha kwamba vizazi vyetu vinakwenda kwa mujibu wa utaratibu kama ambavyo tumeamrishwa na dini zetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa naomba kidogo niingie katika mswada wetu huu, kwa kuanza na kifungu namba 6 cha mswada huu. Kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, kinazungumzia sifa za Mwenyekiti, pamoja na sifa ambazo zimeorodheshwa hapa, lakini nimekuta kwamba kuna sifa tatu hapa, ambazo zinasema kwamba mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza ikiwa ni Mzanzibari, ana uzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa na ana maadili yanayokubalika katika jamii. Lakini hapa hatujaona sifa ya kiwango cha elimu kwa mtu huyu ambaye atachaguliwa kuwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumezowea kuziona bodi nyengine. Hilo moja.

Jengine kuna sifa ambayo mara zote inakuwepo, sifa ya yule mtu ambaye anachaguliwa kuwa Mwenyekiti, awe hajawahi kuhusishwa na vitendo vyovyote vya makosa ya jinai, hapa hatujaona. Pengine yule mtu ndio utamaduni wake au desturi yake kufanya mambo kama hayo, sasa leo anakuwa kiyoo katika jamii. Sasa naomba na sifa hiyo vile vile tuizingatie katika kuboresha sifa za yule mtu ambaye anapaswa kuwa Mwenyekiti katika eneo hili.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, vile vile nakuja katika kifungu cha 7 ambapo kuna kazi za Baraza, hapa katika kazi za Baraza kifungu kidogo cha (1)(h) kinasema, pamoja na kazi nyengine ambazo zimeanza nyuma huko, kuweka utaratibu mzuri wa kuwatambua, kuwapa tunzo wasanii wa zamani ambao wamechangia maendeleo ya kazi za sanaa Zanzibar. Hili ni jambo jema na ni jambo zuri, lakini tunaomba taasisi inayohusika katika kulifanya hili, tufanye kwa kuweka utaratibu maalum utakaokuwa unazingatia vigezo, pamoja na sifa halisi ambazo zitakuwa zipo kwa mujibu wa taratibu na kikanuni au sheria ambazo mtakuwa mnazipanga ndogo ndogo katika taasisi zenu.

Vile vile, kifungu (i) kuhakikisha kwamba filamu zote zinazo rekodiwa ndani na nje ya Zanzibar zenye lengo la kuoneshwa hadharani zinakaguliwa na Baraza. Mimi hapa Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa tahadhari tu, ziko filamu ambazo zinataka kuoneshwa katika hadhara zinakuja kwa muda mrefu, zinaweza kupita katika taratibu hizi. Zile ambazo zina matukio ya papo kwa papo je, utaratibu wake unakuaje?Mhe. Waziri atakapokuja hapa tutaomba atusaidie zaidi ili tuweze kufahamu kutokana na maendeleo ya dunia kwa sasa, hizi filamu ambazo zitakuwa zinakuja haraka haraka na zikawa zinataka kuwafikia wana jamii.

Nikiondoka hapo nakuja katika kifungu kidogo cha (2), Baraza litafanyakazi zake kwa mujibu wa masharti yaliyotolewa na kanuni na litatoa vibali na leseni zifuatazo. Tumeonesha hapa vibali vya ngoma kutoka namba ya kirumi (i) mpaka (v). Lakini mimi nakuja hapa leseni yoyote nyengine itakayoonekana inafaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa ningependa kutoa tahadhari vile vile, hususan kwa kutilia maanani kipindi kifupi kilichopita nyuma. Siku moja niliwahi kufuatwa na mama mmoja, yeye alikuwa na malalamiko yake juu ya suala zima la hizi ngoma, pamoja na utaratibu wa kufanya mambo ya kupunga, mambo ya kibuki. Sasa huyu mama yeye alikuja katika misingi ya kwamba amekuja kulalamika na alitaka hoja yake iweze kuletwa katika serikali, ili iweze

kutafutiwa ufumbuzi. Yeye anasema hili suala la kupunga vibuki imekuwa siku hizi kama ni biashara, kila pahali inafanyika, kila mtu anafanya.

Sasa huyu mama yeye akaomba kwamba mwingi wanamokwenda kufanyiwa shughuli hizi, inakuwa hazifanywi kwa mujibu wa utaratibu unaopaswa hasa, inakuwa ni masuala ya kunyang'anyana fedha tu na ukitilia maanani suala la upungaji wa kibuki ni kazi ambayo inatia fedha nyingi sana.

Sasa huyu mama yeye akataka kujenga utaratibu utakaosababisha kuangaliwa hawa watu ambao wanafanyakazi hizi, ili watendaji wa kazi hizi waweze kuwa ni watu ambao wana taaluma na kazi hizi na wanafanya kwa lengo la kuwasaidia watu ili waweze kuneemeka na yale matatizo na shida zao walizonazo.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika kifungu cha 8, uwezo wa Baraza. Katika kifungu kidogo cha (1) "Baraza litakuwa na uwezo wa...", kuna mambo yameorodheshwa hapa kutoka (a) mpaka (g). Mimi nataka kuzungumzia zaidi katika Ibara (c), kuzifanyia sensa filamu au kaseti za video yoyote, kama *CD, DVD, HDV* na kitu chengine chochote chenye kuhusiana na hivyo ambavyo vimerekodiwa ndani au nje ya Zanzibar kwa lengo la kuoneshwa hadharani.

Hebu jamani tusaidieni na sisi utaratibu gani utakaoweza kufanyika kuweza kuhimili au kuweza kuli- *control* suala hili, wakati mambo haya yanaruka *24 hours* na watu wanaweza kuoneshana mambo bila hata ya kutegemea, matokezeo yake hata hiyo Kamati ya Sensa itakapokwenda watu tayari wameshamaliza kila kitu. Sasa hebu tusaidieni, kuna utaratibu gani ambao mtakuwa mnaufanya ili kuhakikisha kwamba haya mambo yanamilikiwa kweli kama ambavyo mnazungumza katika sheria hii.

Jengine ambalo ilikuwa natarajia kuwa itakuwa ni katika kifungu (h), ni namna ya kuweza kuwa- *control* wageni wetu wanaokuja katika nchi yetu hususan kwa mavazi yao.

Mhe. Naibu Spika, suala la maadili kama tunakubaliana kwamba maadili haya yatakuwa ndio maadili yanayofuatwa katika nchi. Kuna wageni wengi wanaokuja hususan kupitia katika njia ya Uwanja wa Ndege, mavazi yao wengine hayaendani na maadili yetu. Sasa kwa sababu wizara hii pia inashughulika na masuala ya utalii, sijui Mhe. Waziri wana mpango gani wa kutekeleza, ili kwa wageni ambao watakuwa wanakuja nchini waweze kutengenezewa utaratibu ili waweze kuendana sambamba na maadili ya kimavazi katika nchi yetu, ili wanapotoka katika maeneo ya Viwanja vya Ndege vya nchi yetu, wakiingia ndani waweze kuona kwamba wanakuwa sawa kama walivyo watu ambao wamo ndani wanavyoendelea na shughuli zao.

Tukiondoka hapo tuje katika kifungu cha 11, muda wa Wajumbe wa Baraza. Mhe. Naibu Spika, hapa katika kifungu kidogo cha (2) Mjumbe wa Baraza atasita kuwa mjumbe iwapo atafariki, hatohudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya sababu ya msingi, ametiwa hatiani kwa kosa la kimaadili, amejiuzulu, amekuwa Mjumbe wa Baraza kutokana na nafasi yake na ikiwa amesita kuendelea kufanyakazi katika nafasi hiyo.

Vile vile, ningependa hapa kuongezwe kifungu cha (f) ambacho kitakuwa kinazungumzia suala endapo itabainika kwamba mjumbe yule anahusika na masuala yote ya jinai, kama nilivyokuwa nimezungumza kule mwanzo, ningeomba kipengele hicho kiweze ku-*appear* katika eneo hili.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nakuja katika kifungu cha 24(2), mimi kimenishtusha kidogo na kimenishtusha baada ya kuona kwamba waziri anaweza kupokea na kupitia maamuzi yaliyotolewa na Baraza kwa kufanya yafuatayo.

(i) Kupokea na kupitia maamuzi yaliyofanywa na Baraza na;

(ii) Kutoa maelekezo kwa Baraza njia ya kufanya kukubali au kufanya mabadiliko au kukataa maamuzi yaliyofanywa na Baraza.

Sasa hapa kwenye kirumi (iii), hapa ndio panaponitisha. Nikiangalia hapa na nikiangalia kifungu kidogo cha (3) katika Ibara ya 23 hiki ambacho kinasema kwamba;

Ibara ya 23;

"Uwamuzi wa waziri utakuwa ni uwamuzi wa mwisho"

Mwenzangu aliweza kunukuu kifungu cha 134 cha Katiba pale asubuhi, ambapo kilikuwa kinampa hofu kuona kwamba waziri atakuwa na maamuzi ya mwisho wakati katiba inakataa hivyo. Katiba inakataa hivyo na kama ambavyo sitaki kurudia ambavyo mwenzetu amekwisha kuzungumza mwanzoni. Lakini hofu yangu zaidi inajengeka kuona kwamba kifungu cha 20, 21 na 22, ambapo vifungu hivi vinazungumzia majukumu ya Mrajis na uwezo wa Mrajis.

Nikiangalia katika uteuzi kule kuna Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais, kuna Katibu Mtendaji ambaye anateuliwa na Rais. Lakini huyu Mrajis anateuliwa na waziri. Sasa hapa kidogo napata hofu kuona huyu Mrajis anateuliwa na waziri, lakini nikawa nimefarijika niliposoma kifungu cha 24 vifungu vya mwanzo kule nilikuta kwamba kuna Baraza ambalo litakuwa linam-*control* huyu Mrajis, ambapo kama atakuwa amefanya kitu kinyume na utaratibu basi atakuwa amemilikiwa.

Lakini na Baraza lenyewe sasa linanyang'anywa uwezo wake katika kifungu hiki cha kirumi (iii), kwamba maamuzi ya mwisho yanakuwa ni ya waziri, hata yale mambo ambayo Baraza limesema yatakuwa hayana uzito wowote. Hapa pananipa tabu kidogo, naomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa unisaidie kunielewesha ili ikiwezekana tuweze kwenda sambamba katika hili.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja katika kifungu cha 29. Kifungu hiki ni kama kule mwanzo nilivyochangia (e) kukagua ngoma za asili, muziki, santuri, *CD, DVD* na *HDV* zilizorikodiwa wilayani au nje ya wilaya kabla hayajatumika au kuoneshwa kwa jamii.

Suala hili Mhe. Naibu Spika, mimi bado halijaniingia kwenye akili kwamba yataweza kutendeka haya, kwa sababu *DVD* na mambo mengine ya mitandao yanakuja pasi na ku-*control* katika eneo lolote. Sasa ningeomba nifahamishwe ni utaratibu gani utaweza kutumika ili mambo haya yaweze kudhibitiwa na jamii isiweze kuyafikia.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hicho hicho cha 29(f), nimeona hapa kwamba kusikiliza na kuamua rufaa zitakazowasilishwa dhidi ya maamuzi ya Sheha. Hapa kidogo naomba nipate mafahamisho zaidi. Kusikiliza na kuamua rufaa zitakazowasilishwa dhidi ya maamuzi ya Sheha. Kwa uelewa wangu, Sheha ndio mwenye jamii katika eneo lake. Sasa Sheha ndio anaeweza kuthibitisha kwamba eneo fulani au chombo fulani, au watu fulani wanafanya kitu fulani, na yeye akatoa maamuzi kwa mujibu wa sheria ambazo amewekewa. Lakini sasa na huyo Sheha na yeye hukumu zake zinakuja kusikilizwa na Baraza, Baraza ambalo baadaye linaweza likapingwa maamuzi yake na Mhe. Waziri. Hapa kidogo ningetaka kuja kufafanuliwa na niweze kupewa tafsiri ambayo na mimi nitaweza kuielewa.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nakuja katika kifungu cha 23 sasa. Kifungu hiki kinasema,

Kifungu 23;

> "Mkaguzi wa utamaduni wa wilaya atakuwa na uwezo ufuatao, Kuingilia kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote katika eneo lolote au nyumba ya maoneshao anayohisi shughuli za utamaduni zinafanyika"

Kipangele hiki naomba kirekebishwe na kiongezwe maneno kwa mujibu wa sheria hii. Kwa sababu huyu mkaguzi atakapokuwa na uwezo wa kuweza kuingia pahala popote, wakati wowote bila ya mipaka maalum, hapa usalama unaweza ukawa uko hatarini kwa watu wengine. Naomba eneo hili lifanyiwe marekebisho na liwekewe *limitation* kwa hawa watu ambao watakuwa wanafanya, na angalau basi iwe kwa mujibu wa sheria hii, isiwe iko wazi kama hivi ilivyo, kwa sababu hii ni sheria ambayo tunaitengeneza.

Tukiondoka hapo sasa Mhe. Naibu Spika, ninakuja katika kifungu hicho hicho cha 33(2), hapa pana marekebisho kidogo katika sentensi inayosema, "mtu yeyote atakayemzuwia au atakayemuwekea kikwazo Afisa wa Utamaduni, hili neno "aliyeteuliwa" naomba lifanyiwe marekebisho na liwekwe sawa, kuliko kama hivi sasa lilivyo. Naomba lisomeke kwammba aliyeteuliwa, lakini hivi lilivyo sasa halitutoshelezi kutoa tafsiri sahihi au kueleweka vizuri zaidi.

Jengine katika sentensi hiyo hiyo hapa nimeona kuna aliyeteuliwa na Baraza, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyozidi, naomba hapa tutengeneze lugha kidogo itakayokuwa tamu zaidi, iwe kuna

option hapa, isiyozidi na sio chini. Naomba utaratibu huo tuutumie kama ambavyo tunatumia katika sheria nyengine ambazo huwa tuna kawaida ya kuzipitisha hapa, tusiende katika isiyozidi, hapana, yawepo maneno mengine mbadala vile vile kama ilivyo katika miswada mingine ambayo tunakuwa tunaipitisha.

Mhe. Naibu Spika, tukija katika kifungu cha 34, utoaji wa kibali. Sheha atakuwa na jukumu la kutoa vibali kwa ajili ya shughuli zote zinazohusiana na upigaji ngoma, maonesho ya sanaa na maonesho ya jukwaani ya burudani yatakayofanyika katika Shehia yake. "Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kibali kitatolewa kuzingatia masharti yafuatayo; muda wa kuanza na kumalizika kwa shughuli, pahala amabapo shughuli itafanyika na malipo yanayopaswa kutolewa".

Hapa napongeza, lakini sio ngoma zote ambazo zinapaswa kulipwa. Naomba hapa Mhe. Waziri atakapokuja aweza kutupa ufafanuzi kidogo, atufahamishe kwamba sio ngoma zote zinazoweza kuingiliana na masuala haya, zipo ngoma ambazo zinakuwa hazina malipo na wewe kwa sababu ni Mhe. Waziri wa mambo ya sanaa, utamaduni na michezo bila shaka maeneo hayo utakuwa unayafahamu kama vila ambavyo baadhi ya nyakati huwa unanifahamisha mimi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele nakuja katika kifungu cha 47, picha za ngono za watoto. Hapa nitarudia kule mwanzo ambapo nilikwisha kuchangia;

> "Mtu yeyote atakayetengeneza au kushiriki katika kutengeneza, kusafirisha, kuchapisha, kutangaza, kuuza, kuingiza nchini, kutoa nje ya nchi, au kusaidia kwa njia yoyote upatikanaji wa picha za ngono zinazodhalilisha watoto, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini ya shilingi milioni 2,000,000/- za Kitanzania, au kifungo cha miaka miwili, au adhabu zote mbili kwa wakati mmoja".

Hapa Mhe. Waziri naomba unisaidie utaratibu na namna ambavyo mnatarajia kufanya ili kuweza kulikubali hili, kwa sababu kwa utaratibu tuliokuwanao sasa, hili mimi nahisi haliwezekani. Kwa sababu hapa nilipo nitakapoingia kwenye mitandao tu basi nitapata mambo ya kimaajabu ajabu, sasa unaposema kwamba mtu ataweza kuingia kwenye adhabu wakati mambo anayapata mwenyewe yuko nyumbani kwake, si itakuwa tunazungumza vitu ambavyo haviwezekani, hebu tusaidie tuweze kuona namna gani tutaweza kwenda sambamba katika hili.

Mwisho katika kifungu cha 52(2), hapa vile vile inarudi sentensi ile katika masuala ya faini, faini isiyozidi shilingi milioni moja, iweko mbadala yaani si chini ya kima fulani na si zaidi ya kima fulani isiwe kwamba tunatembea humu tu hapa tutakuwa tunawapa uhuru mkubwa Mahakimu wetu hata wakimtoza shilingi mia inakuwa imetosha, kwa sababu haikuzidi kile kiwango kilichokuwa kimezungumzwa kule. Sasa tunataka tupewe ufafanuzi hapa ili isiwe chini ya kima fulani na isizidi kima fulani.

Mhe. Naibu Spika, nikifunga mswada wangu sasa nakuja katika mchango wa jumla. Bado tuna matatizo katika suala zima la kutoa kipaumbele kwa sanaa kama ambavyo ilikuwa sheria yetu inavyozungumza hapa. Tuna mambo mengi yanahusiana na sanaa ambayo muendelezo wake sidhani kama utaweza kutatuka kwa sababu ya kupitisha sheria hii.

Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunavyozungumza tunayo nyumba ya sanaa ambayo iko katika maeneo ya Mwanakwerekwe hapo; nyumba ile naweza kusema kwamba sasa hivi imekuwa kama labda niseme jalala kwa maana haiulizwi mbuka wala taire, wala haishughulikiwi ikaweza kuleta faida kwa maslahi ya vizazi vyetu vilivyomo katika nchi yetu.

Hapo hapo tumekwenda katika kutengeneza sheria ya kuweza kutengeneza masuala hayo wakati ile *station* yenyewe ina mushkeli na ina matatizo, ningelimuomba sana Mhe. Waziri kwanza aangalie uhalisia wa jengo lake la sanaa lililokuwepo pale Mwanakwerekwe na liweze kulingana na kazi ambayo tayari tunatarajia kwenda kuifanya, ili iweze kuleta matumaini mazuri na kuhakikisha kwamba wenzetu hawa ambao tunawatengenezea hii sheria wanapata na maeneo ya kwenda kuzungumzia, au kwenda kusimamia masuala yao yanayohusiana na sanaa.

Vile vile, ningelipenda hapa kuzungumzia suala zima la wasanii wetu Mhe. Naibu Spika, wasanii wetu ambao wapo hapa wanajitahidi kujishughulisha katika mambo ya sanaa mbali mbali, hawafaidiki na kazi yao hii ya sanaa, mara nyingi na mara zote wamekuwa wakipata na wanachopewa sio kupata kile ambacho wanachokitaka, tunakusudia kusema kwamba sanaa kwa sasa tunatarajia kwamba iwe ajira kwa vijana wetu basi ni vizuri tukatengeneza utaratibu ulio makini ambao unaweza kuwasaidia vijana wetu, kile ambacho wanachokitaka kwa mujibu wa sanaa

zao wanazozitengeneza, ndicho ambacho wanachokipata. Sio kama sasa hivi ambapo wanapewa kile ambacho kilichopo, sio kwa mujibu wa uwezo wa kazi ambayo waliyokuwa wanaifanya.

Vile vile Mhe. Waziri atakapokuja hapa naomba tuwasaidie hawa wenzetu katika taasisi ya hati miliki kwa jina jengine wanaitwa KOSOZA, pamoja na mambo haya tunayoyafanya tuwape mamlaka na madaraka ya kufanya kazi zao KOSOZA, ili waweze kuendana na haja halisi ya kutengeneza sheria hizi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelekezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia 85 na asilimia kumi na tano nasubiri Mhe. Waziri anitosheleze kwa majibu ambayo yataweza kuwasaidia watu wengine ambao tunazungumza kwa niaba yao, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya watu wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono kwa asilimia hiyo, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii ili niweze kuchangia Mswada huu angalau kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri ambaye yeye pamoja na watendaji wake wameweza kuandaa Mswaada huu mzuri na kutuletea wajumbe ili turekebishe na baadae tuupitishe. Pia nitoe shukurani za pekee kwa Mhe. Waziri kwa jinsi ya utaratibu alioutengeneza kwa mswada huu, yaani Mswada huu mara hii unaonekana umetengenezwa vizuri kitaalam na kisheria zaidi, kwa hivyo napenda kutoa shukurani hizo na niseme niombe kwa Waheshimiwa wengine basi kufuata utaratibu huu uliotumiwa katika kutungwa Miswada, kwa sababu unaonekana uko vizuri na unaeleweka vizuri. Mhe. Naibu Spika, kuiga jambo zuri sio vibaya, vibaya kuiga jambo baya.

Mhe. Naibu Spika, niseme mila na desturi zetu zinaondoka kwa kasi kubwa kwa sababu ya kuiga tamaduni za nje ambazo jambo hili sio zuri kwetu, tunatakiwa kudumu na mila zetu na tamaduni zetu jambo ambalo linawavutia sana wenzetu; wageni mbali mbali tunapata katika nchi yetu kwa ajili ya kupendezewa na mila, silka na tamaduni zetu. Jambo ambalo linaleta sifa katika nchi yetu kwa sababu nchi ambayo haina utamadui inakuwa ina kasoro, kwa hivyo jambo hili linaitangaza nchi yetu na pia inakuwe ni utambulisho wetu popote tunapoonekana, maana yake tunajulikana.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tuendeleze mila na desturi za nchi yetu ambazo zinapelekea kupata utambulisho mzuri na sifa nzuri ya nchi yetu. Pia, nimuombe Mhe. Waziri ambeye ametuletea sheria hii, atuletee na ile sheria inayohusu mavazi ili iendane na sheria hii, kwa sababu sheria hii inaonekana mambo mengi humu tayari yamekatazwa, lakini iwapo sheria ile itakuwa haijaletwa basi itakuwa inatoa mwanya kwa mambo mengine kuweza kufanyika.

Mhe. Naibu Spika, sasa na mimi niingie katika Mswada huu ili niweze kuchangia machache. Kwanza kabisa nataka nichangie sehemu hii ya pili ya uanzishwaji wa Baraza la Sanaa na Sensa ya filamu na utamaduini.

Kifungu cha 5(i) ambacho kinaeleza kuna Wawakilishi wawili kutoka katika Jumuiya za Kidini. Mhe. Naibu Spika, mimi wajumbe hawa nimewaona hapa tu, sasa sijui nikiangalia katika Mswada sikuona labda wao kama wana sanaa au tamaduni zozote zinazohusiana na dini zimo katika Mswada huu. Kwa hivyo Mhe. Waziri, utakapokuja unieleze kama hawa Wajumbe wamewekwa kwa ajili gani, maana yake ukiwaweka na wao wawe wana sehemu ya kuwakilisha kitu katika Mswada huu... Sasa mimi humu nimejaribu kutizama tizama sijaona, pengine sijaangalia vizuri utakapokuja utanielewesha, kwa sababu naona mambo ya kidini nayo yapo, yenye Tamaduni za kidini ingefaa nayo yangepewa kipaumbele yakawekwa.

Nikenda katika kifungu cha 6 kinaeleza mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza ikiwa..., mimi nilikuwa naomba nifanye marekebisho kidogo hapa niseme "mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza akiwa na sifa zifuatazo" halafu ndio ije awe Mzanzibari.

Halafu na (b) hapa inaonekana kuwa ana uzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa, mimi nasema awe na uzoefu katika mambo yanayohusiana na sanaa, lakini pia hapa mambo yanayohusiana na Sanaa Mhe. Naibu Spika, hayakutajwa uzoefu huu kwa muda gani na tumezoea sheria nyingi zinasema awe na uzoefu usiopungua miaka mingapi, lakini hapa naona haikuwekwa.

Pia, kifungu cha (c) kuna ana maadili yanayokubalika, maana yake tukisema ana tayari huyo mtu yupo ameshateuliwa, lakini awe maana yake ndio tunatarajia ndio kuja kumteua, kwa hivyo nilikuwa naomba marekebishi hayo.

Halkadhalika, nikija katika kifungu cha saba katika kazi hizi za baraza Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namshauri Mhe. Waziri kuongeza kama ataona inafaa kuongeza vifungu hivi ambavyo nitavisoma. Katika kazi hizi zimetajwa kazi nyingi lakini mimi nilikuwa nataka niongeze kwa kusema kifungu hicho kuhakikisha tunakuwa na sanaa na utamaduni usioipotosha jamii, hicho kimoja.

Chengine kuwa na mpango endelevu wa kutoa elimu ya sanaa na utamaduni utakaoipatia jamii maendeleo, halafu chengine kwa sababu ndani ya Tamaduni na mila huwa kuna mila nyengine potofu hazifai kwa jamii, pia ningesema kuzuia mila zote zenye kuleta madhara kwa jamii; mila ambazo zitaleta madhara kwa jamii basi hizo tukaweza kuzizuia kupitia sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika kifungu cha 2 ambacho kinasema kuthibitisha maombi kwa vikundi vya sanaa kutoka nje ya Zanzibar vinavyotaka kufanya shughuli zao Zanzibar; hapa nilikuwa nataka kuuliza hivi vikundi vinavyotoka nje je, vitaweza kuzingatia mila na silka zetu? hawatokwenda kinyume wao kwa sababu wasije wakawa wanakuja kufanya hapa, lakini kunakuja wageni wao tunawaachia wanaendelea kupotosha mila zetu.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika kifungu cha 22(b), hapa kuna kutofautisha majina katika fomu maalum ambayo atasajili vikundi vya sanaa na utamaduni. Hapa mimi nilikuwa naomba Mhe. Waziri ukija unifafanulie kwa sababu sijapafahamu vizuri.

Pia, katika kifungu cha 21(c) kunatakiwa hapa Mrajis huyu awe na uzoefu usiopungua miaka saba; mimi kwa ushauri wangu nilikuwa naomba labda tuipunguze iwe mitano.

Halafu nikija katika kifungu cha 24 kwenye rufaa mtu yeyote ambaye hakuridhishwa na maamuzi ya Baraza anaweza kukata rufaa kwa Waziri, lakini wengine wanaweza wakaona Waziri labda hatowasaidia, ningesema au Mahakama, yaani mtu kama hajaridhika kwa Waziri basi aweze kuitumia Mahakama kwa kupata analolikusudia.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu cha 29(e) hapa kifungu hiki kinasema kukagua ngoma za asili, muziki, santuri, *CD, DVD* na *HDV* zilizorikodiwa wilayani au nje ya wilaya kabla hayajatumika au kuoneshwa kwa jamii. Hiki ni kifungu kizuri lakini hapa panahitaji umakini na umakini wenyewe unaweza kukaangaliwa hizi *CD* na matokeo yake ukaja ukaona tunaoneshwa michezo ambayo haistahiki, kwa sababu imeshawahi kutokea hapo nyuma na baadae mnakuja kuulizana kwani hili halikupita katika Baraza hili la sanaa.

Kwa hivyo, hapa watu wawe makini, watu wanaweza wakazipitia *CD* lakini tuone sasa je, huyu ambae atakuwa *CD* ameshazipitisha washaziangalia na washazipitisha, je, inapokuja kutokea kosa la kuonekana picha zile ambazo hazitofaa yeye atakuwa anachukuliwa hatua gani? Kwa sababu tusije tukamchukulia yule tu anayechapisha lakini na huyu nae analo kosa la kuona katumia kupitisha hiki kitu na ambacho hakitastahiki.

Hapo nyuma nakumbuka kulikuwa na wimbo ule kulipokuwa na bodi ya sanaa ulikuja ukaimbwa "...ingawa haramu malipo yake moto lakini msaidie mwenzako", haukusitishwa mpaka ulikwenda ukaimbwa. Kwa hivyo, inaonekana kwenye bodi ya sanaa ulipita lakini matokeo yake ikaja ikatoka nyimbo ile hilo linakuwa ni kosa, kitu kipite ikionekana hakifai kistopishwe huku huku.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye kifungu cha 34(ii) kinachosema mahala ambapo shughuli itakapofanyika, Mhe. Naibu Spika, mahala hapa napo ni muhimu kwa sababu ndio yale yanayotokea kufanyika yaani vibali hivi vinatolewa halafu kunafanyika sehemu ambazo hazistahiki ikiwemo katika mitaa, ambapo haifai huko kupiga magoma na kuwaudhi watu usiku wa manane. Lakini pia katika sehemu za ibada, tuangalie huyo anayechukua kibali hatokwenda kupiga karibu ya au chini ya msikiti akawaudhi waumini wanaotaka kuswali pale? Lakini pia maskuli, kwa sababu Kiwengwa mimi nilikwenda mara moja na tulipiga kelele Mwenyezi Mungu akajaalia likaondoka, palikuwa panapigwa mziki karibu sana na skuli hali ambayo iliwafanya wanafunzi kupata shida sana ya kusoma, kumsikiliza mwalimu, wakawa wanasikiliza nyimbo ambazo zinapigwa nje. Kwa hivyo vitu hivi ni muhimu kuviangalia, ni wapi ambapo huyu muhusika aliyechukua kibali atakwenda kufanyia shughuli zake hizi.

Mhe. Naibu Spika, pia niende katika kifungu cha 39(b) ambacho kifungu hichi kinaeleza "itakuwa ni halali wakati wowote Afisa wa Utamaduni au Mjumbe wa Baraza kusimamisha au kutoa maelekezo mengine yoyote atakayoona yanafaa kwa ajili ya usalama wa nyumba ya maonesho, au watu wanaohudhuria kwenye maonesho haya". Kifungu hiki pia nakipongeza, mumekiweka kiko vizuri, lakini pia msisitizo wangu kuona huyo ambaye anakwenda kukagua basi akiona kama jambo hili halifai, maana yake aweze kusema kama mahala hapa kwa usalama wa watu patakuwa hapafai, kuonesha yaani pengine sehemu ndogo watu wataingia wengi, watakwenda kubanana na kutokea madhara mengine. Ili hiki kifungu kije kionekane kinafanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia niende katika kifungu cha 41(1) ambacho kinasema Baraza, mkaguzi wa utamaduni, polisi au afisa yeyote aliyeruhusiwa na Baraza anaweza kuingia katika nyumba ya maonesho wakati wowote kwa lengo la kuhakikisha masharti ya leseni yamezingatiwa kwa mujibu wa sheria hii". Kifungu hiki nacho kipo vizuri napenda nitoe msisitizo tu kwamba tayari tuwe makini kwa huyu mkaguzi anapokwenda kukagua, maana yake mtu anaweza kwenda kukagua na akaona pana hitilafu lakini akaja akaghilibiwa, pengine kwa kupewa pesa akaambiwa bwana nisaidie niweze kupitisha shughuli yangu hii. Lazima aangalie iwapo itakuwa hali hii hairidhishi basi asije akaghilibika kwa pesa, badala yake aweze kusimamia utaratibu mzuri ambao utaweza kuleta mafanikio.

Mhe. Naibu Spika, pia niende sehemu ya nne ambayo kuna katazo la picha za ngono; kwanza mimi nilitaka kujua tafsiri ya hili neno ngono maana tuna maalim Haroun kila siku hapa anaturekebisha kwa kutumia maneno ambayo sio yetu ya asili.

Pia, nilitaka kusema mahala hapa ndipo panapotuharibia sana jamii yetu, kwa hivyo, mimi napendekeza Mhe. Waziri faini iliyowekwa mimi naiona ni ndogo na pendekezo langu kila penye faini hizi mimi nilikuwa nataka kusema penye 2,000,000/= basi iongezwe ya tatu, na penye 1,000,000/= basi iongezwe ya pili, kwa sababu hapa ndipo pahala ambapo tatizo lake linakuwa kubwa na limeshaathiri jamii yetu kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Sehemu ya Tisa ambayo inaeleza masharti ya fedha katika kifungu hiki cha 49(1). "Kutakuwa na fedha za Baraza zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi". Fedha hizi mimi nadhani ni za ruzuku, kwa hivyo nadhani tungelisema kwamba kutakuwa na fedha za ruzuku za Baraza zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi lakini na fedha nyengine zitakazopatikana kutoka kwa wafadhili au ada nyenginezo, ili kuweza kuweka vizuri hii sentensi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mchango wangu haukuwa mkubwa sana na naomba nimuombe sana Mhe. Waziri, sheria hii kama alivyotangulia kusema Mjumbe mwenzangu mama Raya Suleiman Hamad pale, alisema tunahitajika tuanze kutoa elimu, ili sheria hii itakapokuwa tayari basi tuone watu wetu tumewaelimisha kwanza, wasijewakasema wamevamiwa tu. Elimu iendelee kutoka na sisi Wazazi ambao ndio tunao hao vijana na watoto ambao wanaoshughulika na mambo haya, bado tuchukue fursa hii kuwaelimisha watoto wetu, ili waone kama wanaulinda utamaduni wao wasije wakawa watumwa kwa kukosa utamaduni wa nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja na nawaomba Wajumbe wenzangu wote wachangie na kuunga mkono ili iweze kupita sheria hii iweze kuleta tija kwa watu wetu, kwa sanaa za nchini kwetu na tamaduni zetu ili watu waweze kupiga hatua moja kwenda mbele.

Mhe. Naibu Spika: Asante Mheshimiwa kwa mchango wako, sasa nafasi tunampa Mhe. Mgeni Hassan Juma, afuatiwe na Mhe. Hija Hassa na tunamalizia na Mhe. Saleh Nassor Juma, muasisi.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa muda wa kuweza kuchangia katika Sheria hii ambayo itawezesha kuwa na Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehma ambaye katujaalia kuwepo hapa leo tukiwa wazima wa afya. Lakini vile vile nimpongeze Mhe. Spika, nimpongeze sana Waziri anayehusika kwa kutuletea sheria hii ambayo tunaweza kuona kwamba ni sheria itakayosaidia sana katika kuweka maadili yetu, utamaduni wetu na silka zetu katika mstari ulionyooka,

Mhe. Naibu Spika, naanza kwa kusema kuwa lengo kubwa la Baraza hili ni kusimamia majukumu ya kulinda na kuhifadhi mila, silka na maadili ya Wazanzibari. Lakini pia lengo jengine ni kuhakikisha kwamba silka hizi na

utamaduni unatumika katika kupunguza umasikini kwa Wazanzibari. Kwa maana hiyo Sheria hii ina umuhimu mkubwa sana. Kwa sababu moja katika jambo ambalo Serikali imekuwa ikilisimamia vizuri ni kuhakikisha kwamba wananchi wake wanafaidika kutokana na rasilimali walizonazo.

Mswada huu unamaanisha kuwa mbali ya kutoa vibali maalum kwa ajili ya michezo, utamaduni, lakini itasaidia katika kuhifadhi utamaduni wetu ambao tunapouhifadhi, ina maana tunatengeneza mazingira ya watu kutoka nje kuja Zanzibar kuona silka zetu na utamaduni wetu. Hilo ni jambo ambalo linaweza kuongeza mapato ya kitalii.

Mhe. Spika, nchi mbali mbali duniani zinautumia sana utamaduni wake kwa ajili ya kuongeza kipato na kuleta mapato ya fedha ndani ya nchi. Tukitizama katika nchi za Asia hasa katika visiwa vidogo vidogo rasilimali yao kubwa ni utalii.Lakini utalii ule unatengenezwa kwa kuhakikisha kwamba utamaduni utaweza kuvutia watu kutoka nje. Lakini utamaduni ule ni ule ule ambao wa kiasili, ambao wenyewe wanautumia katika maisha yao ya kila siku. Sasa tatizo kubwa kwetu sisi kwamba mambo yale ya asili mengi tumeyapoteza. Hilo ni tatizo na itakuwa ni vigumu sana kuona yale mapato yanaingia kwa sababu bado hatuna uhifadhi mzuri wa mila na tamaduni zetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimepata faraja kubwa sana kuona kwamba leo sasa tunaanza kuona umuhimu wa kuhifadhi tamaduni pamoja na silka zetu. Tamaduni hizi hatuchukulii kwamba ni kucheza ngoma. Mimi nimesikitishwa na sijui itakuwaje au vipi, lakini kuna mambo ambayo humu kama hayajajitokeza vizuri. Isipokuwa kwa sababu lengo hasa la kuanzisha Baraza hili, linaonekana kwamba ni kuhifadhi zaidi masuala ya ngoma, pamoja na vitu vyengine, lakini utamaduni, mavazi yanaingia kwenye utamaduni, chakula kinaingia katika utamaduni.

Tuna tamaduni nyengine ambazo mfano masuala ya hadithi yanaingia katika tamaduni za watu na yanaweza kupamba utamaduni wa taifa lolote. Niseme tu kwamba ndani ya faraja hiyo naona bado kunatakiwa kufanya utafiti wa hali ya juu kuhakikisha tunaweza kuhifadhi ule utamaduni.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni *promoters,* tunatamaduni nyingi sana. Tunatamaduni ambazo zinatokana na nchi nyengine na hizo ni muhimu sana kuzihifadhi kwa sababu ndizo zilizotengeneza Wazanzari. Sasa tukizikosa tamaduni zile na kama hatujazihifadhi nchi za nje hazitojua Zanzibar imetokana na nini na hiyo ni fahari ya Wazanzibari. Kwa hivyo mimi ningeomba sana tunapozungumzia uhifadhi wa utamaduni na mila na silka ya Mzanzibari, tuanzie mbali, ili na vizazi vyetu vinavyokuja vijue kwamba tulikuwa na utamaduni huu na tamaduni nyengine, zina umuhimu mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, tamaduni nyengine tunazihisi kwamba hata hizi njia ambazo walikuwa wezee wetu walikuwa wanazitumia kwa kutukataza, kwenye makatazo, mfano kama ukila usiku kwenye kiza unakula na shetani. Haikuwa lengo ni hilo lakini zile ni tamaduni ambazo unaweza ukaona kwamba katika maeneo mengine uhisikuti lakini zipo Zanzibar. Kwa hivyo katika utafiti ambao utafanywa ningeomba sana tutizame zile tamaduni na silka zilizomtengeneza Mzanzibari, zina umuhimu mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nafikiri una kazi kubwa sana na kazi kubwa hasa itakayokupata ni ile ya kusimamia utandawazi. Nimeona kwamba moja katika mambo ambayo yamo katika madhumuni ya malengo ya sheria hii ni kuweka mipango ambayo itadhibiti utandawazi hasa katika masuala ya kuporomoka kwa maadili. Mimi niseme kazi hii sio rahisi hata kidogo na inahitaji kushirikiana na taasisi mbali mbali zinazoshughulikia masuala ya mawasiliano. Kama tunavyofahamu kwamba utandawazi hauji hivi hivi lakini kuna masuala mazima ya mawasiliano.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba sana wizara yako ndani ya haya ambayo tumeyazungumza hapa kuhusiana na utandawazi, kuhisiana na kuporomoka kwa maadili kwa sababu vijana wetu wengi wanatumia mawasiliano, wanatumia vifaa mbali mbali vya teknolijia, wanapata *influences* za sehemu nyengine nje ambazo leo tunasema kwamba vijana wetu wameharibika lakini ni kutokana na utandawazi.

Mhe. Naibu Spika, kama Mhe. Wanu Hadidh Ameir, alivyosema asubuhi wakati unafungua dirisha hupati upepo peke yake, utapata na vumbi na nzi na mbu, vyote vitaingia ndani. Kwa hiyo mimi nafikiria kwamba kazi nzito ya kudhibiti silka zetu na mila zetu, lazima teknolojia itumike ya hali ya juu kuhakikisha na wanafanya nchi nyengine mfano China. China haviingii vitu upuuzi upuuzi, kwa sababu wanauwezo wa teknolojia na kweli wanahakikisha kwamba wanataka kudhibiti watu wake. Kwa hivyo hilo ningeliomba Mheshimiwa lifanyiwe kazi.

Mhe. Naibu Spika, jengine niombe Wizara yako itumie nafasi ya kuelimisha wazee. Wazee wanahitaji sana kuelimishwa na wanahitaji kuelimishwa kwa sababu hawagundui kwamba kuachiwa watoto wakatumia utandawazi kunasababisha watoto wao maadili kuporomoko. Sasa elimu inahitaji kutolewa katika maeneo mbali mbali. Mpaka vijijini sasa hivi hakuna pahali ambapo utandawazi haujaingia. lakini tuhakikishe kwamba elimu inatolewa. Ningeomba sana mshirikiane na Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu ndiyo yenye watoto, Wizara ya Elimu ndiyo yenye wazee. Kwa hivyo, mshirikiane kuhakikisha kwamba yale mambo ambayo hayapendezi ndani ya jamii yasifanyike.

Mhe. Naibu Spika, jengine tunaweza kuwatumia viongozi wa dini mbali mbali ambao hawa nao, kwa sababu Wazanzibari karibu asilimia 99 wote ni waumini wa dini mbali mbali. Ina maana kwamba hawa tunaweza kuwatumia katika masuala mbali mbali ya kuelimisha jamii. Nashukuru kwamba katika zile kamati ambazo zitaundwa basi na viongozi wa dini watashirikishwa. Kwa hilo nikupongeze sana Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilikuwa nataka kulizungumzia ambalo nimeliona ni muhimu sana, ni suala zima la udhibiti wa maeneo ya starehe. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Waziri kushirikiana na Kamati za Wilaya na kushirikiana na masheha. Kunajitokeza maeneo ya starehe kwenye nyumba ambazo zinaitwa *bar* bubu, ambazo ni nyingi sana sasa hivi. Naamini kwamba watu wengi wanazijua na naamini viongozi katika maeneo yao wanayajua, lakini hazifanyiwi kazi. Kwa bahati mbaya sana watoto wetu wanakwenda katika maeneo hayo, watoto wadogo wanaanza kujifundisha kunywa pombe.

Mhe. Waziri nikwambie kitu kimoja ambacho Mhe. Wanu Hafidh Ameir alikizungumza asubuhi. Kwa nchi za wenzetu ambao hao tunasema wanatuletea hayo mambo mengine mtoto aliyekuwa hajatimia miaka 18 hana nafasi ya kupata pombe mahali popote. Kwa sababu inajulikana kwamba huyu *under 18* na yule mwenyebiashara anahofu sheria, kwamba sheria hii inanikataza kumpa pombe huyu, pindipo nikimpa pombe biashara yangu itafungwa.

Lakini kwa sababu tumeyaachia haya mambo watu wanafanya kweupe na hii ni hatari. Mhe. Naibu Waziri nakuomba sana katika masuala haya ambayo unaweza kufanya kazi na wenzio ufanye kazi na wenzio, ili uhakikishe kwamba haya mambo tunapozungumza yanahitaji kufanyiwa kazi. Kwa sababu hizi sheria tunapozileta hapa kwa kweli inawezekana na zina *sound* vizuri. Lakini kama kunakuwa hakuna utekelezaji katika sheria hizi inakuwa ni bure. Mhe. Waziri nafikiri sote tunaelewa kwamba inakuwa hazina maana na hili ni tatizo na sisi ndio wa kulaumiwa sio mwengine yoyote sisi ndio tunabeba jukumu hilo.

Mhe. Waziri kwa hiyo kila mmoja awe makini katika suala hilo. Kesho tutakwenda kusema nini mbele ya haki, kwamba tumeacha vizazi vyetu viharibike. Kama hatujachukua hatua leo mimi naamini kabisa kwamba Mhe. Waziri tutakuja kuulizwa mbele ya haki, hiyo ni imani yangu.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niingie katika sheria yenyewe. Katika kuangalia Sheria hii katika tafsiri ya neno sanaa. Kidogo nimepata wasi wasi na nimeona kwamba tafsiri imetafsiri neno *conscious* ambayo maana yake humu limewekwa kwamba ni akili. Lakini ninavyofahamu mimi *conscious* sio akili tu lakini *sense* nyengine ambazo tulizonazo nazo zinakuwa zipo *conscious*. Sasa basi naona kwamba neno *conscious* limetumika vibaya. Kwa sababu sanaa inasema maana yake ni:

> "Ubunifu unaotumia akili au kazi iliyotayarishwa kwa njia ya sauti, rangi, umbo au mwendo, jambo jengine katika hali ambayo inashawishi akili."

Lakini ya kiingereza inasema kwamba:

> "Art *means a conscious production or arrangement of sounds, colors, forms, movements or other elements in a manner that affects the sense of beauty, specifically the production of the beautiful in a graphic such as paintings, sculpture, music, carvings, photographs, drawings, maps and otherrelated handicraft work."*

Sasa hii tafsiri yake Mhe. Waziri, mimi sikuona umuhimu kwanza wa kusema ubunifu ambao unatumia akili. Kwa sababu tayari ubunifu unatumia akili, ukisema mtu kabuni kitu fulani maana yake kabuni kwa kutumia akili. Sasa hapa badala yake ingekuwa inasema tu kwamba maana ya ubunifu ni kazi.

Sanaa maana yake ni kazi ya ubunifu au kazi iliyotayarishwa kwa njia ya sauti na kuondoa neno lile 'akili'. Naomba hili mlitizame tena lakini mimi haliingii kwenye akili yangu kwamba hili neno *conscious* maana yake ni akili.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia ni katika ukurasa wa 389 ya muundo wa Baraza. Nilikuwa naomba tu kwamba juu ya kuwa pamewekwa Mkurugenzi anayehusika na masuala ya wanawake lakini isifunge nafasi nyengine pia kuteuliwa mwanamke kusimamia zile. Kwa hiyo ningeomba sana katika Baraza hili nafasi hii isiwe tu kwamba kwa sababu mwanamke yupo kwenye idara basi wengine wasiweze kuja.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni katika kifungu cha 6 ambayo ina sifa za Mwenyekiti. Sifa ya Mwenyekiti, tumezoea hapa kwamba sifa mara nyingi za Mwenyekiti, anaambiwa awe na Shahada, awa na hili, lakini hapa hamna. Mhe. Waziri natambua kwamba kuna watu hapa Unguja wana Shahada za sanaa au Diploma za Sanaa kwa sababu tunavyo vyuo vya sanaa vya muda mrefu. Sasa kwa nini tusiweke na sifa ya elimu hapa kwa sababu ni Mwenyekiti wa Sanaa tukuchukulie kwamba ni mtu yeyote ambaye ana uzoefu na ujuzi. Sanaa inataka elimu, sio ujuzi peke yake na uelewa peke yake wa sanaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeshauri kwamba hapa pia iwekwe sifa ya elimu. Kwa sababu sheria hii itatumika baadaye huko mbele miaka ijayo. Hiki kitakuwa ni kigezo kimoja ambacho kitasababisha watu wengine wenye elimu wanaweza kupata hii nafasi. Tunaposema elimu tunatayarisha , watu wengine kujua kwamba umuhimu wa elimu ni nini. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri hilo pia liwemo ndani ya sifa za Mwenyekiti.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na jambo ambalo kidogo nilikuwa linanitatiza na nimeona nimuulize Mhe. Waziri kuwa nani atakuwa na mamlaka ya kutambua kazi za sanaa za watu binafsi au vikundi ili waweze kwa sababu ninajua kwamba kuna taasisi ambayo inatoa haki miliki. Lakini sasa Baraza la Sanaa lina wajibu wa kuweza kutambua ni ile *recognition* ya ile kazi yake si jengine lolote. Ni *recognition* ambayo inasema kwamba fulani amebuni kitu fulani, sasa nani atakuwa na mamlaka hayo. Nimetizama bado nilikuwa sijaweza kufahamu kwamba ndani ya humu sikuona pahala ambapo inampa mtu kutambuliwa kwa kazi yake ambayo ameifanya. Mhe. Spika, ningemuomba Waziri na hilo pia aje anijibu.

Nakwenda katika ukurasa wa 396 ambapo wenzangu walizungumzia, ingawa Mwanasheria mmoja kanambia hiyo haihusiani suala la kwamba Waziri anakuwa na maamuzi ya mwisho lakini kuna Mwanasheria kanambia hiyo inawezekana kubakia hivyo, lakini ikawa kwamba bado ile Katiba kwenye Katiba yenyewe ina mamlaka yake vile vile na uzito wake. Kwa hivyo mtu yeyote anaweza kupeleka malalamiko mahkamani. Nilikuwa nataka kwa sababu na mimi kama wenzangu wameliona hili kwamba kwa kweli sio jambo jema kwamba Waziri amalizie hapo.

Mhe. Naibu Spika, mengine ambayo nimeyaona ndani ya mswada huu, kwa kweli yote ni mazuri na niseme tu kwamba kidogo nimepata masikitiko kuona kwamba kuna vitu ambavyo havijaainishwa humu ndani. Zanzibar tuna utajiri wa hadithi za kale na hizi hadithi za kale zinataka kuhifadhiwa. Na kuna watu ambao wanazo vichwani mwao na nyengine kuna watu wanazijua na bado wanaendelea kuzihadithi. Hii iwe ni *task* muhimu sana, kwa sababu nasema tena na ninafikiri nimeshasema kwamba kuna baadhi ya hadithi zinatoa mafunzo mazuri kwa watoto.

Kwa hivyo, hizi hadithi, hili Baraza la Sanaa lihakikishe kwamba linachukua shughuli hii ya kuhifadhi hadithi na kuweza kuziandika katika maandiko ambayo yataweza kuziweka hadithi hizi kwa muda mrefu. Hilo nimeona kwamba halijaelezewa na kwingi ukizitazama kunazungumziwa ngoma, *CD*, *film* na nini lakini hadithi za kale humu hazijawekwa. Ningependa sana kuona kwamba na hadithi za kale zinathaminiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia ninaingia katika sehemu ya tano kwenye ukurasa wa 401. Nimefurahi sana kuona kuwa kutakuwa na maonesho ya machapisho au usambazaji wa mabango ya matangazo, na hawa wapo kwa sababu kwenye jamii yetu hasa mjini hata ukenda katika vijiji unakuta kuna matangazo mengi sana. Na kwa sababu hamkuainisha hapa ni matangazo ya aina gani lakini kama ikiwa ya sanaa, kama ikiwa yanahusiana na waganga wa kienyeji, nyinyi mtakuwa mnakataza matangazo yote ambayo hayaendani na maadili yetu, mna uhuru wa kuyakataza.

Sasa mimi hapa nilikuwa na suala kwa sababu kuna matangazo ambayo kwa kweli yanaanza kututia wasiwasi. Kuna watu wanafanya kazi ambazo kazi hii anaiweza Mwenyezi Mungu tu wao hawawezi na matangazo hayo yanawekwa na yale matangazo yatawapa picha mbaya vizazi vyetu, kwa sababu wataanza kuelewa kumbe kuna wengine wanaweza kurudisha uhai wa binaadamu. Kuna matangazo nyote nyinyi mnaona matangazo, kuna matangazo

ambayo mtu anatangaza kusema kwamba, anatoa mashetani, anarudisha nguvu za kiume, matangazo ya aina mbali mbali yale ambayo watoto wanakuwa wanaoneshwa mambo ambayo hayahusiani.

Sasa mimi nitafurahi sana kwa sababu naona wengine ambao wana kazi hizo wameshindwa kufanya Mhe. Waziri, kama kazi hiyo umepewa wewe mimi nimefurahi sana. Kwa sababu ninaamini utaifanya lakini kuna matangazo hayaendani na silka zetu na haya matangazo si mazuri kuwepo katika maeneo yetu. Kwa sababu yanatuharibia watoto wetu pia yanawapotoa hata wale wengine wenye ufahamu mdogo wa kuona kwamba kuna mwengine zaidi ya Mwenyezi Mungu ambaye anaweza kuwarekebishia matatizo yao kwani kuna mengine wanazidisha hao wanaotangaza.

Mheshimiwa kwa hivyo mimi ningekuomba sana kuwe na udhibiti wa matangazo haya sijui kama wewe yanakuhusu haya lakini mimi naamini kama wewe yanakuhusu au wengine ambao wanashindwa matangazo haya, basi wewe utaweza kuyazuia matangazo haya.

Mhe. Naibu Spika, mimi tu niseme la mwisho kabisa ingekuwa napewa mimi rungu hawa wanaosema kwamba wakionesha picha hizi za ngono watalipa faini ya shilingi 2,000,000/= mimi naona ni kidogo sana. Milioni mbili *is nothing* sasa hivi, ningeomba sana hawa walipishwe zaidi ya milioni mbili, kwa sababu 2,000,000/= sana hivi imekuwa kila mtu analipa 2,000,000/= watu wanaziona ni kidogo. Huyu mwenye uwezo wa kufanya haya, huyu afanye biashara hii kwa 2,000,000/= Mhe. Waziri, hizi ni biashara zenye pesa nyingi sana. Sasa mtu mwenye Kampuni au mwenye *film* ambayo inaonesha mambo haya thamani yake ni kubwa. Kwa hivyo Mheshimiwa kwa hili isiwe 2,000,000/=, naomba sana hii iongezwe mara dufu, ili hili jambo likomeshwe.

Mhe. Waziri, tukisema kwamba leo anayeleta picha chafu hapa Zanzibar akazisambaza tunamtolesha 2,000,000/= watakuja wengi mno, wengi watakuja hapa kwa sababu wanaona kwamba hii wamefunguliwa mlango 2,000,000/=, atatoa na atakwenda zake ataleta nyengine. Kwa sababu ndani ya faida ambayo anaipata 2,000,000/= sio kitu. Kwa hivyo ningeomba sheria hii ihakikishe kwamba wale ambao wana nia au wanaleta *film* hizi watozwe zaidi ya milioni mbili ambazo zimeandikwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache nikushukuru tena kwa kunipa nafasi lakini nimtakie kila la kheri Mhe. Waziri na pia naunga mkono sheria hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii na mimi kukushukuru na naomba nitoe mchango wangu kwa mswada huu na nadhani dakika 40 zitanitosha kutoa mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwenye ukurasa wa 405 kwenye sababu na madhumuni ya mswada huu. Mhe. Waziri amesema kwamba madhumuni ya mswada huu ni kufuta Sheria Namba 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki na Sheria Namba 1 mwaka 2009 ya Bodi ya Sensa na Kutunga Sheria mpya ya Baraza la Sanaa ya 2015.

Madhumuni ya sheria hii Mhe. Spika, ni kuhifadhi mila silka na maadili mema ya wazanzibari na kwamba utamaduni unaozingatiwa ni utamaduni wa kizanzibari. Kwa hivyo ningetegemea mswada huu utazungumzia silka, mila, utamaduni wa wazanzibari kwa hivyo kadiri ambavyo tutazungumzia kwenye mswada huu kwa madhumuni haya Mhe. Waziri aliyosema ni kwamba lazima tuzingatie maadili, silka na utamaduni wa wazazanzibari wenyewe.

Mhe. Waziri ameseama zaidi kwamba sababu nyengine wanakusudia kupunguza malalamiko kwamba baadhi ya maeneo kupigwa ngoma mpaka saa 4.00 za usiku au zaidi, kwa hivyo hizo ndio sababu mswada huu umekuja ili kupunguza mambo hayo na kulinda utamaduni wa wazanzibari na maslahi ya wazanzibari wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi Mhe. Farida kasema hapa kwamba wananchi maeneo ya Amani Mkoa wa Mjini Magharibi kila siku ya Mungu wamekuwa wakilalamika kwamba utaratibu unaoendeshwa pale wa kupiga ngoma bila ya kuzingatia utaratibu kwa kweli umekuwa ni maudhi makubwa. Kwa hivyo sheria hiyo Mhe. Spika, ikiwa kweli Serikali ina lengo hilo watapumzika wananchi wa Amani na wananchi wa maeneo mengine Unguja na Pemba. Wakati mwengine mimi nimekuwa nikishangaa sana kwamba Wizara inatoa vibali vya kuendesha shughuli ya ngoma au kuendesha mabaa katikati ya mji au kati kati ya misikiti ambayo watu wengine wanafanya ibada. Sasa pengine sheria hii itawakumbusha wale wenye tabia ya kutoa vibali ndani ya maeneo ya makaazi ya watu, maeneo ya makaazi ya majengo ya ibada na maeneo ya makaazi ya majengo ya kutoa elimu kwa maana ya shule.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa niende kwenye mswada wenyewe, niende kwenye ukurasa wa 387 tafsiri. Mhe. Naibu Spika, tafsiri ya neno ada maana yake ni "kiasi cha fedha kitacholipwa na mtu", naomba tuongeze "mtu na taasisi kwa ajili ya kupata kitu au huduma" ili isiwe mtu tu bali iwe na taasisi ili lengo lake kupata huduma.

Lakini tafsiri ya neno utamaduni maana "ni aina zote za vikundi vinavyojihusisha na utamaduni", naomba tuongeze "wa Zanzibar". Kwa hivyo mswada huu lengo lake ni kuulinda utamaduni wa Zanzibar kwa hivyo tafsiri ya utamaduni neno Zanzibar liongezwe ili kulinda maslahi ya utamaduni wa Zanzibar.

Ukurasa huo huo Mhe. Naibu Spika, inaonekana serikali haijui tofauti ya ngoma na ngoma za utamaduni. Kwa sababu mswada huu umechanganya mambo hayo kwamba ngoma wao wanaona ni ngoma tu, lakini kwa tafsiri yangu mimi ziko ngoma kwa maana ya ngoma na ngoma za utamaduni wa Zanzibar. Sasa huwezi ukasema kwamba baikoko ni utamaduni wa Zanzibar, rusha roho ni utamaduni wa Zanzibar, *disco* utamaduni wa Zanzibar. Wazanzibari wamezoea kuona Msewe, Kibati, Sindimba, Msondo, Pungwa, Mwaka Kogwa na Mbio za Ngalawa; haya ndio mambo ambayo Wazanzibari wameyazoea kuyaona.

Kwa hivyo Serikali ikiwa haioni tofauti baina ya ngoma za kileo baikoko na mambo mengine wanachanganya kuwa hizo zote ni ngoma za utamaduni. Mhe. Naibu Spika, naomba tuongeze tafsiri; kuna tafsiri ya ngoma nyenginezo na ngoma za Utamaduni wa Zanzibar ziwe bayana tuzijuwe; kwamba rusha roho wala haitakuwa utamaduni wa wazanzibari, rusha roho ni fujo tu lakini mzanzibari hatopigiwa msewe akakasirika, mzanzibari hatopigiwa kibati akakasirika. Lakini mzanzibari akipigiwa *disco*, akipigiwa rusha roho na mashaka mengine lazima wazanzibari watakasirika kwa sababu ni ngoma ambayo haizingatii utamaduni, haizingatii heshima ya mavazi kwani huwezi kuingia kwenye msewe baadaye ukavaa buti na koti lazima uvae vazi la kimsewe.

Huwezi kuimba kibati usivae nguo za kibati. Huwezi kuimba, kupiga maulidi ya homu usivae mavazi ya maulidi ya homu, huu ndio utamaduni wa Zanzibar.

Kuna watu watashangaa sana wakimuona mtu anaimba maulidi ya homu lakini amevaa tai, ataonekana huyu jamii kidogo ameingia mchomo. Kwa hivyo si utamaduni wa wazanzibari wenyewe. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, lazima Wizara iongeze tafsiri ya ngoma nyenginezo na tafsiri ya ngoma za utamaduni wa Zanzibar.

Ukurasa wa 389 Mhe. Naibu Spika, naomba kifungu cha 3(2), naomba kusoma;

> "Baraza litakuwa ni wakala wa serikali na lenye muhuri na litakuwa na uwezo wa kutumia jina lake, tuongeze kwa badala ya wa."

Mhe. Naibu Spika, ukurasa mwengine ambao ninataka nichangie ni 392 kifungu cha 9(5) akidi ya kikao cha Baraza itapatikana kwa zaidi ya nusu ya wajumbe "watakaohudhuria" sio ya "waliohudhuria". Wajumbe wataohudhuria wakifikia zaidi ya nusu hiyo ndio itakuwa ni akidi ya kikao cha Baraza hilo.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 393 kifungu cha 11(2)(c), naomba kusoma:

"Ametiwa hatiani kwa kosa la kimaadili..., naomba tuongeze na "jinai" kwamba mtu huyu akitiwa hatiani kwa kosa la kimaadili na jinai basi anakuwa hafai kuwa mjumbe wa Baraza". Sio maadili lakini pia tuongeza na jinai.

Mhe. Naibu Spika, kifungu chengine ambacho naomba kuchangia ni kifungu cha 22(b) na 22(e) ukisoma kwa makini vinalingana naomba 22(b) kiondoke na kibakie 22(e) kwa sababu maana yake ni sawa sawa na naomba kusoma. 22(b) kinasema:

Kutafautisha majina katika fomu maalum ambayo atasajili vikundi vya sanaa na utamaduni, 22(e) ataweka kumbukumbu za orodha ya vikundi vya utamaduni vilivyosajiliwa kwa utaratibu maalum. Naomba kwa kiswahili kizuri 22(b) nadhani kiondoke ibakie 22(e) kwa sababu ni kazi za kuweka kumbukumbu za vyama vya usajili vya utamaduni.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ni kifungu cha 24(3) kwamba uamuzi wa Waziri utakuwa ni wa mwisho. Mhe. Spika, nadhani baada ya mtu kutoridhika na maamuzi ya Baraza akakata rufaa kwa maamuzi ya Waziri, nadhani

maamuzi ya Waziri yasiwe ya mwisho bado mtu apate nafasi ya kwenda Mahkamani. Kwa sababu Baraza limeamua na mtu hakuridhika wameamua kukata rufaa kwa Waziri, Waziri ameamua mtu hukuridhika bado mtu huyo apewe fursa ya kwenda mahkamani ili kupingana na maamuzi ya Waziri ili kuweza kupata haki. Mahkama ndio peke yake inaweza kutoa haki kwa mtu yeyote kwa taasisi yoyote.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ambayo nataka niiseme kwenye mswada huu ni ukurasa wa 402 na naomba tuongeze kwamba kifungu cha 47 kinasema hivi;

"Biashara za ngono za watoto."

Mhe. Naibu Spika, hapa imewekwa adhabu kwa wale ambao wanaonesha picha za ngono, wenzangu wamezungumza lakini Wizara imesahau kwamba kuna watu wanaonesha picha za ngono, lakini kuna watu wanauza biashara ya ngono. Kwa hivyo, mimi nimechukua mtandao nimeonesha picha ya ngono ninatiwa hatiani, lakini wanaojikusanya maeneo fulani hapa Zanzibar wakafanya biashara za ngono wao hawana kosa.

Kwa hivyo, nadhani kifungu cha 47 kiongozwe 47(1) ili liongezwe suala la biashara ya ngono. Wale wote ambao wanafanya biashara ya ngono hadharani au kwenye majumba ambayo ni majumba ya biashara ya ngono basi wawe ni wakosa na watiwe hatiani kama ambavyo sheria hii ilikusudia. Haiwezekani kwamba mtu anayeonesha picha yeye atiwe hatiani, afungwe lakini anayefanya biashara hadharani kwa maana ya biashara, nyumba zimekodishwa kwa ajili ya biashara hiyo hatimaye iachiwe na iwe si kosa, nadhani Mhe. Waziri hili lizingatie na tuweze kuchukua hatua kama ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 49 naomba tuongeze kifungu cha 49 (3) kwamba fedha na mapato ya Baraza yataingizwa kwenye *account* maalum ya Baraza. Naomba kuwe na *account* maalum ya Baraza na kiwe kifungu cha 49 (3) kwamba kutakuwa na *account* maalum ya Baraza kwa lengo ya kuhifadhi mapato yote na fedha zote za Baraza badala ya kuachwa hivi hivi.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 51 (3) mwisho naomba tuongeze “kwa ukaguzi”, kwamba katika kipindi cha miezi mitatu ya kila mwaka wa fedha ikiwemo ripoti ya matumizi ya fedha ya Baraza itawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, naomba tuongeze maneno “kwa ukaguzi” ili kazi yake hiyo iweze kufanyika vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 53 (3) hapa kuna adhabu kwa mtu ambaye anafahamu kwamba lipo kosa la kufanya vitendo vya ngono na kufanya makosa mengine. Kwamba mimi kama nitafahamu huyu anafanya kosa na nisitoe taarifa basi kuna hatia, nadhani ni hatua nzuri itawafanya wananchi sasa kutofumbia macho makosa ili kosa likitendeka lazima tutoe ripoti na wahusika waweze kuchukuliwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 54 waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sheria hii. Naomba tuseme kwamba “waziri atatunga kanuni” sio anaweza, anaweza ni ridhaa lakini tumpe lazima kwamba atunge kanuni ili sheria hii iweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kanuni sheria hii itakuwa haiwezi kufanya haraka na badala yake anaweza waziri alazimishwe tu kwamba baada ya sheria kupitishwa basi atunge kanuni kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi wa sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 55 kufuta na kubakiza 55 (2) naomba tuongeze maneno kwamba "bila ya kuathiri ufutaji uliofanywa na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki jambo lolote litakalofanywa kwa mujibu wa sheria zilizofutwa linachukuliwa kama limefanywa kwa mujibu wa sheria hii". Naomba tuongeze kwamba "isipokuwa liwe linapingana na sheria hii", kwa sababu inawezekana liko jambo linapingana na sheria hii tukisema tuliache itakuwa ni makosa. Kwa hivyo, tuongeze maneno kwamba “isipokuwa liwe limepingana na sheria hii” litakuwa linakubali kufutwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo niseme tu kwamba mswada huu lazima tuwe wazi, lazima Mhe. Waziri tuongeze na tulinde maadili na utamaduni wa Mzanzibari na wizara isichanganye baina ya utamaduni wa Mzanzibari na utamaduni wa nje. Lazima mutuwekee wazi upi utamaduni wa Mzanzibari na upi utamaduni wa nje ili Wazanzibari tuulinde na ule utamaduni wa nje lazima tuuchunge, kwa sababu huwezi mambo ya ndani ya nchi

ambayo watu wameyazoea na hayana athari yoyote ukayawekea sawa sawa na mambo ya nje ambayo ni mambo ya kuiga.

Lazima nchi yoyote duniani iwe na utamaduni na ulindwe kwa nguvu zote na yale mambo ya nje ambayo sio mambo yetu lazima yachungwe na iendane na sifa ya utamaduni wa ndani. Nasisitiza kwamba mavazi mafupi yanayoathiri maadili yetu lazima yadhibitiwe kwenye sheria hii, ili wananchi wetu waweze kulinda maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba kuunga mkono.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii ya kueleza chochote katika hoja iliyoko mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, mimi si msemaji sana katika masuala haya ya mambo ya ngoma ngoma na mambo ya muziki, lakini nitatia tia nyalio tu kidogo na kuielekeza serikali katika baadhi ya mambo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuleta huu mswada. Unajua kabla sijaanza kumpongeza nilisifu Baraza zima la Mawaziri hili la Mawaziri wa Zanzibar kwa sababu nimeangalia nikaona kwamba ni miongoni mwa Mabaraza makini sana. Sasa nimemuangalia Maalim Said Ali Mbarouk, Waziri wa Wizara hii nimelinganisha na waziri mmoja yuko katika Baraza moja la Mawaziri katika *Monarch Country* sitaki niitaje, ni makini sana katika mambo. Kwa hivyo, kwa hili nachukua fursa hii kukupongeza Mheshimiwa kwa kuweza kutuletea huu mswada.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mswada huu naweza nikauchukulia kwamba ni muarubaini pengine kwa kero ambazo tunazipata sana katika nchi hii kutokana na bughudha za haya magoma.

Mhe. Naibu Spika, kipo kilio cha muda mrefu sana kwamba hivi vikundi haviwi *assessed,* vinapiga piga tu magoma jambo ambalo ni tatizo. Ni tatizo kubwa tunakuwa na shida sana sisi Wazanzibari katika siku za sherehe mbali mbali za nchi, katika maadhimisho ya sherehe za serikali wanajipigia pigia vyao tu magoma katika maeneo ambayo hayastahiki wakati mwengine.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni mimi niko karibu na sehemu moja ya starehe wanaita *Mortuary* pale Vitongoji *Fidel Castro* yalifanyika maadhimisho ya mwenge wa uhuru, yalipofanyika maadhimisho ya mwenge wa uhuru kuanzia Umangani, Udusini, Vumba, Changuo mwahala mote humu watu hawakupata usingizi kutokana na zogo lilikuwepo la ngoma la maadhimisho ya sherehe za mwenge wa uhuru.

Asubuhi tulipata balaa jengine ilibidi tuwaite Baraza la Mji kwa sababu sisi tulishindwa kuondosha zile taka taka zilizowekwa baada ya maadhimisho ya sherehe za mwenge, maana nyengine zilikuwa hazikamatiki kwa mikono. Naogopa kuja kukiuka Kanuni za Baraza kwa sababu nikizitaja pengine itakuwa nimetumia lugha chafu, lakini zinaweka mpaka mambo ambayo hayatajiki katika Baraza hili, huwezi kutaja. Sisi tulizoa, tukashindwa tukawita Baraza la Mji la Chake Chake wakaja wakatusaidia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kwamba sheria hii itakuwa mkombozi wa adha hii tuliokuwa nayo ya muda mrefu sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba tu serikali katika kuvitathmini na tukiangalia hivi vikundi vya sanaa pamoja na kuvitafutia maeneo basi wawe makini sana. Kwa sababu hapa *Fidel Castro* karibu na *Mortuary* mbali na kwamba kuna wanafunzi wanawakera sana pale wakipiga ngoma, lakini hapa wanapiga ngoma, hapa wanaadhimisha sherehe za mwenge, wanaadhimisha sherehe za Mapinduzi na huu ni Msikiti. Mambo hayo mengine ambayo si rahisi kuyakamata unayakuta yapo katika Baraza la Msikiti. Jambo hili ni tatizo sana Mheshimiwa.

Mimi naamini pengine muarubaini wa matatizo yale, muarubaini wa misikiti kunajisiwa kwa kiasi kile, nadhani huenda ikawa hii sheria. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa katika hili basi sheria tuiunge mkono na *inshaallah biidhinilahi* ipite na Rais asaini ili hizi adha za kupigiwa ngoma, kutupiwa tupiwa madude yaliyokuwa hayafai mle Ubunguni yaondoke.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nimeuangalia huu mswada na nikaangalia huu muundo wa Baraza la Sanaa. Muundo wa Baraza la Sanaa nikaja zangu moja kwa moja mheshimiwa katika kifungu hiki cha 5 (h), wawakilishi wawili

kutoka Jumuiya za Kidini. Kwa kweli hapa Mhe. Waziri umefanya la maana sana kuwatia hawa. Mimi nilifikiri ni vikundi vya sanaa tu vyenye adha pamoja na kuserebuka, pamoja na kucheza ngoma kinyume na mila na silka za Kizanzibari, kumbe mpaka vikundi vya kidini vinafanya tatizo hili.

Hivi juzi nilikuwa na harusi ya binti yangu pale, watoto wangu wakaalika dufu, ilikuwa mtaani hapakaliki, mtaani Mhe. Waziri ilikuwa hapakaliki dufu utafikiri wanacheza ndomboro.

Sasa mimi nimefurahi sana kuwepo wawakilishi wa dini katika masuala haya. Nadhani mheshimiwa na Ofisi ya Mufti japo mtu mmoja aingie ili kusudi waweze kuvi-*handle* hivi vikundi vya dufu, wawape ustaarabu wa kucheza. Mimi nilikuwa si mwanamuziki mheshimiwa lakini rafiki zangu wengi walikuwa ni wana muziki na walikuwa wanapiga bendi hizi za muziki wa dansi akina Songa na Kasaloo Kianga, hawa ni rafiki zangu wakubwa sana walikuwa. Lakini wao hawendi kupanda jukwaa kama hawajavaa suti, hawaendi Songa Kianga na Kasaloo Kianga nilikuwa nakaa nao nyumba moja pale Dar es Salaam, walikuwa wanapiga Kalkat Almasi na baadae wakaja wakaungana na Dkt. Remy pale na Msubwa Matimbila, leo unakuja mtu tu kwenye dufu kavaa na kikanzu hapa. Sasa nakupongeza Mhe. Waziri kwamba sheria hii inaweza ikatunza, mila, silka pamoja na utamaduni wa Kizanzibari, kwa sababu haya mambo yamepotea hivi juzi juzi tu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakumbuka katika miaka ya 1960 katikati wakati huo wajukuu zangu akina Mhe. Wanu hawajazaliwa, alikuwapo muimbaji mmoja anaitwa Siti Binti Sadi, yule mama alikuwa makini sana katika kufanya sanaa zake. Yaani yeye alikuwa akiimba anajifunika uso inasikikana sauti tu kama kinamba, lakini uso wake hauonekani. Jamaa wakaanza kusema ana sura mbaya, mimi ninayo picha yake Siti Binti Sadi, bibi ana sura nzuri sana yule nimejaribu kuangalia angalia sana wanawake na nimekuwa naangalia sana mimi mashindano ya urembo. Lakini nimeangalia haya mashindano ya urembo yaliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, hata yale ya Ulaya Mama Siti kwa sura nzuri alikuwa anawashinda wengi sana katika wale, na alikuwa akijifunika mwenyewe haonekani, unasikia sauti tu.

Sasa hapa inasikitisha sana mheshimiwa kwamba maadili ya nchi kwa sababu sheria iliyokuwepo haisimamii wanakuja kutuvalia vinguo vya kubana, anapanda jukwaani maana yake unaona katika kila sehemu ya mwili. Sasa binadamu tumepewa macho pamoja na utuuzima tuliokuwa nao mheshimiwa wakati mwengine jicho linaweza kupotea likalenga, jicho likiona moyo unatamani, moyo ukitamani inakuwa tatizo, mnatupa shida. Sasa naamini sheria hii itakuwa mkombozi wa mambo mengi sana katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani ili tuweze kufikia sifuri tatu wataalamu katika haya masuala ya afya na ukimwi na maradhi mengine ananiangalia kwa jicho zuri kule kwamba niendelee. Mheshimiwa ili tufikie sifuri tatu yaani ukimwi ziro, maambukizi mapya ziro na *HIV* ziro basi lazima sheria hii tuipitishe hapa, itatusaidia sana kabisa wala musifikiri kwamba inalenga mila na silka tu, tuipitisheni italinda mila ma silka na tutafikia lengo lile serikali inalolitaka.

Nadhani mtaalamu Dkt. Sira kafurahia sana hili, kwa sababu anaona ni kweli sheria hii iko makini sana.

Mhe. Naibu Spika, nije sehemu ya kifungu cha 7 (h), kifungu hiki ambacho kinahusiana na kazi za Baraza naomba Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu uniruhusu nikinukuu kidogo, kinasema hivi;

> “Kuweka utaratibu mzuri wa kuwatambua, kuwapa tunzo wasanii wa zamani ambao wamechangia maendeleo ya kazi za sanaa Zanzibar."

Kwa kweli Serikali ilipokiweka kifungu hiki imefanya jambo la maana sana. Kwa mfano, mheshimiwa hivi sasa serikali inaangalia sana mambo ya magoma magoma tu haya, lakini hawaangalii sanaa nyengine, sanaa hizi zinazohusiana na mambo ya uandishi. Kuna sanaa za aina mbili, kuna fasihi andishi na simulizi.

Sasa ukija ukiangalia katika fasihi hizi; sanaa ya uandishi katika nchi hii imedharauliwa sana na kama kuna waandishi mahiri katika Kusini mwa Jangwa la Sahara basi Zanzibar imekuwa ikiongoza. Hebu tumuangalieni mtu kama Bwana Msa, hebu tumuangalie mtunzi wa Asali Chungu, tuangalie mtunzi wa Nyota ya Rehema ni wa hapa hapa Zanzibar, tumuangalie mtu kama Mzee Haji Gora, hawa watu wanatupotea potea tu hivi hawakumbukwi tena. Halafu kulikuwa na Mama mmoja pale Chake Chake nyimbo zake ilikuwa Mfalme katika miaka ya 1967, Mfalme huyu Said Khalifa alikuwa kila akija Pemba sisi tunampeleka Mama huyu anamuimbia, Mame Kibakora pale na

Binti Silime kutoka Mwambe tulikuwa tukimpelekea. Sasa hivi nashangaa kwamba hawajuulikani tena hawa Mame Kibakora na Binti Silime kutoka Mwambe kwa sababu ya kuwadharau... (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ...Mfalme alikuwa akija siku hizo bado hatujapindua hapa, Mfalme akija Pemba lazima awapate hawa, leo tumewasahau kabisa. Sasa utakutia mheshimiwa mimi nafikiri katika hili tuwe makini sana na sanaa zetu kwa mfano kulikuwa na mama mmoja alikuwa akipiga msondo Bi Hamisa, Bibi huyu alikuwa akichukuliwa Nairobi kwenda kupiga msondo pale harusi mbali mbali Nairobi leo watu hawamjui tena.

Mimi naamini sheria hii itafanya tathmini hata wale wasanii wa zamani akina Bi Hamisa, Bi Saumu Gongo ambao walikuwa wakipiga msondo hawa wakienda mpaka Mombasa, washawahi kufika DRC kupiga msondo tu hawa, leo hatuwajui tena! Ni hazina zimetutoka hivi hivi. Mimi nadhani kuna mambo mengine tukiyafanya hapa kama Siti Binti Sadi, mimi nafikiria kuandaa utaratibu hapa familia yake kuitambua yule mama na kumjengea japo mnara mdogo wa kumbukumbu kiasi ambacho watalii wanaweza kufika na kutalii ule mnara. Mhe. Naibu Spika, mimi nakuomba sana Mhe. Waziri mawazo hayo usiyadharau kwa sababu pamoja na kwamba mimi ni mtu wa sayansi lakini *art* ninaipenda sana mheshimiwa.

Kwa hivyo, sasa nije hapa tunaambiwa kuna yaani ibara ya 7(l) kukuza, kueneza utaratibu wa kusaidia wasanii waliofanya kazi zao kwa uzalendo na si kwa ajili ya kupata kipato bali kwa kuendeleza taaluma na sanaa na kupeleka mbele jumuiya zao na serikali.

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna wasanii nyie mnajali haya Mabongo flava, Zenj Flava hebu jamani tuangalieni mara baada ya Mapinduzi wasanii walivyokuwa wakiimba nyimbo za kutetea nchi yao, za kusifu Mapinduzi kina *Capt*. Mwadini anajuulikana tena hapa? Amedharaulika moja kwa moja nikitaja wadogo zangu akina mheshimiwa hapa hawamjui hata *Capt.* Mwadini, nina hakika wangeipata sauti ya *Capt*. Mwadini hawa basi siku zote wangekuwa wakifurahi. (*Makofi*)

Mimi naomba watu kama wale tusiwasahau sauti zao kama zinapatikana muzichukue ili wajukuu zangu akina Mhe. Wanu pale na Mhe. Ali, hawa waweze kupata sauti nzuri za kina *Capt.* Mwadini kabisa kabisa mheshimiwa. Leo nyimbo za siku hizi zinazoimbwa maana sanaa ni kioo mheshimiwa, sanaa ni kioo ambayo jamii hukitumia halafu ikajirekebisha kama inakosea lakini wao wanaangalia Bongo Flava ndani ya Bongo Flava ujirekebishe nini, ndani ya Zenj Flava ukiangalia kama kioo ujirekebishe nini, huna la kujifunza pale maana hizo nyimbo zenyewe nampenda Binti Kiziwi, haya Binti Kiziwi wapendeka au wapenda Binti Kiziwi unamdhalilisha.

Kama nyimbo nampenda Binti Kiziwi unamdhalilisha, eti nikizungumza na kimada hasikii, haya jamaa hilo si tatizo unadhalilisha jamii, lakini hebu tuangalie zile sanaa za zamani Mhe. Waziri alizokuwa akiimba hapa mama yetu marehebu Siti Binti Sadi, naomba kuniruhusu japo beti moja ninukuu ya nyimbo yake uone jinsi ya nyimbo zilivyokuwa zikitungwa. (*Makofi*)

Kwa mfano, Mama Siti Binti Sadi katika wimbo wake mmoja alisema: "Tamu ya sukari umenipa wewe, umenipa nyingi kusudi nilewe, tamu ya shirika na pesa nitoe?"; unaona mambo haya Mhe. Waziri hazina kama hii leo eti nampenda binti kiziwi, vitu hivi vya zamani mnaviacha. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini katika hili utakwenda huko kwenu nambari yenu hiyo mzitafute hizi hazina, inasikitisha sana kwamba wao nyimbo zao ni za mapenzi tu watoto wa siku hizi, nyimbo za kizazi kipya nyimbo zao wao ni za mapenzi tu hazielimishi sana jamii, mu-*assess* nyimbo hizi mapenzi yakateni wambieni tungeni nyimbo hizi tuelekezeni huku.

Kwa mfano, sisi wakati tunapambana na nduli Idd Amini muziki wa dansi ulitawaliwa na nyimbo Mtukula, Nduli Iddi Amini mbaya kila kikundi unachokwenda, leo sasa hivi tunaelekea kwenye uchaguzi nyimbo ni za mapenzi tu sanaa zao hazielekezi umuhimu wa amani na utulivu katika nchi, tutalinda vipi utamaduni katika nchi kwa nyimbo za mapenzi tu, nampenda binti kiziwi ni tatizo Mheshimiwa. Hawa waelekeze jamii hii, sheria mimi nataka itiwe saini kesho nyimbo za mapenzi wazipunguze watuelekeze katika jamii.

Kuna uchaguzi keshokutwa nyimbo zielekezwe umuhimu wa amani na utulivu katika nchi hii kitu kama hicho ndio ninachokihitaji. Sasa naamini sanaa hapo itakuwa ni kioo ambacho jamii inakitumia na kujirekebisha, wale wanaotaka shari ikiwa kila wakati zile nyimbo za kupelekea amani, za kulinda amani, umuhimu wa amani, wale

walio na hasadi katika nchi watatoa mawazo yale na wataleta mawazo mazuri katika vichwa vyao. Hili naomba Mhe. Waziri sanaa yake ituelekeze huko.*(Makofi)*

Sasa niende katika kuratibu na kuweka utaratibu wa zawadi kwa wasanii wanaoleta heshima. Mtu kama Bi Kidude, Fatuma binti Baraka almaruhum kafika mbali sana kuinadi Zanzibar, leo sidhani hata kama familia yake pale wametengenezewa jambo hivi la kukumbukwa, sidhani kama hilo limetokea. Mimi nadhani katika hili tujitahidi sana, mtu kama Dokta Ayoub aliyekuwa anafanya sanaa za maigizo wengi hawamjui humu watoto wadogo wadogo, Dkt. Ayoub alikuwa akifanya vitu vikali vikali hapa hatumjui tena.

Juzi nazungumza na jamaa wananipigia kutoka hizi nchi za Ghuba wamefurahishwa sana na usanii wa Halikuniki pamoja na Bi Tele, lakini na wao wanaweza wakaondoka hivi hivi sijui kama hata watakumbukwa na mtu, naamini sheria hii itakapokuja itawaangalia kina Halikuniki, Bi Tele pamoja na Makombora na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwa *Prof*. Gogo. Mheshimiwa kama kuna mtu anayetumbuiza nyimbo nzuri *Prof.* Gogo kajitahidi sana kule Pemba, maana yake nakwambia alizama chini kuitoa lulu akaileta juu, ndizi kaikata sijui mgomba si wake, alimuradi ninavyokwambia Mheshimiwa leo *Prof.* Gogo tunaaza kumsahau hivi hivi. Hata kile kikundi cha Tumbe nacho kimefanya kazi nzuri kilichokuwa cha Mhe. Rufai hapa nacho kishaanza kupoteza nyimbo zake hazijulikani tena alimradi mimi naona wasanii hawana raha tu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije kazi za Baraza kwamba Baraza litafanya kazi zake kwa mujibu wa masharti yaliyotolewa na kanuni na litatoa vibali na leseni. Hapa kifungu cha 2 kinasema kwamba kuna mambo ya kibali kwa vikundi vya wasanii na taasisi nyengine zinaenea kuonesha sanaa zao Zanzibar. Hivi vibali kutoa ni muhimu sana na hapa ilipowekwa hii imetusaidia sana kwamba lazima vitoke vibali ndio papigwe densi si jambo geni.

Sisi katika *Afro* Shirazi tulikuwanacho kipengele hiki, tulikuwa na *presidential decree* ambapo ilikuwa husubutu kupiga ngoma bila ya kupata kibali cha serikali. Sasa siku moja tulipata tatizo kidogo naomba mnisikilize umuhimu wa hiki kifungu.

Mhe. Naibu Spika, kuna kipindi pale Kidongo Chekundu palikuwa panataka kufanywa Fete na Fete huandamana na ngoma nyingi, sasa Mzee Karume alikataa kutoa kibali kuwa isifanyike ile Fete kwa sababu tu ya karibu na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Basi akatokea muasisi mmoja na Mzee Karume alikuwa kaondoka kenda Dar es Salaam kidogo, akasema fanyeni bosi hayupo, akatoa amri ifanyike pale miongoni mwa sisi waasisi.

Sasa bwana ikapigwa Fete pale na mabendi, matarabu Kidongo Chekundu pale, kilichotokea wendawazimu miezi sita wao wanacheza mabeni tu, siku moja iliwahangaisha karibu miezi sita wewe ukifika hawalali wanakula rumba tu wendawazimu. Sasa hili ni tatizo lilitutokezea katika mwaka 1971 Kidongo Chekundu pale.

Kwa hiyo, umuhimu wa kutoa vibali tena kwa kuangalia maeneo wasije wakatoa vibali Kidongo Chekundu wendawazimu wakaja wakacheza beni usiku wa kucha, mchana wa kutwa au mwezi mzima ikawa wendawazimu wanacheza beni tu, mchague pahala pa kutoa vibali.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kumtaka Mhe. Waziri hii sheria tukijaaliwa itapita lakini vile vile hivi vikundi viangaliwe sana na msiangalie sana vikundi vya ngoma tu, muangalie na hivi vikundi vya sanaa ya uandishi ambapo sanaa ya uandishi sasa hivi Zanzibar imeanza kupotea sana, hawawi *facilitated* hawa. Dkt. Said Ahmed katunga kitabu chake sasa hivi yuko Ujerumani, wao hawapati kupeleka kwenye mitihani vitabu vinatoka Bara tu vya kufanyia mitihani ya *'O' Level* na nyinyi museme kule kwamba hawa wasanii wetu nao vitabu vyao viingizwe katika mitihani. Watunzi wanatunga vitabu vizuri leo kila kitabu kinachokuja kufanyiwa mtihani wa *'O' Level* na *'A' Level* ni kutoka upande mwengine wa nchi na hawa mnawavunja moyo na wanaacha kazi za uandishi. Kwa hivyo, naomba sana na hawa wasanii vitabu vyao viingizwe katika Baraza la Mitihani ili wapate moyo wa kuweza kufanya kazi zao za sanaa.

Baada ya maelezo hayo nimalizie katika kulinda mila na silka za kizanzibari, ili mtu acheze muziki si lazima acheze nusu uchi lahasha. Hapa palikuwa na ngoma inaitwa Tuntulanga, Tuntulanga Mheshimiwa ilikuwa unavaa koti, tai, mwavuli, unakwenda pale na koti yako na tai unacheza Tuntulanga na watu wanafurahia sio lazima ucheze nusu uchi. Walikuwa wanacheza Tuntulanga kinamama wamevaa mahijabu wanaita vizero siku hizo sasa hivi ndio mnaita nikabu, wanavaa na mabaibui yao ya kamba wenyewe wanapita mule na mashada yao ya maua wanacheza

Tuntulanga, huku tukiwa tumefurahia sio kutuchezea nusu uchi hili ni tatizo. Mimi nadhani miongoni mwa sheria ya adhabu iwekwe huku mbele, iongezwe sheria ya adhabu kwamba kikundi chochote kitakachocheza, kitakachokuwa hakikufuata mila na silka za kizanzibari basi kifungiwe; lazima wa-*regard* na mambo haya ya mavazi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya watu wa Jimbo la Wawi wakiwa Mortuary pale, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mawazo yangu katika mswada huu wa kutunga sheria mpya ya Baraza la Sanaa. Vile vile nichukue fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Aza Wajalla kutujaalia afya njema na uhai leo tukiwa tunaendelea katika kutekeleza majukumu ya nchi yetu. Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kutuletea mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme tu kwa kweli mswada unaonesha dhamira njema katika kuweka nchi yetu katika hali ya utamaduni na ustaarabu uliokuwa mzuri wa nchi hii. Kabla sijasema lolote nitaonekana kama labda natoa pongezi zaidi lakini ndio ustaarabu na uungwana, wenzako wanapofanya matendo mazuri basi kuwashukuru sio vibaya.

Nataka nimpongeze sana Mjumbe ambaye amekaa hivi punde Mhe. Saleh Nassor Juma, kwa kweli mawazo mengi aliyoyachangia ni mambo ambayo nyuma tulikuwa tukiyatekeleza lakini katika zama za karibuni mengi yameanza kutoweka na kuharibu utamaduni wa nchi hii. Wamejaribu kuyazungumza wengi tu ambao walikuwa wakifanya mambo ya tamaduni mbali mbali, lakini lengo na dhamira ilikuwa ni kuutangaza utamaduni na kuweza kuweka nchi yetu katika hali ya usalama, utulivu na amani na akatolea mfano wasanii wengi.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa wasanii aliowazungumza pia aliweza kumtambua Almarhoom Kapteni Mwadini Pandu na akasema wengi hawamtambui, lakini kwa kweli ndugu yetu Mwadini tunamtambua ni msanii ambaye aliweza kuihamasisha nchi katika mambo mbali mbali ya kitamaduni. Tunamtambua alikuwa ni mkaazi wa eneo la Amani Freshi hadi kufariki kwake alifariki katika eneo hilo hilo la Amani Freshi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo ndogo ya pongezi mimi nataka kusema kitu kidogo, kweli sasa hivi vijana wengi wa kizanzibari wamekuwa rahisi kuiga mambo ya nchi za kiulaya, labda wao imani yao ndio kwamba tamaduni ambazo wanahisi zinaweza kuwapeleka mbele au kuleta taswira katika nchi yetu. Mimi nafikiri kuna haja ya kujifunza kwa nchi za wenzetu kama jirani, nchi ambazo bado zinaendeleza tamaduni zao na tamaduni zao zimekuwa zinawajengea sifa hususan katika masuala ya kivazi. Hii inapelekea hata akiwa nje ya nchi yake mtu yule kuweza kumtambua kwamba huyu ni mtu ambaye ana asili kutoka wapi.

Mhe. Naibu Spika, watu wa Nigeria kadiri unavyokwenda wanajitahidi kutunza utamaduni wao katika suala la kivazi na ukimuona tu huyu mtu utasema huyu Mnaijeria.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri katika kazi za Baraza mimi nilipata bahati ya kusafiri na Mhe. Ismail Jussa kwenda Burundi na kwa kweli tulifikia pahala tukajifunza namna ya kinamama wa Burundi wanavyoenzi tamaduni zao, yaani kwa vile vivazi. Burundi ukiwaangalia namna wanavyovaa unavutiwa na yale mavazi yao pasipo na yale matarajio ya wengi, watu wengi wanahisi labda kuvaa vivazi ambavyo havistahiki vya nusu uchi basi ndio vivazi vinavyoweza kuwavutia watu na kuona kwamba labda wamevaa vizuri lakini sivyo hivyo, watu wanavaa vivazi tu.

Burundi kule nguo wanazovaa utashangaa, mtu anavaa lemba na kanzu inaburura huku kwetu mavazi kama yale tunakuwa tunavaa ule wakati wa harusi tu. Bi harusi wa Zanzibar ndio anapovalishwa yale makanzu makubwa, kanzu imetandawaa mpaka mtu nyuma anaikamata lakini wenzetu ni mavazi ya kawaida na ni mavazi ambayo kwa kweli kila mtu anakuwa anasifia kwa namna nakshi zake zilivyosanifiwa.

Sasa ni vyema basi na sisi tukarudi katika zile asili zetu za kuvaa vivazi ambavyo vinatuweka katika mazingira mazuri na zinavutia na kuweza kuitangaza Zanzibar juu ya hali halisi ya utamaduni wetu ulivyo.

Jengine ambalo nilitaka nilizungumzie nilipokuwa nikipitia Ripoti ya Kamati ya Mwenyekiti, katika ripoti hiyo Mwenyekiti kuna pahala amewasilisha kwamba kuomba au kutaka sheria hii basi itumike mpaka katika maeneo ya kambi, zile ambazo huwa zinapigwa mambo ya *disco* na mambo mengine. Mimi hili nataka tuliangalie kwa kina

sana, kwa sababu kambi nazo zina taratibu zake na kambi wana sheria zao za kikambi. Kwa sababu moja ya sheria za kambi kama sikosei baada ya kazi nzito wanahitaji mambo ya kuburudika na ndio maana hata wanapata *exception* katika masuala mbali mbali ya vinywaji. Kwa sababu inakuwa ni moja katika shughuli zao kutokana na uzito wa kazi zao. Sasa tunapoanza kusema kwamba sheria hii itumike katika maeneo ya kambi, mimi nafikiri tutafikia pahala tutakuja kukosana na maaskari.

Mimi nilikuwa nina wazo moja tu katika hili, ni kweli baadhi ya kambi sasa hivi wanazidi mipaka ya yale mambo yao sasa nafikiri tusingewawekea sheria ya kufuata sheria hii, lakini nafikiri kuna haja ya kuwaongoza katika namna ya kutumia kambi zao. Nafikiri ndio wanasema kwamba mambo ya serikali hii yanavyopangwa watu wa siku hizi wanakuwa wanakwenda kinyume na yale makusudio ya zile sheria ambazo zimewekwa.

Mhe. Naibu Spika, hapa kinachoonekana sasa labda yale ndio malengo ya starehe katika kambi, sasa hivi yamekuwa yameingiliwa na raia na hili ndio tatizo, kwamba raia wanakwenda kuingia kwenye kambi kufanya starehe ambazo hivi sasa yanazidisha kasi ya kufanya hayo mambo.

Sasa mimi nafikiri kulikuwa kuna haja ya kupiga marufuku raia kwenda kufanya starehe kwenye kambi na tukawaachilia wenyewe wenye kambi kuendesha mambo yao, vyenginevyo hili suala linaweza likaja likatuweka pabaya na wananchi wakafikia pahala wakaja wakaleta malalamiko kwamba sisi tunazuiliwa na kambi hazifuati taratibu.

Sijui kama kuna mtu ana uwezo wa kuingia kwenye kambi kwenda kuzuia lisipigwe *disco*, sijui; kwamba wewe mtu ambaye huna silaha kambi tunajua ulinzi wake na silaha zake. Sasa tusijetukaweka jambo ambalo baada ya kutengeneza likaja likaleta shari baadae. Mimi nafikiri tungeandaa sheria au tungetafuta kifungu na kutafuta namna ya kufanya masuala haya katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, la zaidi mimi nahisi kwamba tatizo sio kupigwa *disco* au tatizo sio kufanya mambo ya kileo katika maeneo, mimi nafikiri kuna tatizo moja tu na nimejaribu kuangalia mswada huu hili sijaliona na nataka Mhe. Waziri atusaidie alitafutie namna ya pahala pa kuliweka.

Tatizo tunalokosea kwa bahati mimi nilipata bahati ya kwenda Uturuki na mimi ni kijana, nilipofika baada ya kufanya shughuli zangu nilitafuta pahala pa *disco* kwenda ku-*fresh mind* baada ya shughuli nzito za mikutano yangu ambayo niliendea kule. Watu wengi hapa wamepiga kelele kwamba *disco* zinaendeshwa katikati ya mji, tatizo sio katikati ya mji.

Mhe. Naibu Spika, Uturuki madisko yako mjini kabisa, lakini kinachosaidia na nafikiri hili ndio tatizo kwamba yale majengo yenyewe yamejengwa katika mazingira ya ki-*disco*. Sasa tatizo letu sisi yale mazingira ya majengo hayako ki-*disco* na ndio maana linapigwa *disco sound* yake inakera mtaani, inakera na zaidi ya mtaa mwengine wa pili yake.

Mhe. Naibu Spika, unapita chini ya mlango lakini hujui kama hii ni kumbi ya *disco*, kwa sababu kumbi ya *disco* iko *underground* na kumejengwa na milango hakuna mambo ya madirisha hata milango yake haiwezi kutoa sauti nje, huwezi kujua utachokijua wewe ni baada ya kuona *slogan* kwamba huu ni ukumbi wa *disco.* Sasa hilo ndio tatizo, mimi nafikiri tungetafuta namna ya kuweka kipengele cha sheria kwa wale ambao wanataka kuweka kumbi za *disco* basi kumbi ziwe na namna maalum ya kuweza kuhifadhi sauti nje isitoke.

Mheshimiwa Bwawani iko mjini lakini hebu kaa nje ya Bwawani nani atajua kama Bwawani kuna *disco* labda wawe wanapiga juu wale, lakini wakipiga kwenye ukumbi wenyewe kule chini sauti haitoki Sasa wale wanaopiga juu kule ndio wanaonfanya ghasia Mhe. Ismail Jussa. Lakini ile kumbi yenyewe iliyotengenezwa kwa mazingira ya disko Bwawani haitoi sauti, unapofunga mlango na kuingia hiyo *sound* kidogo inatoka sekunde mmoja au mbili kazi imekwisha.

Sasa mimi nafikiri tungetafuta kipengele lazima kumbi za *disco* ziwe kumbi maalum ambazo zinastahiki au zina ubora wa kufanya hilo *disco* lenyewe. Lakini vyenginevyo kwa kusema kwamba tuzuie huku tuzuwie huku kwa mazingira ya majengo yetu .

Mimi nafikiri itakuwa tabu na kwa kusema kwamba tusiweke ma-*disco* katikati ya mji, sijui tutaweka wapi. Kwa sababu huo mji wenyewe sasa hivi umeshafika mpaka Jendele, sijui wapi sasa, ili watu waweze kulifatilia, kwa sababu mji sasa hivi umepanuka na mji umekuwa mkubwa.

Kwa sababu zamani tunafahamu maeneo ya *disco* yalikuwa maeneo maalum lakini kutokana na mazingira ya mji wenyewe yalikuwa yanastahiki, utaambiwa unde Maruhubi lakini Mahuruhubi kwenyewe sasa hivi pia kumeshakuwa mjini.

Mimi nafikiri Mhe. Waziri tuje katika namna ya kutafuta vipengele vya kuandaa mazingira katika maeneo yale ya kumbi za *disco*. Nalo hili ndilo linalotupelekea kwamba kila mtu akishazungusha ukuta wake anakwambia kumbi ya *disco*, sasa hili ndio tatizo. Lakini kungekuwa na sheria ya kumbi za *disco* mtu ambae anataka kutengeneza kumbi ya *disco* basi apate kibali kwa kufuata utaratibu wa nama gani hiyo kumbi inaweza ikawepo.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka niende kwenye mswada yenyewe baada ya dibaji ndogo na ushauri kwa Mhe. Waziri. Nina imani kwamba hayo ameyasikia na kwa ninavyofahamu jinsi ya umahairi wake na utendaji wake wa kazi basi mengi anaweza akayachukuwa kwa kusaidia taifa hili, kuepukana na ukosefu wa maadili ambao sasa hivi ndio unatuvunjia heshima nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niende katika ukurasa wa 291, Kazi za Baraza. Katika ukurasa huu napenda ninukuu kwa ruhusa yako vifungu viwili, kifungu (h) na (n) halafu nataka nitowe na mawazo yangu, kinasema;

> (h) "Kuweka Utaratibu mzuri wa kuwatambuwa, kuwapatia tunzo wasanii wa zamani ambao wamechangia maendeleo ya kazi za sanaa Zanzibar".

Nashukuru na nampongeza Mhe. Waziri kwa kuleta kifungu hicho, kinasema;

> (n) "Kuratibu na kuweka utaratibu wa kuwazawadia wasanii waliolileta heshima taifa kwa kazi zao nzuri za Sanaa".

Ni mambo mazuri ambayo yameletwa lakini sasa mimi ningeomba Mhe. Waziri atafute namna ya kuengeza kifungu kwa sababu tunaweza kuwapa tunzo katika yale mazingira ya kazi zao, kwa kazi nzuri walizofanya lakini pia utaratibu wa namna ya kuzawadia tutawapa zawadi. Lakini kinachoonekana na ndilo labda Mheshimiwa Mwana Afro Shirazi hapa Mwalimu Saleh, ambalo alilipigia kelele kwamba wasanii mara nyingi wanatumia nguvu katika ujana wao ndivyo ilivyo lakini matokeo yake wanapoteza nguvu katika utuuzima wao.

Sasa mimi nafikiri zawadi pamoja na nishani bado haijawa nguvu zaidi katika kumuenzi msanii na ndio maana akajaribu kutoa mifano kwa aina Bi Kidude kuitangaza Zanzibar ndani na nje ya nchi. Lakini mwishowe anamalizia katika hali gani. Sasa nafikiri kungewekwa kifungu ambacho kitasaidia namna ya kutafuta namna. Nafikiri ingekuwa labda kuwaenzi na kuwatunza, kwa sababu watu hawa mara nyingi wanamalizia maisha yao katika hali za uduni hata mtu akipata maradhi ile kumuenzi na kumfanyia matibabu.

Mhe. Naibu Spika, tunaona hapa na tunafahamu kwamba wengi wa viongozi basi wanapofikia pahala wakapata matatizo namna ya kumtunza ile hali yake ya kiafya inafika pahala unaambiwa kwamba mtu huyu kwa heshima yake basi itabidi tumsafirishe akatibiwe India au Ulaya.

Sasa nafikiri hawa nao tungewaekea kifungu cha kuwaenzi na kuwatunza, maana yake mtu unapomuenzi na kumtunza inabidi katika uhai wake wote anaomalizia. Nafikiri Mhe. Waziri ungetafuta namna ya kukitengeneza hiki kifungu cha namna ya kuwaenzi na kuwatunza katika maisha yao, kwa sababu pale inakuwa ule muda wa usanii ameshamaliza kabisa nguvu hana. Sasa namna ya kumuenzi na kumtunza ili kutoa nguvu kwa vijana nao kuona kwamba serikali yao inawajali katika ule wakati ambao walitumia nguvu zao katika kuitangaza ndani na nje Zanzibar, sasa hilo ndilo nilikuwa nataka kueleza.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka nizungumzie katika hizo hizo kazi za Baraza katika kifungu kidogo cha pili. Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu kidogo;

"Baraza litafanya kazi zake kwa mujibu wa masharti yaliyotolewa na Kanuni na litatoa vibali na leseni zifuatazo:"

Hapa leseni zimeandikwa kwa mtiriiko wake, (i-v) kibali cha vikundi vya usanii na Tasnia ya kuonesha. Sasa mimi nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri tatizo sio vibali tatizo ni ufatiliaji wa vibali. Sasa kuna kifungu huku mbele katika huu mswada kimeelezea namna ya kuajiri Maafisa pale ambapo bodi itakapoona kwamba inafaa.

Sasa mimi nafikiri ni vyema na kulingalia hili zaidi tatizo linaloonekana hata sasa hivi kufatilia wale watu ambao wanapiga ngoma kwamba wana vibali au hawana, kama sikosei labda wana mtu mmoja tu Zanzibar nzima. Sasa inakuwa ni tatizo kuweza kujua huyu anaefanya hii shughuli ameruhusika kisheria.

Sasa mimi nafikiri pia kuna haja pamoja na kuwa mswada mzuri na sheria hivi ilivyoandikwa; kuna haja namuomba Mhe. Waziri baada ya kutafuta mikakati ya kuandaa Maafisa wa Leseni, kufatilia hizo kazi zao. Tunaona sio kwenye Sanaa Mhe. Naibu Spika, hata kwenye biashara za kawaida Baraza la Manispaa linapata tabu sana, kwa sababu hizo sheria zimetamka kwamba kila anaetaka kufanya biashara basi aende akakate leseni katika taasisi inayohusika, iwe Baraza la Manispaa au Halmashauri lakini kutokana na uzito wetu, kutokana na mazonge ya wananchi wetu huwa hizi taratibu hawazifati.

Sasa Baraza la Manispaa huwa wanafanya misako maalum kwa wakati maalum. Sasa Mhe. Waziri nafikiri hili namuomba tu awe na usafiri uliokuwa mzuri na ambao utakuwa ni mkakati mzuri wa kushikirikiana na baadhi ya taasisi kwa mfano Masheha na Polisi ili wale Maafisa wao wasipate matatizo wanapokwenda katika yale maeneo kwenye kufanya uchunguzi kwa wale ambao hawana vibali. Sasa hili nalipongeza kwa namna alivyolileta lakini namuomba kwamba aandae mikakati ya kuhakikisha kwamba utekelezaji wake unakuwa mzuri.

Mhe. Naibu Spika, chengine ambacho nitakachokizungumzia katika mswada huu ukurasa wa 292, Uwezo wa Baraza Mhe. Naibu Spika, pana kifungu hiki (c) naomba nikinukuu kidogo halafu nimshauri Mhe. Waziri, namna ya kuweza kukisaidia.

(c) "Kuzifanyia Sensa filamu au *cassette* za video yoyote kama *CD, DVD,HDV* na kitu chengine chochote kinachohusiana na hivyo ambavyo zimerikodiwa ndani au nje ya Zanzibar kwa lengo la kuoneshwa hadharani".

Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo naona pana udhaifu ambao unaweza ukatukwama kwa wakati tulionao sasa hivi katika hili neno la mwisho la "Kwa lengo la kueneshwa hadharani".

Mhe. Naibu Spiaka, watu sasa hivi wamekuwa wajanja na sheria imezungumzwa hadharani. Sasa hivi watu wanajenga mabanda na mabanda yale huwa yanaoneshwa video na mambo mbali mbali na *cassette* nyengine huwa haziko katika mazingira mazuri. Sasa mtu akiwa yuko ndani na akakionesha kile kitu ndani na wewe umeshakionesha hadharani, sasa mimi kidogo napata mashaka hapa.

Sasa nafikiri hapa tungetafuta namana ya kuweza kuzuia kama itaandikwa kuwa hadharani atafute neno zuri la kuweza kulisaidia hili. Vyenginevyo ukisema hadharani tu kidogo inaweza kuwa likaleta tabu katika uendeshaji wa sheria hii kutokana na mazingira tuliyokuwa nayo sasa hivi. Tunajua kuna mabanda mengi tu kama utafanya utafiti Mhe. Waziri mpaka sasa hivi kuna watu wanaonesha filamu za *X* ndani ya majumba yao. Sasa ndani ya nyumba inakuwa mtihani watu wanaingia wao, wanajua tu kwamba nyumba hii kuna mtu anafanya biashara hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie tu kwa kuchangia mswada huu katika ukurasa wa 296 kwenye kifungu cha 26, Ada na Malipo.

Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu tu kifungu hiki;

"Kila kikundi cha Utamaduni kitalipa gharama za huduma kwa Baraza kama zitakavyoainishwa na kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii."

Mhe. Naibu Spika, napongeza suala hili lakini nataka akija Mhe. Waziri hili anisaidie kidogo kwa sababu kwa ufahamu wangu kwamba ada za gharama za huduma hizi, zamani kama sikosei zilikuwa zinalipwa na mwananchi

mwenyewe ambaye anataka kufanya huduma kwa mfano kupiga Rusha roho, yeye anapata barua kwa Sheha halafu anakwenda Baraza la Sanaa kulipa, ili apatiwe ile huduma. Lakini sheria hii au mswada huu inaonesha kwamba kikundi chenyewe ndicho itabidi kiende kikalipe na kutoa huduma.

Sasa hapa ningeomba kama kitakuwa kimekaa hivi basi sina matatizo na kifungu kilivyokaa, lakini ni kwamba ningeomba Mhe. Waziri kuona umakini kwa wale ambao wanatoa huduma na tayari wameshalipia, kwa sababu mtu anaweza akalipia na akeshalipia maana tayari umeshampa nguvu ya kisheria kupeleka huduma. Lakini tatizo pale unapopeleka huduma ikawa wananchi wa eneo lile hawako tayari ile huduma inayotaka kufanywa katika eneo lile. Zamani utaratibu ulikuwa nzuri, sasa pia pamoja na hayo yule mtu ambae anataak kutoa huduma pia basi nafikiri kuna haja pia ya kupata baraka kwa Sheha anaehusika, ili ile huduma pale anapoenda kuipeleka wenyewe wale wawe wako tayari kufanyiwa huduma ile.

Sasa hili nafikiri ni suala ambalo tuwe makini katika kuliangalia tutafute kitu cha kuendelea. Vyenginevyo anakwenda analipa na watu wetu hawaoni tabu kulipa kwa sababu yeye anapolipa anajua na yeye anapata faida. Yeye itakuwa kazi yake ni kuongeza thamani tu katika ile huduma, kama zamani rusha roho ilikuwa laki moja, akiaambiwa huku atoe elfu ishirini atasema sasa hivi rusha roho ni laki na ishirini. Kwa sababu anajua ishirini zinakwenda kwenye huduma na laki moja anapata yeye katika kujipatia riziki yake.

Mhe. Naibu Spika, hili nataka nimueleze Mhe. Waziri kwa ushahidi kabisa, karibuni katika maeneo yangu ulitokezea mgogoro kama huu, wananchi kwa bahati hawakufata utaratibu wa kwenda kuomba kibali kwenye Baraza la Sanaa na Sheha hakuliulizia lile suala. Lakini alifika Afisa wa Baraza la Sanaa kuja kuulizia na alipoona watu hawana kibali sasa tatizo lilikuwa hapa, vikachukuliwa vifaa vya aliyetoa huduma vikazuiliwa Polisi lakini walipofika Polisi yule analalamika anasema mimi nimekodiwa, suala la kodi liko kwa mwenye kodi kuomba barua kwa Sheha, kwenda kukata kibali Baraza la Sanaa, sasa tatizo liko wapi.

Basi kule polisi akaambiwa kuwa sisi hatutoi vitu mpaka hao waliokukodi uwalete, sasa hapo kukawa na ugomvi kwa aliyekodiwa na waliomkodi. Anawaambia muende Polisi mkaripoti ili vifaa vyangu niweze kuvipata na kule ili wavipate wana faini zao Baraza la Saa, kama hujakata kibali unapigwa faini. Sasa faini kubwa yule aliyetoa huduma anasema mimi gharama hizo sitoi, kwa sababu nikitoe faini zile pesa mlizonikodi hazitoshelezi.

Sasa pakawa pana sokomoko kubwa sana katika hili na ndio maana Mhe. Waziri atafute namna ya kuliweka sawa katika kuona baina ya mtoa huduma na wanaotolewa huduma nani hasa zaidi anastahiki kukata kibali, vyenginevyo tuseme wote wawili ili wapate ridhaa ya eneo kwamba kweli ile huduma inatakiwa ifanyike. Sasa nafikiri tukiwaweka wote wawili tunafanya suala moja la msingi wasije kukera watu wa mitaani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machahe nakushukuru na naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Kwahani nakushukuru, Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii tukawa tuko hapa kwa kupitisha Mswada huu ambao umetugusa wananchi sote.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo na Uvuvi. Pia niwapongeze wadau waliopitia mswada huu kifungu hadi kifungu na kuweza kuufikisha hapa mbele ya Baraza la Wawakilishi.
Pia nisisahau kumpongeza Mhe. Waziri kwa mashirikiano ya pamoja kuweza kutekeleza majukumu yetu ya wizara. Pia niwapongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Bodi ya Sensa na filamu wote, nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kutoa ufafanuzi mdogo kuhusu Mheshimiwa wa Jimbo la Mtambile, amezungumzia kuwa Utamaduni una maana gani.

Utamaduni unaendeleza mila, Silka na Utamaduni wetu wa Kizanzibari na kuweza kuendeleza na kuudumisha, ili wananchi waweze kuona kama utamaduni huu ni utamaduni wetu wa asili.

Pia niende kwa Mhe. Wanu Hafidh Ameir, yeye kwa kweli ameeleza mambo mengi; ameeleza kuhusu vijana wetu ambao wanakwenda kwenye mabaa ambayo hayastahiki kwenda. Ni kweli Mhe. Wanu Hafidh Ameir tunajua

kwamba watoto wetu kama tunavyowajua watoto wetu hawawezi kutusikiliza pale tunapowaambia, hilo ulione na mtu hawezi kwenda pahali bila ya kuona kitu.

Kama tunavyosema utamaduni wetu tuuenzi mtu yeyote yule hawezi kwenda pahali kama hakuona kitu kile ambacho kimemvutia, na kama tunavyojua sasa hivi watoto wetu kwa kweli wanapotoka maadili yetu sio sisi wazee lakini watoto wetu pale unapoambia nendeni hapa hawendi, kwa kweli nawaomba sana Waheshimiwa wenzangu muone hilo, ni suali ambalo limetugusa sote.

Pia, niende kwa Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Mheshimiwa huyu nampongeza sana kwa hekima zake na busara zake na amefafanua vizuri. Ni kweli Mheshimiwa kuna historia nyingi za zamani, wazee wetu walikuwa wanatupa historia, wanatupa hadithi hata kwenye utamaduni wetu kuna kitu kama adabu za kula. Kwa kweli ili ukitaka kula lazima uwe umekaa vizuri na unaweza kula na wazazi wako huwezi ukatoelea mwazo, lazima tuseme ukweli wazee walikuwa wanatufundisha. Kinapowekwa chakula huwezi kunawa mwanzo, wala huwezi kula ukatoelea mwanzo, lazima kitoweo ulikuwa unaweka kwa mkono wa kushoto. Nakumbuka yote na sisi tulielimishwa na wazee wetu. Kwa kweli tulikuwa tunakikamata mkononi hivi hivi kitoweo mpaka umalize kula unaondoka nacho.

Sasa nawaomba sana Waheshimiwa wenzangu kama mnavyojua mswada huu umegusa vipengele mbali mbali kuhusu matatizo, maendeleo; mifano mingi inetolewa hapa na Waheshimiwa hata Mheshimiwa Muasisi kwa kweli amezungumzia mambo mengi ambayo yametugusa na Mheshimiwa Muasisi nampongeza sana kwa juhudi zake na kuweza kutuelimisha mambo mengi ya wasanii ambayo amewataja kama Siti bint Saadi.

Mhe. Saleh nakuhakikishia kwamba Siti bint Saadi kuna kijukuu chake kama unataka kukiona pia utakiona na kijukuu chake kunaimba vizuri kama ile nyimbo uloghani pale.

Waheshimiwa Wajumbe kweli sitokuwa na mengi sana isipokuwa niwashukuru na niwaombe sana mswada huu tuupitishe kwa sababu mswada huu umelenga sehemu mbalimbali na unatugusa sisi viongozi na mswada huu utakapopita nyinyi viongozi mliomo humu ndio, muweze kuisimamia isijefika pahali kuna kijana amefanya matatizo nyie mnakwenda kumkingia kifua. Lakini muone tu kama sheria hii inafuata mkondo wake.

Halafu mmezungumzia sheria ya mavazi, sheria hii ya mwaka 1973 ipo. kila siku kama tunavyoeleza kwamba sheria ipo lakini inafanyiwa marekebisho pindipo Mwenyezi Mungu akitujaalia kama tutarudi tena kwenye Baraza hili au ni kipindi hiki hiki atakaekuja humu ataichangia na ataweza kuifatilia na itaweza kutekeleza majukumu yake.

Naunga mkono hoja, ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri kwa mchango wako nakuunga mkono hoja. Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa ushirikiano wenu mlionipa jioni hii. Lakini kabla sijaakhirisha nina matangazo mawili.

(1) Kesho tuna Semina tunakujafanyiwa na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ratiba yao inaanza saa 2:30 wafike Wajumbe na saa 3:00 Mhe. Spika, atafungua. Tunaomba sana asije Mhe. Spika, akajakufungua Semina mna watu 6; kwanza tutawavunja moyo na wataona kuwa hatukuwathamamini . Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa tuje mapema kwenye semina.

(2) Jumapili pia tuna semina katika ukumbi wetu huu wa Baraza, pia tuje mapema saa 2:300 ili saa 3:00 tuweze kuanza.

Baada ya hayo Mhe. Waziri atafanya majumuisho Jumatatu tukijaaliwa baada ya masuala na majibu. Naakhirisha kikao chetu hadi siku ya Jumatatu tarehe 16/3/2015 saa 3:00 asubuhi.

(*Saa 1:22 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 16/3/2015 saa 3:00 asubuhi)*